

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 15 Novemba, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MHE. SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge imelazimika tutawanye orodha mpya ya shughuli za leo kwa sababu iliyopita iliyokwisha tawanywa ina makosa. Kwa hiyo, mzingatие hii sasa. Kwenye orodha hiyo katika hati za kuwasilisha mezani, ni pia Mheshimiwa Naibu Spika, kuwasilisha Rasimu ya Kanuni za Bunge. Ni jambo muhimu la Kikatiba na lilikuwa limeachwa. Kwa hiyo, Katibu kwa orodha ya shughuli za leo.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU SPIKA:**

Taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge Kuhusu Mapendekezo ya Kanuni za Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Dhamana ya Uwekezaji Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2006 [*The Annual Report and Accounts of the Unit Trust of Tanzania for the year ended 30th June, 2006*].

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Twiga Bancorp kwa Mwaka wa Fedha 2006 [*The Annual Report and Accounts of the Twiga Bancorp for the Financial year, 2006*].

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 173

**Ahadi ya Maisha Bora kwa Kila Mtanzania**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya awamu ya Nne iliwaahidi wananchi maisha bora kwa kila Mtanzania:-

Je, Serikali imefanikiwa kwa kiasi gani kutekeleza ahadi hiyo kwa watanzania?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (DR. BATILDA S. BURIAN) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa napenda kukiri kwa dhati kuwa, Ni kweli kwamba Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005/2010 inatamka wazi azma ya kuhakikisha maisha bora kwa kila Mtanzania yanapatikana. Azma hii Mheshimiwa Spika, imetafsiriwa kwa vitendo katika programu, mikakati mbalimbali ya Serikali, lengo ni kuhakikisha kuwa fursa za kiuchumi zinaongezeka na kuboreshwa zaidi. Upatikanaji wa huduma za kijamii unaimarishwa na kuwafikia Watanzania wote na hasa wale walioko vijijini.

Aidha ajira zimeongezeka na taratibu za uendeshaji biashara zinaboreshwali kutoa nafasi kwa Watanzania wengi kujajiri wenyewe na kuingia katika sekta binafsi. Aidha taratibu za upatikanaji wa mikopo na mitaji inaimarishwa. Kwa ujumla jithada zote hizi zinafanywa ili kuhakikisha kwamba mkakati wetu wa kukuza uchumi na kuondaoa umasikini unatekelezwa kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda ieleweke kwamba maisha bora hayawezi kupatikana kwa mwaka mmoja au miaka miwili. Ni mchakato wa maendeleo ambayo hayapatikani kwa miujiza, bali yanapatikana kwa kujituma na kufanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 mpaka Oktoba 2007, imeonesha kuwa mafanikio yanaridhisha sana. Kwa kipindi hiki Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 21 kwaajili ya dhamana ya mikopo kwa wananchi wajasiriamali kwa ajili ya mikoa yote. Hadi kufikia mwezi Septemba 2007, benki za CRDB na NMB ziliweza kutoa mikopo kwa wananchi yenye thamani ya shilingi billion 21.1.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, maisha bora kwa kila Mtanzania ni pamoa na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma bora za kijamii na za kiuchumi. Katika kutekeleza hili serikali imeongeza bajeti yake mwaka hadi mwaka katika Sekta ya Elimu, Afya, Maji na Miundombinu. Kwa mfano sekta ya Elimu iliongezeka kwa asilimia 53.5, sekta ya Afya imeongezeka kwa asilimia 36.2.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya jitihada hizi ni ya kuridhisha. Idadi ya vyumba vya madarasa ya awali, shule ya msingi na sekondari imeongezeka na hali kadhalika wanafunzi wameongezeka. Aidha Serikali imeandaa mpango maalum wa kuhakikisha kwamba kila kijiji nchini kinakuwa na zahanati na kila kata inakuwa na kituo cha afya ili kuboresha huduma za afya. Kwa kuwa, Serikali imetekeleza na inaendelea kutekeleza miradi, programu na mikakati mbalimbali ili kuwawezesha wananchi kuwa na maisha bora, haitakuwa rahisi kutaja mambo yote hapa. Hata hivyo intosha kusema kwamba Serikali ya CCM ipo makini na kupitia utekelezaji wa mipango yake ya miundo mbinu kwa maana ya sekta ya barabara, ujenzi, uchukuzi na mawasiliano imeimarika na kuboresha huduma zake.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeendelea kujitangaza na kuvutia utalii, biashara, mikutano na makongamano ya kimataifa ili kuongeza mapato na ajira. Serikali imeendelea na programu yake ya kugatua madaraka kwa wananchi kwa kushusha rasilimali na wataalamu kwenye Halmashauri. Na hata masuala ya utawala bora na demokrasia yameimarishwa katika kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya rushwa. Pamoja na kuwa na mchakato wa kuanzisha huduma za msaada wa kisheria ili kuwawezesha wale wasio na uwezo kupata msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kumalizia kwa kurudia maneno ya Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwamba Tanzania yenye neema tele inawezekana, Maisha Bora kwa kila Mtanzania yanawezekana na kila mmoja wetu atimize wajibu wake. (*Makofi*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake marefu. Lakini Watanzania, Maisha Bora waliyoyategemea ni kupata nafuu ya maisha kwa kupata vyakula kwa urahisi, kupata vitu vya ujenzi kwa urahisi, pamoja na usafiri na usafirishaji. Lakini mambo hayo bado hayajapatikana katika Tanzania yetu, Watanzania bado hawajayapata ni magumu, kila siku bei zinafumuka kunakuwa na mfumuko wa bei, vyakula vimepanda maradufu, vitu vya ujenzi vimepanda maradufu na usafiri vile vile umepanda. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusiana na hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shoka Juma, kama ifuatavyo:-

Kwanza nikiri tu kwamba tatizo ambalo linatokea sasa hivi ni tatizo la ulimwengu mzima. Mfumuko wa bei unatokana na kupanda kwa bei ya mafuta hatuna uwezo nao na *control* nao. Lakini kama ninavyosema tunachojenga ni mfumo, mfumo ambao utawezesha wananchi wetu kuijendeza na kuweza kupata manufaa zaidi katika kipato chao na kuweza kushiriki katika shughuli mbalimbali za kujiletea riziki. Tunaweka taratibu kama nilivyosema, kilimo kimeongezeka, tunesema suala la vifaa vya ujenzi, saruji tumeimarisha na tumeangalia kila mahali ambapo kulikuwa kuna kero, tumefanya kila jitihada kuhakikisha kwamba kero zile tunazitatua.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa, hali ya maisha bado ni duni hasa kule vijijini na mikopo inayotolewa mingi inaishia mijini kwa wale wenye nacho.

Je, Serikali inasema nini kuhusu hili kwa wale wananchi wa vijijini ambao wanazidi kutaabika?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Kiwel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Spika, kama yalivyo, majibu ya Serikali ya awali kwamba mwaka jana tulitenga fedha shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kukopesha wajasiriamali wote wa mijini na vijijini, zoezi hilo limekwenda vizuri katika mwaka wa kwanza lakini limekuwa na mapungufu. Moja ya mapungufu ni hilo alilolisema Mheshimiwa Mbunge, kwamba mikopo katika huu mwaka wa kwanza, mingi imekwenda mijini, hilo tumeliona. Tunapoingia awamu ya pili tunasahihisha yale makosa yaliyofanyika katika awamu, mapungufu yaliyofanyika katika awamu ya kwanza. Ambapo mikopo mingi haikufika vijijini. Halafu pili kuna Wilaya ambazo hazina benki.

Kwa hiyo, nazo hazikupata kabisa. Katika mwaka wa pili tunashirikisha asasi za fedha ndogo ndogo, Benki Kuu imesha ainisha asasi 14. Hizi Serikali tutawapa fedha ili wakopeshe, na msisitizo wa asasi hizi sasa ni vijijini katika mwaka wa pili na katika yale maeneo ambayo hayana benki. Benki Kuu inakamilisha maandalizi ya kuziandaa hizi asasi 14 na Waziri Mkuu amesema katika muda wa mwezi mmoja haya maandalizi yaishe ili mikopo ianze. Msisitizo mwaka huu ni vijijini na katika zile wilaya ambazo hazina benki (*Makofi*).

**MHE. GODFREY W. ZAMBI :** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza :-

Kwa kuwa, kundi moja ambalo linajitahidi sana katika kujiletea maisha bora ni wakulima. Lakini kwa kuwa, kundi hili linakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa mbolea Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa ziarani kule Mbeya, alishaahidi kuwaongeza wananchi hawa wakulima mbolea ya ruzuku.

Je, Serikali inatamka nini katika jitihada hizi za wakulima kujiletea maisha bora hapa hapa nchini? (*Makofi*).

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zambi kama ifuatavyo:-

Lakini kabla ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zambi, nilitaka nimpongeze Mheshimiwa Grace Kiwelu, kwa kukiri kwamba mikopo tuliyoianzisha ni sehemu ya kuondoa umasikini ili tuweze kuleta Maisha Bora kwa kila Mtanzania. Huko ni kukubali kwamba tunazo sera sahihi katika Chama cha Mapinduzi.

Kwa swali la Mheshimiwa Zambi, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Mbozi, ni wakulima hodari wanaofanya kazi kwa kujituma sana. Kila nilipopita katika Mkoa wa Mbeya malalamiko ilikuwa ni mbolea mbolea.

Hawa ni watu wanaojiendeleza, ukianza kuona watu wanadai mbolea maana yake wanatambua maana ya maendeleo. Tumewaaahidi kuwaunga mkono, na nina waahidi tutaongeza mbolea na mbolea ya ruzuku itakuwa nyingi zaidi (*Makofii*).

Na. 174

### **Majina ya Mitaa (Streets) na Vijiji**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wananchi wanapopata matatizo kama ya ajali barabarani, ujambazi, majanga ya moto, na kadhalika. Wanapowaarifu Polisi hutakiwa kueleza kwa usahihi mahali tukio lilipotokea:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, lawama zinazotolewa kwa Polisi kwa kutofika haraka kwenye matukio ya ajali sio zao bali ni za mamlaka nyingine?

(b) Je, iko sheria yoyote inayozitaka Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya kuandika majina ya mitaa, vijiji na namba za nyumba?

(c) Je, ni Jiji lipi hapa nchini limefanya vizuri kwa kuwa na majina ya mitaa yote na namba za nyumba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekiel Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo :-

(a) Ni kweli kwamba Polisi wakati mwengine wanaweza kuchelewa kufika kwenye eneo la tukio baada ya kupokea taarifa kutoka kwa wananchi. Hali hii inasababishwa na mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ubovu wa miundombinu kama

barabara na madaraja, umbali mkubwa wa upatikanaji wa maji ya kuzima moto, uchache wa magari na ugumu wa kutambua sehemu tukio lilipo kama mwenye kutoa taarifa hakufika kituoni na kueleza ni mtaa gani tukio hili limetokea.

(b) Mheshimiwa Spika, sheria namba 8 ya Halmashauri za Miji, kifungu namba 14 kifungu kidogo cha 3 kinaeleza kwamba Halmashauri ndiyo chombo chenye mamlaka ya kugawa eneo la Kata katika mitaa kwa kuzingatia idadi ya kaya ziatakazokuwepo katika kila mtaa. Sheria hiyo kifungu namba 55 moja J, kinazitaka Halmashauri, Majiji, Manispaa na Miji kuandika majina ya mitaa na namba za nyumba.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kutoa majina ya mtaa na namba za nyumba, sheria namba 8 kifungu namba 59 E, kinazitaka Halmashauri kubuni na kupanga matumizi mbalimbali ya ardhi. Hii ni pamoja na zoezi zima la upataikanaji wa viwanja, ugawaji na kusimamia uendelezaji wake. Aidha, uendelezaji wa viwanja hufanywa na mtu mmoja mmoja, taasisi, hata Serikali ambapo kila mmoja anakuwa na mipango yake ya uendelezaji kwa nyakati tofauti inayofanya maeneo yasiweze kuendelezwa kwa pamoja na hivyo kuleta ugumu katika utoaji wa majina ya mtaa na namba za nyumba

(c) Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa zoezi la kuweka majina ya mtaa na namba za nyumba, Majiji, Manispaa, Miji zimekuwa na mazoea ya kuandika majina ya mitaa na namba za nyumba hasa maeneo ya katikati ambapo uendelezaji wake umekamilika. Kwa mfano, Halmashauri ya Jiji la Tanga, limeweza kutoa majina 48 ya mitaa na namba za nyumba 22,000. zote zipo eneo la katikati ya Jiji la Tanga.

Aidha, katika eneo la katikati ya Manispaa ya Dodoma, mitaa yenyewe majina 70 na baadhi ya nyumba katika maeneo hayo tayari zimeshapewa namba. Jiji la Mwanza limeandikisha mitaa 481, Jiji la Dar-es-Salaam, mitaa 185,361. Kwa hiyo, Jiji la Dar-Es-Salaam, ndilo linaloongoza kwa kuwa na mitaa iliyoandikwa majina, lililoandikwa majina mengi na limeandika majina ya mitaa jumla 186,361.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba na kuwataka wananchi wasiondoe mabango yanayoonesha majina ya mitaa bali wayalinde mabango hayo yanayowekwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwani yanawekwa kwa lengo la kuwajulisha watu mbalimbali, wakiwemo wageni wanaotembelea miji yetu, askari wanaotoa huduma za dharura majina, ili wajue majina ya maeneo ya mitaa mbalimbali.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza:-

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, nadhani atakubalina na mimi kwamba suala la alama linagusa taasisi nyingi sana katika utekelezaji wake. Hospitali kama kuna mgonjwa kuna ajali, sasa katika kuangalia jinsi Halmashauri zinavyofanya kazi, unaona wazi kabisa kwamba suala la alama halina hata Bajeti.

Je, Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba katika Bajeti ijayo, kila Halmashauri iweke kitengo cha alama?

Na kumbuka Jiji la Dar-Es-Salaam, lilikuwa na kitengo cha alama, lakini kilikuwa hakina uwezo, mpaka Ofisi ya Waziri Mkuu wakati huo, tukiwa na Mheshimiwa Anna Abdallah na Mheshimiwa Lowassa, ilinunuliwa gari maalum, *pick up*, kwa ajili ya kuimarisha uwekaji na uandikaji wa alama. Kwa hiyo, nadhani suala hili Mheshimiwa Waziri lingetolewa maelekezo ni muhimu sana ili lawana zisiende kwa Polisi na vyombo vungine zinaposhindwa kufanya kazi hizo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kupokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba ni vyema kitengo hicho kikaimarishwa na nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli Bajeti sio kubwa sana ya kuweka hivyo vibao katika mitaa mbalimbali. Kwa hiyo, tutalingalia suala hili tutalifanyia kazi ili tuweze kuimarisha sehemu zetu za mitaa na kuweka alama mbalimbali.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Eeh, kwa kuwa, pamoja na majibu mazuri. Kwa kuwa, mitaa mingi katika jiji la Dar es Salaam ni mita ile ambayo imeandikwa na kubuniwa na watu binafsi wenyewe kufuata majina yao, majina ya vizazi nya nyuma vilivyopita.

Je, Serikali inachukua nafasi gani katika hili, kuhamasisha Halmashauri na maeneo ya Kiserikali mengine kuhakikisha mitaa hii inachukua hadhi ya majina ya wale watu wanaojulikana ambao wameleta matukio yanayojulikana ya faida katika nchi yetu. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janet Kahama, kama ifuatavyo:-

Katika kuandikisha mitaa au kupanga majina ya mitaa, kuna vigezo mbalimbali ambavyo vinaangaliwa. Vigezo hivyo ni pamoja na umaarufu wa watu.

Lakini kubwa zaidi ni wananchi wenyewe ndio wanaoshirikisha kwa karibu zaidi kulingana na mazingira ya mtaa husika. Mara nyingi wanaweka umaarufu wa majina ya watu walioko katika mtaa huo, au walioishi katika mtaa huo, mara nyingi wanaweka umaarufu labda wa milima, mito, na kadhalika. Kwa hiyo, majina yanawashirikisha zaidi wananchi wenyewe kuliko Serikali.

Lakini sehemu nyingine tunaweka yale majina ambayo ni maarufu kwa viongozi wetu mbalimbali na ni maarufu kwa matendo mbalimbali. Kwa hiyo, nikubaliane na Mheshimiwa Janet Kahama, kwamba mitaa hiyo tunaipanga kulingana na umaarufu wa mahali na umaarufu wa majina ya watu mbalimbali, lakini washiriki wakubwa na wadau wakubwa ni wananchi wenyewe wa sehemu husika.

Na. 175

### **Kuongezwa kwa Ushuru wa Mawasiliano**

**MHE. MGENI J. KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 ushuru wa huduma ya mawasiliano ya simu za mikononi umeongezeka kutoka asilimia 5 (5%) hadi asilimia 7 (7%) ili kukaribiana na kiwango cha asilimia 10 (10%) kinachotozwa katika nchi za Kenya na Uganda:-

(a) Je, vipato vya Watanzania vinakaribiana na vile vya wananchi wa Uganda na Kenya?

(b) Je, *Exchange Rate* ya nchi yetu inalingana na zile za Uganda na Kenya?

(c) Je, ongezeko hilo la asilimia saba (7) litaliingizia Taifa fedha kiasi gani kwa kila mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, taarifa ya viashiria vya Maendeleo katika nchi za Afrika ya mwaka 2006, yaani *Africa Development Indicators 2006*, iliyotolewa na Benki ya Dunia, inaonesha kwamba katika mwaka 2004 wastani wa kipato cha mwananchi kwa mwaka ni dola 320 kwa Mtanzania, dola 250 kwa Mganda, na dola 480 kwa Mkenya.

Mheshimiwa Spika, aidha taarifa hiyo inaonyesha kwamba wastani wa ukuaji wa kipato cha kila mwananchi kwa mwaka katika nchi hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni asilimia 4.6, Uganda ni asilimia 1.8 na Kenya ni asilimia 0.3.

(b) Mheshimiwa Spika, takwimu zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, Benki Kuu ya Uganda na Benki Kuu ya Kenya, zinaonesha kuwa katika mwezi wa Novemba mwaka 2007, dola moja ya Kimarekani ni sawa na wastani wa shilingi 1,133 za Tanzania, Wastani wa shilingi 1,665 za Uganda na wastani wa shilingi 66.51 za Kenya.

Hata hivyo Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, *Exchange Rate* katika nchi zetu inategemeana sana na nguvu ya soko, viwango vya *Exchange Rates* baina ya shilingi hubadiliya mara kwa mara kutegemea na hali ya soko.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 21,151.5 milioni zilitarajiwa kukusanywa kwa kiwango cha asilimia 5 kwa ushuru wa bidhaa kwenye simu za mikononi. Hili lilikuwa ni ongezeko la asilimia 28 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya kiasi cha shilingi bilioni 16,763.7 milioni mwaka 2005/2006.

Ongezeko la kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye simu za mikononi kutoka asilimia 5 hadi asilimia 7 katika mwaka 2006/2007, ilitarajiwa kuiingizia Serikali ongezeko la shilingi bilioni 6,719 milioni kama mapato kutoka chanzo hiki.

Aidha katika mwaka wa fedha 2006/2007 mapato halisi yaliyopatikana kutoka kwenye chanzo hiki, yalifikia shilingi 32,294.3 milioni, sawa na ongezeko la shilingi bilioni 4,123.8 milioni zaidi ya matarajio.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 jumla ya mapato yanayotarajiwa kukusanywa kutoka chanzo hiki ni shilingi bilioni 39,253.2 milioni sawa na ongezeko la asilimia 22 ya mapato yaliyokusanywa kwenye chanzo hiki mwaka 2006/2007.

Aidha, katika kipindi cha robo mwaka ya kwanza ya mwaka 2007/2008, yaani Julai hadi Septemba 2007, jumla ya shilingi bilioni 10,227.3 milioni zilikusanywa kutoka chanzo hiki, ikilinganishwa na matarajio ya kukusanya shilingi bilioni 9,042.4 milioni.

**MHE. MOHAMMED H. J. MNYAA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri na ameonyesha vipato vinavyopatikana kutokana na makampuni haya ya simu. za mikononi. Na kwa kuwa, huwa tunalamika wenye migodi *contrubution* yao kwa wananchi na kwa kuwa, yapo makampuni kama vile ya bia tunayaona namna gani yanavyo *contribute* katika huduma za jamii na michezo.

Je, ni kiasi gani makampuni haya ya simu yanasaidia katika shughuli za jamii huko vijijini kama vile ujenzi wa mashule na michezo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Makampuni ya simu yanasaidia sana shughuli za kijamii. Kwa mfano kampuni moja ya *Vodacom*, ndiyo inayoghamia mashindano ya *Super League* ya timu 14. Vile vile, yamejenga mashule, yanajenga hospitali na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa ni kwamba ujaribu kuwasiliana na yule meneja wa pale ulipo, ili maombi ya jamii ya sehemu ile yaweze kuwasilishwa katika kampuni ya simu katika Makao Makuu yao. (*Makofi*)

Na. 176

**Fedha Zilizotengwa kwa Ajili ya Kilimo na Mifugo  
Mwaka 2005/2006**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali hutenga Bajeti ya kazi za Maendeleo kwa kila Mkoa na Wilaya nchini; na kwa kuwa, Kilimo na Mifugo ni moja ya Sekta zinazopewa kipaumbele na Serikali ya Awamu ya Nne:-

Je, kwa mwaka wa fedha 2005/2006 ni fedha kiasi gani kilipelekwa kwa Mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam na Wilaya zake kwa madhumuni ya kuendeleza Kilimo na Mifugo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukubaliana na Mheshimiwa Job Ndugai kuwa Serikali hutenga Bajeti ya Maendeleo kwa kila Mkoa na Wilaya nchini; na

kwa Kilimo na Mifugo ni mojawapo ya Sekta muhimu zinazopewa kipaumbele na Serikali ya awamu ya nne.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo na mifugo inapewa kipaumbele na Serikali kwani sekta hii ni muhimu katika kuteleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA). (*Makofi*)

Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Serikali kupitia sekta za Kilimo na Mifugo ilitenga kiasi cha shilingi 4.5 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Wilayani (*DADPs*). Fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya, Mijini na baadhi ya Manispaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa fedha hizo ulikuwa kama ifuatavyo:-

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Kilimo - Tshs. 4,027m.

Ufuatiliaji - Ngazi ya Wilaya	- Tshs. 242m
- Ngazi ya Mkoa	Tshs. 82m
- Ngazi ya Taifa -	Tshs. 151m

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ilitengewa fedha za Maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Kilimo na Mifugo kama ifuatavyo:-

<b>DAR ES SALAAM</b>	<b>TSHS.</b>
ILALA	11,500,759
TEMEKE	14,800,978
KINONDONI	15,120,613
<b>JUMLA</b>	<b>41,422,340</b>
<b>DODOMA</b>	<b>TSHS.</b>
<i>Dodoma District Council</i>	49,859,471
<i>Dodoma Municipal Council</i>	16,691,091
Kondoa	64,139,013
Kongwa	33,730,539
Mpwapwa	34,199,624
<b>JUMLA</b>	<b>198,619,758</b>

Mheshimiwa Spika, pamoja na fedha za Maendeleo, Mikoa hii ilitengewa jumla ya shilingi 1.558 bilioni kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na mishahara kwa sekta ya Kilimo na Mifugo.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Ninaanza kwa kumshukuru

Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ingawaje katika majibu yake amenipa fedha za jumla wakati mimi nilitaka anitenganishie kilimo na mifugo ziwe tofauti. Kwa hiyo, maswali yangu yanakuwa hapo hapo, ni kwa nini mifugo inachukuliwa kama ni *substance* ya kilimo na kwa hiyo fedha zake zinakuwa hazieleweki, kama nilivyokuwa nimeomba hapa. Hata Mheshimiwa ameshindwa kunichambulia za mifugo peke yake na za kilimo peke yake? Lakini la pili ni kwamba kwa fedha hizo hizo za mifugo wakati mwingine Dar es Salaam inapata fedha nyingi zaidi kuliko Dodoma ambao hawana mifugo kama Dodoma, au unakuta kwa Wilaya Dodoma Manispaa hapa tulipo wanatengewa fedha nyingi zaidi za Maendeleo ya mifugo kuliko Kongwa. Sasa *disparity* hii Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje kuhusu kurekebisha jambo hili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Job Y. Ndugai, kama ifuatavyo: Kwanza ni kweli kwamba sikutofautisha na orodha ipo Mheshimiwa Mbunge akiitaka nitampa, ni orodha ndefu kidogo. Pili, ni kwamba Dar es Salaam inapata pesa zaidi kuliko Dodoma, kwa hesabu nilizozisoma Dar es Salaam ilipata milioni 41,422,340 wakati Dodoma ilipata milioni 198,619,758 mara tano zaidi ya Dar es Salaam. Labda miaka ya nyuma, kweli kulikuwa na tatizo lakini kwa mwaka unaohusika Dodoma imepata pesa zaidi kuliko mahali pengine. Kuhusu Kongwa kupata pesa kidogo kuliko Manispaa ya Dodoma, kwa mwaka unahusika Kongwa ilitengewa milioni 33,730,539 wakati Manispaa ya Dodoma ilitengewa milioni 16,651 kwa hiyo Kongwa ilipata mara mbili zaidi.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swalii la nyongeza. Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kuuliza kama ifuatavyo. Ruzuku hizi zinaletwa kwenye Bajeti na tunazipitisha lakini ruzuku hizi tunapitisha mahesabu tu ikija wakati wa kutoa fedha, fedha hazitolewi kwa wakati unaohitaji na kiasi kinachohitajika. (*Makofî*)

Kwa mfano mpaka sasa hivi mwaka huu tulipitisha Bajeti kubwa sana kwa Serikali za Mitaa kwa utengenezaji wa barabara hasa vijijini lakini mpaka sasa hivi hata senti moja haijatolewa kwenye Halmashauri yoyote ya Wilaya ya fedha za barabara vijijini. Fedha hizi zisipotumika mpaka mwezi Juni, 2008 zikibaki lazima zirudishwe kwa sababu hazikutumika. Sasa mimi nauliza, hivi hii ruzuku Serikali haioni umuhimu wa kuona kwamba ruzuku hizi hasa hizi za barabara na nyingine zitolewe kwa wakati unaotakiwa ili ziweze kutumika kuleta manufaa yanayohitajika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa John Malecela, kama ifuatavyo. Ni kweli tukiri kwa miaka ya nyuma fedha hizo zilikuwa zinachelewa lakini kwa mwaka huu fedha hizi za barabara awamu ya kwanza zimeshatolewa na awamu ya pili zinaendelea. Nina uhakika kwamba zimeshatolewa kwa sababu nilikuwa katika ziara ya Mtwara, Lindi na fedha hizo zimeshafika kuko.

**MHE. MARIA I. HEWA (K.n.y. MHE. JACOB D. SHIBILITI) aliuliza:-**

Kwa kuwa kilimo huhitaji maandalizi mapema ili kufanikisha mavuno bora na ya kutosha:-

- (a) Je, Serikali imejiandaa vipi juu ya usambazaji wa mbegu bora za Pamba katika msimu wa 2008/2009?
- (b) Je, dawa za kuua wadudu wanaoshambulia zao hilo zimeandaliwa?
- (c) Je, ni nani anayehusika kuagiza na kusambaza dawa hizo kwa wakulima katika msimu huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, naomba kutoa maelezo mafupi.

Kwa kutambua umuhimu wa pembejeo katika kilimo cha pamba, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika sekta ndogo ya pamba imewezesha uundwaji wa Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba ambapo wadau wote wakiwemo wakulima, wanunuzi wa pamba, wachambuaji na Serikali wanachangia sio tu kwa ajili ya pembejeo bali kwa Maendeleo ya zao la pamba kwa ujumla. Katika mwaka wa 2007/2008 Serikali imetoa ruzuku ya shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya madawa ya pamba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba sasa kujibu swal la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, swal lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jumla ya tani 15,000 za mbegu bora za pamba zitasambazwa kwa wakulima katika msimu wa kilimo wa 2007/2008. Mbegu za Pamba zitakazotumika wakati wa kupanda ni zile ambazo zina mabaki ya nyuzi. Mbegu hizo zitataki moja kwa moja kwenye viwanda vya kuchambua pamba na Bodi ya Pamba itahakiki ubora wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbegu za msimu wa 2008/2009 Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba uko kwenye mchakato wa kumpata mwekezaji atakayewekeza katika teknolojia ya kuondoa nyuzi kwenye mbegu za pamba kwa kutumia tindikali (*acid delinting*).

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imejiandaa vizuri kuhusu mahitaji ya dawa za kuua wadudu. Jumla ya *acre packs* 700,000 za viuutilifu na vinyunyizi 3,500 vimeagizwa na vinatarajiwu kufika nchini mwezi Novemba, 2007. *Acre pack* moja ni kiasi cha dawa kinachotumika kunyunyizia ekari moja kwa wakati mmoja. Aidha, yapo masalia ya *acre packs* zipatazo 500,000 na vinyunyizi 6,500 kutoka mwaka 2006. Pembejeo hizo zitaanza kusambazwa kuanzia mwezi Desemba, 2007.

(c) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba ndiyo chombo mahsusini kinachoagiza dawa kwa ajili ya zao la pamba. Usambazaji wa pembejeo za zao la pamba ikiwemo mbegu na dawa unafanywa na makampuni ya wanunuzi na wachambuaji wa pamba.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda niulize maswali mawili mafupi ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, moja, mbegu hizi za pamba zinahitajika sana kwa wakati muafaka wakati wakulima wanapozihitaji mbegu hizi lakini inaleta usumbufu kidogo wakati hizi mbegu zinapelekwa kwenye ofisi za watendaji badala ya kuzipeleka karibu na maeneo ambayo wakulima wamezoea kwenye vyama vya msingi.

Je, Serikali inaweza ikabadilisha utaratibu huu badala ya kupeleka kwenye ofisi za watendaji ambao wana kazi nyingi sana za kufanya pindi mkulima kazi yake ni kilimo tu kuzipeleka kwenye vyama vya msingi badala ya kupeleka kwenye ofisi za watendaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu haya madawa ambayo yanahitajika katika kunyonyuzia wakati hawa wakulima wanahitaji madawa haya, mwaka jana Serikali iliahidi kupunguza bei kwa sababu bei iko juu sana. Je, Serikali inaweza ikawaambia wakulima hawa imepunguza kiasi gani katika lita moja walau wakawa na ahueni kujuu kwamba Serikali inawajali kuwapunguzia bei kwa kuwawekea ruzuku na watawaonyesha kwa njia ipi. Je, aidha kwa sinema au kwa njia ipi ili wajue kuyatumia kwa manufaa ya kupata zao linalostahili? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maria Hewa kwa niaba ya Mheshimiwa Jacob Shibili, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupeleka mbegu kwenye vyama vya ushirika, Serikali haina matatizo kilichojitokeza na ambacho kinaendelea kujitokeza ni kwamba vyama vya ushirika katika sehemu hizo zinazolima pamba vingi havina usafiri na malalamiko yaliyopo ni kwamba ukipitisha mbegu ile inachelewa lakini kama wao watajipanga na vyama vitaimarika na ikaonekana kwamba ndio utaratibu unaofaa kufikisha mbegu hii kwa wakulima haraka basi hilo nadhani halikuwa na matatizo, tatizo ni hilo kwamba vyama havina usafiri wa kusafirisha mbegu na kwa hiyo matatizo yanabaki pale pale.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku naomba kueleza kwamba Serikali imeshatangaza ruzuku ya madawa kama tulivyosema katika hotuba yetu ya Bajeti tumetoa ruzuku kwenye madawa ya pamba takriban lita milioni 1,200,000 na kitakachofanyika ni kwamba tutakuwa na kiasi kama asilimia 30 ya bei itapunguzwa, kutakuwa na hati punguzo kiasi hicho.

Kama mkulima mwaka uliopita alitumia Sh.3,000/= kununua hekapaki moja, basi kupitia maelekezo yake katika ule mfuko wa pamba zamu hii kama alipata hekapaki 10 katika Sh.3,000/=, sasa safari hii hekapaki atakazopata ni zaidi, kwa asilimia 30 utakuta inakuja kama hekapaki 13. Kwa hiyo, hiyo ndiyo njia ambayo itaonyesha kwamba kuna ruzuku katika madawa haya ya pamba.

Na. 178

### **Wanunuzi wa Zao la Korosho**

#### **MHE. DUSTAN MKAPA aliuliza:-**

Kwa kuwa, zao la Korosho ni la nne (4) kwa kuingiza fedha za kigeni na kwa kuwa msimu uliopita wanunuzi waluszusia kununua au walinunua kwa kasi na kwa kiwango kidogo licha ya kuingia mkataba na Bodi ya Korosho, hali iliyoyumbisha uchumi wa nchi yetu:-

- (a) Je, kitendo hicho kilichofanywa na wanunuzi si cha kuhujumu uchumi?
- (b) Je, kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria?

#### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA aliuliza:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Dustan Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wakulima na wanunuzi wa korosho wamejiwekea utaratibu wa kukutana na kujadili masuala yanahusu uzalishaji, upatikanaji wa pembejeo na masoko ya zao la korosho kila mwaka. Katika mwaka wa 2006/2007, baada ya majadiliano ya bei yaliyofanyika Mjini Lindi kuanzia tarehe 18 hadi 19 Septemba, 2006 na baadaye Mjini Mtwara tarehe 25 Septemba, 2007 walikubaliana bei ya kununulia korosho kwa msimu wa 2006/2007 iwe Sh.600/= kwa kilo moja ya korosho daraja la kwanza na Sh.480/= kwa kilo moja ya korosho daraja la pili. Hadi tarehe 2 Oktoba, 2006 msimu wa ununuzi wa korosho ulipoanza, jumla ya makampuni 27 yalikuwa yamepewa leseni za kununulia korosho.

Baadhi ya wanunuzi wa makusudi kabisa walichelewa kuingia sokoni kununua korosho kwa lengo la kuwachosha wakulima kisaikolojia. Aidha, wanunuzi wengine kwa kiburi wamekuwa wakitanganza kuwa korosho ya Tanzania ni ya ubora wa chini ili kuwababaisha wakulima wakubali kuuza korosho yao kwa bei ya chini.

Kiburi hiki kilionyeshwa waziwazi kwa Mheshimiwa Rais alipowataka wanunuzi kununua korosho katika msimu 2006/2007 ili kuokoa korosho zilizokuwa zinaharibika. Wanunuzi wakilikataa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dustan Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kwama ifuatavyo:-

Sheria ya uhujumu uchumi ya mwaka 1984 inavieleza vitendo vya uhujumu uchumi kuwa ni pamoja na vitendo vya rushwa na kuhodhi mali au bidhaa ili kusababisha bei kupanda au kushuka. Baada ya kupitia vifungu vya sheria hiyo Serikali ilibaini kwamba kitendo cha wanunuzi kususia kununua korosho au kununua kwa kiwango kidogo kilikuwa cha kuhujumu uchumi.

Baada ya kubaini hivyo, Serikali ilichukua hatua za kisheria za kuwafutia leseni wale wote ambaao walikuwa hawajanunua korosho, chini ya Sheria ya Korosho ya Mwaka 1984 baada ya kukiuka agizo la Serikali kuwataka wanunue korosho kwa bei ya dira iliyokubalika na pande zote mbili kati ya wanunuzi na wakulima. Kampuni zilizofutiwa leseni ni *Fidahussein Co.Ltd., Kapila Enterprises; Ascorp (T) Ltd.; Hebri Enterprises; Compass Services; Annar Cashew Factory na Senga Enterprises*.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda maslahi ya wakulima, wanunuzi wa korosho na wabanguaji, Serikali imepitisha sheria maalum kuruhusu matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani (*Warehouse Receipt System*) kwa kupitia magilio ya Vyama vya Ushirika. Mfanikio yaliyopatikana katika mazao ya pamba na kahawa kwa kutumia mfumo huu kwenye zao la korosho ili kuondoa kero zinazowapata wakulima wa korosho. Kwa kuanzia mfumo wa stakabadhi ghalani utatumika katika Mkoa wa Mtwara na baadaye utatumika katika Mikoa mingine inayolima korosho.

Chini ya mfumo huu wakulima watawasilisha korosho zao kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi na watalipwa asilimia sitini ya bei inayokisiwa kupatikana katika soko la Dunia na Vyama vya Ushirika vya Msingi vitalipa malipo hayo kutohana na mikopo ambayo vimepata kutoka *NMB*. Hatua hii imechukuliwa ili kunusuru zao la korosho kwa kumpa mkulima soko la uhakika na bei ya uhakika kama mbinu mahsusizi za kukuza uchumi wa zao la korosho na wakulima wa korosho.

**MHE. DUSTAN MKAPA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa pamoja na nia nzuri ya Serikali kuanzisha mtindo wa stakabadhi ghalani kwenye zao la korosho, kero bado zinaendelea hasa katika utekelezaji wa mtindo huu imetokea wilayani kwangu Nanyumbu. Nimetembelea Kata ya Nandete katika magilio ya Ulanga, Mkangara, Ngarikachao, Semeni na kwingineko lakini nimekuta wakulima wanalamika sana kuhusu utekelezaji wa mtindo huu wa stabadhi ghalani. Kwa mfano, pamoja na kwamba wakulima walihimizwa wapande korosho aina ya Brazili, zile korosho hazitakiwi kwa sababu ni ndogo. Vile vile uchaguzi wa korosho pale gulioni mtu anapeleka magunia manne au matano.

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa Mkapa.

**MHE. DUSTAN MKAPA:** Swali ni kwamba je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu kero hizi za kutonunuliwa korosho ndogo na uchaguzi mbovu?

Mheshimiwa Spika, kuna ucheleweshaji mkubwa wa fedha kupelekwa magulioni na kwenye vyama vya msingi pamoja na magunia.

Je, Serikali itaondoaje kero hii au itatatuaje tatizo hili hasa kuweza kumsaidia mkulima aweze kupata fedha yake haraka? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dustan Mkapa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa stakabadhi maghalani ndio tunauanza kwa Mkoa wa Mtwara na kwa bahati nzuri tayari ulikwishaonyesha mafanio mazuri katika mazao ya kahawa na pamba ndio maana tumeuweka na kabla hatujauanzisha Mkuu wa Mkoa wa Mtwara alikaa na aliteuwa tume au Kamati na ikafanya maandalizi ya kuutumia utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa naongea na Mkuu wa Mkoa ili nijue maendeleo ya ununuzi wa korosho na Mkuu wa Mkoa amenihakikishia mwenyewe, kwa kuwa mwenyewe anafuatalia ununuzi wa zao la korosho. Hivi sasa ununuzi wa zao hili unaendelea vizuri na sasa korosho zinatoka kwenye vyama zinaingizwa kwenye maghala yalioandaliwa tayari kwa wanunuzi kwenda kununua pale.

Mheshimiwa Spika, kinachojitokeza hapa ni kwamba katika zoezi hili mbali limewekwa mahususi kwa ajili ya kumlinda mkulima wale *middle man* waliokuwa wanatumia mtindo wa kangomba na wale wanunuzi waliokuwa wanajipangia bei, hao sasa kidogo tumeingilia maslahi yao, ndio hayo wanaoingilia utaratibu huu lakini lengo letu ni kwamba tuhakikishe mkulima wa korosho anapata *take home* ya kumtosha na utaratibu unaendelea vizuri. Kutakuwa na matatizo kidogo kidogo lakini nina hakika yatarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niseme kwamba katika hilo hilo chombo pekee ambacho kinawenza kuhakiki ubora wa korosho na kuhakikisha kwamba korosho hii inafaa kununuliwa si mnunuzi wala mtu mwengine ni Bodii ya Korosho na tumeweka hivyo makusudi kwa ajili ya kumlinda ili ubora wa korosho yake usije ukaingiliwa na *middle man* na wanunuzi wengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kero za maguni, nalo hili limeshatatuliwa, mwanzoni tulipoanza utaratibu huu magunia yalikuwa yamesahauliwa lakini Serikali ilifuatalia na tukapata tena fedha katika fedha tulizopata kutoka *NMB* kwenda kwenye Vyama vya Ushirika sasa maguni yanapatikana kutoka kwenye Kiwanda cha Maguni Dar es Salaam

na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa amenihakikishia kabisa kwamba maguni hivi sasa yanaendelea kupelekwa na hakuna tatizo la magunia.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa, kwa bahati mbaya leo maswali ya nyongeza ni mrefu mno na majibu ni mrefu mno. Kwa hiyo, sasa nitaenda haraka mtaniwia radhi. Tunahamia Wizara ya Usalama wa Raia, swali linaulizwa na Mheshimiwa Charles Kajege, naye ana swali refu la kurasa moja na nusu, sijui leo kuna nini?

Na. 179

**Ongezeko la Vitendo nya  
Uhalifu Ziwa Victoria**

**MHE. CHARLES MUGUTA KAJEGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, vitendo nya ujambazi katika Ziwa Victoria vimekuwa vikiongezeka siku hadi siku ambapo wavuvi wengi wakiwemo na Jimbo la Mwibara wamepoteza maisha yao, kupata vilema nya kudumu na upotevu wa mali kama mashua, nyavu na mashine za kuvulia; na kwa kuwa, hali hii kwa kiasi kikubwa imekwamisha shughuli za uvuvi na pato litokanalo na Sekta hii kwa ujumla:-

- (a) Je, Serikali haioni kwamba, kuendelea kuwepo kwa hali hiyo kunapingana na mkakati wa Serikali wa kupambana na ukosefu wa ajira na kupunguza umaskini?
- (b) Kwa kuwa, majambazi wanafanya uhalifu huo kwa kutumia boti ziendazo kasi. Je, Serikali haioni kwamba, kuna haja ya kufanya doria kwa helikopta katika maeneo yaliyoathirika likiwemo Jimbo la Mwibara ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuli za uvuvi kwa amani?
- (c) Je, ni majambazi wangapi waliokwisha kamatwa na kufikishwa mahakamani katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2000 – 2005) kuhusiana na uhalifu huo katika sehemu za Ziwa Victoria inayopakana na Jimbo la Mwibara.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa mwaka 2005 na mwanzoni mwa mwaka 2006 vitendo nya ujambazi vilikithiri katika sehemu mbalimbali za nchi yetu ikiwemo maeneo ya Ziwa Victoria na mwambao wake katika mikoa ya Kagera, Mara na Mwanza. Vitendo

hivyo vya uhalifu vilikuwa ni tishio kwa maisha na mali za wananchi pamoja na wageni wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kutokomeza ujambazi huu kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

Hatua hizo ni pamoja na kuendesha operesheni maalum kwa kushirikiana na vyombo vyote vya dola, kama vile Idara ya Uhamiaji, Usalama wa Taifa, JWTZ na Mamlaka ya Kodi *T.R.A.* kufanya doria, misako, kuimarisha ushirikiano wa nchi jirani katika kusaka majambazi yanayofanya uhalifu nchi hadi nchi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi zimeimarisha ulinzi na usalama hapa nchini likiwemo eneo la Ziwa Victoria na Jimbo la Mwibara Mkoani Mara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa hali ya usalama katika Ziwa Victoria ni ya kuridhisha. Tunaomba Wananchi waendelee na shughuli zao za kiuchumi na uzalishaji mali ikiwa ni pamoja na kujishughulisha na uvuvi ili kujiongezea kipato kwa nia ya kujiondolea umaskini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kufanya doria hapa nchini hususan maeneo ya ukanda wa bahari na maziwa kwa kutumia helikopta. Lakini kwa sasa haina uwezo wa kununua helikopta kwa ajili ya kazi hiyo. (*Makofî*)

Hata hivyo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Idara nyingine za Serikali limekuwa likifanya doria za nchi kavu na majini kwa kutumia mashua kwa lengo la kuimarisha ulinzi katika maeneo ya maziwa na ukanda wake.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi pia, linaendelea na juhudini za kukarabati mashua ambazo ni mbovu kwa ajili ya kuimarisha doria katika Maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Victoria.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano 2000 – 2005 matukio ya uhalifu pamoja na ajali za ziwani zilizotokea sehemu ya Ziwa Victoria Mkoani Mara pamoja na maeneo yanayopakana na Jimbo la Mwibara ni kama ifuatavyo:-

Unyang'anyi wa kutumia silaha matukio tisa, watuhumiwa wa ujambazi waliouawa na wananchi ni matukio mawili, kuzama majini matukio 10, vifo vyatuzama majini matukio 18, watuhumiwa waliokamatwa saba na watuhumiwa waliofikishwa mahakamani saba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matukio hayo, hali ya maeneo ya uvuvi katika eneo la Mwibara ni ya kuridhisha. Aidha Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Idara ya Uvuvi Mkoani Mara linaendelea kufanya doria katika ziwa Victoria kwa lengo la kupambana na uhalifu wa Ziwani pamoja na uvuvi haramu.

**MHE. CHARLES MUGUTA KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa nataka kупingana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba hali ya usalama katika Ziwa Victoria ni nzuri, ujambazi bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza, kwa kuwa Jimbo la Mwibara lina visiwa vingi ambavyo hutegemea sana uvuvi na kwa kuwa majambazi yamekuwa yanayosumbua sana wananchi katika ziwa hilo.

Je, ni lini Serikali itaanzisha angalau kituo kimoja katika mojawapo ya visiwa hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege kama ifuatavyo:-

Kutokana na mpango wa muda mrefu wa tathmini ya vituo vyatuzama Polisi nchini, Jeshi la Polisi limeona umuhimu wa kujenga kituo katika maeneo hayo na ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mara zitakapopatikana fedha tutajenga kituo katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah Mbunge wa Pangani.

Na. 180

#### **Ziara ya Mbunge Magerezani**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja ya majukumu ya Mbunge ni kutembelea Magereza popote pale nchini kama "Visiting Justice" hasa katika Jimbo lake ili kusikiliza malalamiko ya mahabusu kwa kuchelewa kusikilizwa kesi zao; na kwa kuwa Mbunge hukosa majibu ya uhakika ya kumwezesha kujibu hoja za wafungwa na mahabusu:-

- (a) Je, Serikali haioni haja ya kuweka utaratibu kuwa, Mbunge aongozane na Afisa kutoka Polisi ili asaidie kutoa maelezo juu ya maswali ya mahabusu kwa niaba ya Mbunge?
- (b) Kama utaratibu huo upo, Serikali ipo tayari kutoa mwongozo kwa vituo vyote vya Polisi vya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama lifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Magereza (*The Prisons Act Cap 58 R: E 2002*) kifungu cha 101 Mbunge ni Mkaguzi wa Magereza (*ex Officio Visiting Justice*) kwa magereza yaliyoko katika Jimbo lake. Wakaguzi wengine wa Magereza ni Waziri, mtu yoyote atakayeteuliwa na Mkuu wa Mkoa, Majaji, Mahakimu, Walinzi wa Amani na Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Mkaguzi wa Magereza (*ex Officio Visiting Justice*) kazi yake ni kukagua hali ya magereza ilivyo na kusikiliza hoja mbalimbali za wafungwa. Baada ya kusikiliza hoja hizo na kuona hali ya magereza ilivyo anatakiwa kuandika maoni na mapendekezo yake kuhusu yale aliyoona na kuelezwaa na wafungwa kadri atakavyoona inafaa katika kitabu maalum cha gereza alilotembelea kinachotunzwa na Mkuu wa Gereza husika. Mkuu huyo wa gereza atamshauri Kamishna Mkuu wa Magereza kuhusu maoni na mapendekezo aliyyoatoa Mheshimiwa Mbunge. Hivyo Mbunge anapokwenda gerezani haendi kujibu hoja au kutoa maelezo ya maswali ya wafungwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba kunukuu Kifungu cha 101, kifungu kidogo cha nane cha sheria ya magereza – (*The Prisons Act, Cap 58 R:E 2002*). Nanukuu:-

*“On the completion of each visit every visiting justice may enter in a book to be kept for such purpose remarks, suggestions or recommendations as he may deem appropriate and the officer in-charge shall advise the commissioner of all observation so entered.”* Mwisho wa kunukuu. Kwa mujibu wa kifungu tajwa hapo juu, Serikali kwa wakati huu haina fursa ya kutoa mwongozo kwa vituo vya Polisi vya Wilaya kuwataka maofisa wa Polisi kuambatana na Waheshimiwa Wabunge wanapotembelea Magereza ili wasaidie kutoa maelezo ya maswali ya mahabusu kwa niaba ya Wabunge. Kufanya hivyo ni kukiuka sheria niliyoitaja na kuinukuu.

**SPIKA:** Swalii la nyongeza Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, sina matatizo kuhusiana na wafungwa, Mbunge anapotembelea magereza anakutana na Mahabusu na Mahabusu wanakuwa wengi kuliko wafungwa na matatizo yao Mbunge anakuwa hana jibu na nafikiri Mbunge ana haki ya kujua kwamba matatizo haya yanatatuliwa vipi. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna haja kwamba mahabusu wale wapatiwe majibu kwa sababu bado hawajawa wafungwa ni watuhumiwa?

Mheshimiwa Spika, kuna kesi ambazo kwamba zinachukua muda mrefu na kwa utaratibu kesi inapokwenda Mahakamani zikipita siku 60 kabla hazijasikilizwa kesi hizo zinatakiwa zifutwe mpaka hapo upelelezi utakapokamilika.

Je, Mbunge hana haki ya kusimamia hilo na kuihoji Serikali kwamba kwa nini kesi hizi zinachelewa?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Riched Abdallah, yenyе (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba Sheria iliyopo inamtaka Mheshimiwa Mbunge asikilize maoni na malalamiko ya wafungwa na baada ya kusikiliza hayo ni haki yake ya kutoa maoni yake katika kitabu maalum kilichopo pale gerezani. Kwa msingi huo maoni hayo Mkuu wa Gereza anayapeleka kwa Kamishna wa Magereza na anapoyapeleka kwa Kamishna wa Magereza anachukua hatua zinazofaa. Kwa hiyo, ni haki yako Mheshimiwa Mbunge kuishauri Serikali na kushauri vile anavyoona inafaa kuhakikisha kwamba matatizo ya kesi na mambo mengine hayachukui muda mrefu yanamalizika. Ni nia ya Serikali kuchukua hatua mbalimbali kutatua tatizo hili la ucheleweshaji wa kesi na hivi sasa hatua mbalimbali zinachukuliwa na Kamati Maalumu zimeundwa zinazosimamia mambo hayo ikiwemo hatua ya suala zima la kupeleka kesi haraka yaani *Case Flow Management*.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya kila linalowezekana upelelezi uende kwa haraka.

**SPIKA:** Tunahamia sasa Wizara ya Nishati na Madini na swali linaulizwa na Stephen Jones Galinoma Mbunge wa Kalenga.

Na. 181

### **Utafiti wa Dhahabu Iringa**

### **MHE. STEPHEN J. GALINOMA aliuliza:-**

Kwa kuwa kati ya miaka ya 1995 -1999 Kampuni ya *Anglo - American Exploration Company* ilipiga kambi kwenye Kijiji cha Ihemi kufanya utafiti wa madini ya dhahabu katika Jimbo la Kalenga, hususan Kata za Ifunda, Maboga na Mgama:-

- (a) Je, Serikali inaweza kueleza matokeo ya utafiti huo na kama imegundulika kuwa yapo madini, wananchi watafaidika vipi?
- (b) Ikiwa kwa sababu yoyote ile hakuna matokeo. Je, Serikali inaweza kutumia wataalam wa madini waliopo Wilaya ya Iringa ili waweze kubaini uwepo wa madini hayo?

### **WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mbunge wa Kalenga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Anglo-American Exploration Company* ilifanya utafutaji wa madini katika eneo la leseni ya utafutaji madini PL 714/1996 lililopo Utengulini pamoja na maeneo ya jirani kati ya mwaka 1995 na 1999. Kampuni ilifanya kazi za uchunguzi wa miamba na uchoraji wa ramani za kijiolojia, upimaji wa sumaku ya dunia (*magnetics*) na uchukuaji wa sampuli za miamba, udongo na vichunguu. Kazi zinginezo zilizofanyika ni uchimbaji wa mashimo ya uchunguzi, uchorongaji wa miamba na upimaji wa sampuli uliofanyika katika maabaraza Mwanza na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kazi zilizofanyika katika eneo la Mlima Utengulini yalionyesha kuwepo mashapo ya wakia 38,000 za dhahabu, sawa na tani 1.182 katika kina cha mita 100, upana wa mita 9.51 na kina cha mita 100. Baada ya kubainika kuwa kiasi cha dhahabu kilichopo katika eneo hilo ni kidogo ambacho hakiwezi kuchimbwa kwa faida kwa uchimbaji mkubwa, kampuni iliamua kuliachia eneo hilo. Baada ya kampuni hiyo kusimamisha shughuli za utafutaji katika maeneo hayo, hivi sasa kampuni za *Express Ship Management* na *Honey Guide International Limited* zimepewa leseni ya utafutaji madini katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kama itagundulika kuwepo kwa madini ya dhahabu, wananchi wa Jimbo la Kalenga watanufaika kwa njia nyingi zikiwemo za kupata ajira na pia kuongezeka kwa soko la mazao na bidhaa nyingine ambazo zitahitajika kwa ajili ya mahitaji ya chakula na mahitaji mengine ya kila siku ya wafanyakazi wa mgodi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye sehemu (a) matokeo ya kazi za utafutaji madini zilizofanywa katika eneo la Utengulini yanafahamika. Kwa sasa eneo la Jimbo la Kalenga lina wawekezaji wakubwa wawili ambao wanaendelea na utafiti. Kampuni hizo ni *Express Ship Management* na *Honey Guide International Limited*.

**SPIKA:** Mheshimiwa . Stephen Jones Galinoma swalii la nyongeza.

**MHE. STEPHEN JONES GALINONA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza na pili nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa taarifa aliyoitoa.

Kabla sijaauliza maswali ya nyongeza ningependa kueleza kwa ufupi tu kwamba utafiti huo ulifanyika katika Kata ya Lumuli, Ifunda, Ihemi na Utengulini na ulifanyika kwa muda wa miaka miaka minne kama alivyo sema na wakati huo wananchi wa eneo hilo la Utengulini na sehemu nyingine walipewa hati au leseni za kushughulikia dhahabu. Walipewa leseni nne, sasa kitu ambacho kinanishangana na ninapenda Waziri anisaidie kuelewa ni kwamba pamoja na utafiti uliofanyika, zimetolewa *licence* nyingine na mojawapo ambayo ndiyo inayotusumbua sana kule ni ya *Green Hill Mine* ambayo amepewa leseni mwezi wa nne mwaka huu 2007 bila kujali kwamba wananchi wa pale wana leseni.

Je, Waziri atakubaliana nami kwamba kwa kuwa utafiti ulikwisha fanyika na kwa kuwa wachimbaji wadogowadogo yaani wananchi wapo pale na wamekuwa wakishughulikia suala hilo kwa miaka 10 iliyopita kuna haja gani ya kuwa na leseni mpya ya utafiti?

Ni kweli kwamba dhahabu iliyopo pale siyo nyingi kwa madhumuni ya wachimbaji wakubwa kwa maana hiyo ingestahili wachimbaji wadogowadogo wapewe umuhimu. Je, Waziri atakubaliana nami kwamba maeneo hayo yaachiwe wananchi waweze kushughulikia maeneo hayo na kuondoa umaskini?

**SPIKA:** Naona tunaendelea vilevile tu maana maswali marefu kabisa ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini majibu tafadhali.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nataka kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kumpongeza kwa juhudzi zake ambazo alikuwa anafuutilia eneo hili la Kata kama alivyo zieleza kusudi wachimbaji wadogo wapewe hilo eneo.

Nataka kumhakikishia kwenye swalilake la kwanza kwamba kwa kufuatilia Sheria ya Madini huwezi ukatoa leseni mbili kwenye eneo moja. Kwa hiyo, maeneo yale ambayo kama kuna mtu amepewa leseni ni kwenye eneo ambalo lilikuwa halina leseni na ikigundulika kwamba mtu amepewa leseni kwenye eneo ambalo tayari lilikuwa na leseni ya zamani basi huyu mtu atafutiwa leseni yake.

Mheshimiwa Spika, Swalilaki kwenye eneo hili, kampuni zinatofautiana katika uwezo na utealamu wa kufanya utafiti. Katika hili kampuni moja inaweza kufanya utafiti na kutogundua madini lakini kampuni nyingine ikafanya utafiti wa kina na ikagundua madini katika eneo hilohilo.

Kwa hiyo, ndiyo sababu hizi kampuni za *Express ship Management* na *Honey Guide International* zimepewa. Lakini kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge ni kwamba hizi kampuni pindi zitakapogundua kwamba mashapo yaliyopo yana dhahabu kidogo, uchimbaji hauwezi kuwa mkubwa na wakaachia hilo eneo kwa takwimu hizo ambazo tutakuwa tumezipata kwa hawa na wale waliotangulia naweza kuchukua fursa hiyo nika *designate* na kutoa tamko kwamba hilo eneo liachiwe na kupimwa ili wapewe wachimbaji wadogowadogo.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mohammed H. Missanga.

Na. 182

### **Soko la Mtama Mweupe**

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2003 Serikali iliwajulisha wananchi kuwa imepata soko la mtama mweupe huko Italy ambapo wananchi wanaolima zao hilo walipewa hiyo taarifa na kuhamasishwa kulima zaidi mtama na kwa kuwa wananchi wanaulizia mara kwa mara kuhusiana na soko hilo bila ya mafanikio:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi kuhusiana na ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Mohamed Hamis Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa mwaka 2003 nchi ya Italia ilionyesha nia ya kununua mtama mweupe toka Tanzania ambapo wakulima katika maeneo yanayolima mtama ukiwemo Mkoa wa Singida walianza kuhamasishwa kulima mtama kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya soko hilo.

Pamoja na kuwepo kwa fursa ya soko la zao la mtama mweupe huko Italia, wakulima wetu bado hawajaweza kufikia viwango vya Kimataifa vya ubora na wingi wa kukidhi mahitaji ya soko hilo.

Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji wa mtama mweupe hapa nchini bado haukidhi mahitaji ya masoko ya nje kutokana na wakulima kupanda mbegu mchanganyiko na hivyo kuvuna mtama wenye rangi tofauti ambao haukidhi viwango vinavyohitajika katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuhakikisha kuwa wakulima wetu wanazalisha mtama mweupe kukidhi mahitaji ya soko la Kimataifa, wakulima wetu wanaendelea kushauriwa kuzingatia uzalishaji wa mtama unaohitajika na kwa madhumuni ya kukidhi kiwango cha wingi wa mtama unaohitajika wakulima wanahamasishwa kujiunga pamoja katika vikundi na vyama vyaa ushirika vitakavyowaunganisha na wafanyabiashara wanaohitaji mtama na wakati huo huo kuwasaidia kupata taarifa za bei, ubora na kiasi kinachotakiwa.

Kwa upande mwingine Serikali inaendelea na jitihada za uendelezaji wa miundombinu ya masoko ya mazao ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya barabara na reli kuweza kufikia maeneo mbalimbali na kusafirisha mazao ya wakulima kwenda kwenye masoko.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa soko la mtama mweupe huko Italia bado lipo na wakulima wetu wanaombwa kuzingatia ushauri wanaopewa na Serikali wa kuzalisha mtama unaokidhi mahitaji ya soko hilo kwa wingi na ubora. Kwa upande wake Serikali itaendelea kushirikiana nao kwa kuwaunganisha na soko hilo.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Mohammed H. Missanga.

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri niulize tu kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, kama nilivyouliza kwenye swali la msingi kwamba kauli hii ya Serikali ilikuwa ni ya mwaka 2003 na sasa ni takribani miaka minne au mitano toka kauli hiyo itolewe na kipindi chote hiki hapajakuwa na maelezo yoyote kama haya ambayo anayaeleza Mheshimiwa Waziri hapa hivi sasa kiasi kwamba wananchi wanaendelea kutegemea au kusubiri hilo soko la Italia na maelezo haya ambayo ameeleza Mheshimiwa hayajatolewa.

Je, Serikali haioni kwamba pale ambapo wanashindwa kutekeleza zile ahadi zake basi itoe kauli na ieleze ni hatua gani zinazochukuliwa kulikoni kukaa kimya jambo ambalo linawafanya wananchi wahoji baadhi ya kauli za Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Alhaj Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nisikubaliane sana na Mheshimiwa Mbunge kwa Serikali ilikuwa imekaa kimya kwa sababu jitihada hizi ambazo nilizileta hapa za kushauri wakulima walime huu mtama mweupe zipo kwa wakulima na wakulima wanaendelea kushauriwa mara kwa mara. Labda tu hapa Bungeni ilikuwa haijatolewa taarifa kwa sababu ilikuwa haijahitajika taarifa hii kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge lakini jitihada za Serikali katika kushauri na kuelekeza nini cha kufanya zilikuwa zikiendelea. Kwa hiyo, nataka tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuwahamasisha wakulima waweze wakazingatia masharti ya uzalishaji wa zao hilo ili waweze wakakidhi mahitaji ya soko hilo.

**SPIKA:** Swali fupi sana la nyongeza Mheshimiwa George B. Simbachawene.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa *SGR* na kununua mtama katika Mkoa wetu wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, lakini ninataka kuchukua nafasi hii kuwaambia wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwamba mtama huu ni pamoja na kuutumia sisi wenyewe kama chakula siyo kuuza tu. Lakini nina ombi maalum kwa Serikali kwamba zipo takriban tani 100 pale Gulwe ambazo *SGR* wameshindwa kununua, ninaomba Serikali waende watoe fedha kidogo wakanunue ule mtama kwa maana hakuna uwezekano wa kuurudisha na wananchi wameshautoa kutoka mbali na wameufikisha pale kwenye godauni.

Je, Serikali iko tayari kufanya hivyo? (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba mtama ambaou umelimwa hapa katika Mkoa wa Dodoma ikiwemo na Wilaya ya Mpwapwa ni pamoja na chakula. Sasa ziada ile ndiyo Serikali imeona inunue kupitia katika kitengo chake cha *SGR*.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu *SGR* inapata pesa zake kwa mujibu wa kiwango kilichowekwa kisheria sasa fedha hizo zikishafikia hapo inakuwa ni vigumu wakati mwingine kuweza kupata nyongeza ya ziada. Lakini muwahakikishie tu kwamba Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta nje zozote zile zitakazowezekana kuhakikisha kwamba mtama huu ambaou anauzungumzia uweze kununuliwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata linalekezwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu na linaulizwa na Mheshimiwa Captain Mstaafu George H. Mkuchika, Mbunge wa Newala.

### **Ukarabati wa Chuo cha Kitangali**

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA** aliuliza:

Kwa kuwa, majengo ya Chuo cha Ualimu Kitangali yalirithiwa kutoka kwa iliyokuwa *Kitangali Middle School*, na kwa kuwa hivi sasa majengo hayo yamechakaa hivyo kunahitajika ukarabati mkubwa pamoja na upanuzi wa Chuo:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati majengo hayo na kufanya upanuzi ili kuweza kupokea wanafunzi wengi zaidi?
- (b) Je, kuwepo kwa chuo hicho kunasaidiaje juhudzi za kupunguza tatizo la upungufu wa walimu wa shule za msingi Mkoani Mtwara ambako mpaka kufikia Juni, 2007 kulikuwa na upungufu wa walimu 1229.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI - (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchuka, Mbunge wa Newala lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Chuo cha Ualimu cha Kitangali ni kimoja kati ya vhuo 18 vya ualimu wa Daraja la IIIA vilivyoathiri kutoka zilizokwuwa *Middle Schools* na kina uwezo wa kuchukua wanachuo 200. Chuo cha Ualimu Kitangali kwa sasa hakimo katika Mpango wa Upanuzi wa Vyuo vya Ualimu. Hata hivyo, katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha 2007/2008, Wizara yangu imepeleka kiasi cha shilingi milioni 29,288,200/= kwa ajili ya ukarabati na kununulia vifaa. Wizara itaendelea kutoa fedha za ukarabati wa chuo hicho kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Ualimu vya Serikali kikiwemo Chuo cha Ualimu Kitangali ni vya Kitaifa vinavyotumika kutayarisha walimu kwaajili ya mahitaji ya nchi nzima, ukiwemo Mkoani Mtwara. Wizara inatambua upungufu wa walimu wa Shule za Msingi katika Mkoani Mtwara na Mikoa mingine. Kwa maeneo ambayo hayana walimu wa kutosha, wazo la kupanga walimu wanafunzi wa maeneo hayo katika vyuo vilivyo karibu na maeneo yao litazingatiwa ili mradi waombaji wawe na sifa zinazostahili.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Capt. Mkuchika.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, na pili mimi kama Mbunge wa Newala nishukuru kwa ushirikiano ninaoupata kutoka Wizara hii katika kushughulikia matatizo ya elimu katika jimbo langu.Nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba kuna upungufu wa walimu katika Jimbo la Newala na Mkoa wa Mtwara, wakati nauliza swali upungufu ulikuwa ni walimu 1229, leo asubuhi ni walimu 1230. (*Makofi*)

Kwa kuwa, kukosekana kwa walimu kunaathiri taaluma mtoto anapomaliza darasa la saba anakuwa hajahitimu sawasawa na kwa sababu tatizo hili tunalo tangu mwaka 1961 tulipopata uhuru mpaka leo hii. Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa Jimbo la Newala na Mtwara kwamba ina mikakati gani ya haraka kupunguza tatizo hilikama walivyochukua hatua za haraka za kupunguza matatizo ya walimu wa Sekondari?

Kwa kuwa, kwa ushirikiano uliousema Wizara imetukubalia Wabunge sisi Mtwara kutafuta vijana wazuri waliomaliza form four waende wakasome ualimu, mwaka jana walikwenda na mwaka huu wamekwenda.

Je, Serikali inaweza kutuahidi kwamba ili kupunguza shida hii ya walimu kwamba wale vijana wakishamaliza watawabakiza kulekule ili tupunguze tatizo hili la walimu linalotukabili?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI - (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika Mbunge wa Newala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza niwie radhi nilisahau kumpongeza kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama Tawala. (*Makofi*)

Pia nimpongeze sana Mheshimiwa George H. Mkuchika ni mfuatiliaji hodari maana yeye huja mwenyewe ofisini na akafuatilia mpaka kupata majibu na akaondoka.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo naomba nianze kwa kujibu maswali yake mawili.

Ni kweli upungufu wa walimu kwa mkoa wa Mtwara na baadhi ya mikoa iliyopo pembezoni ni tatizo kubwa. Binafsi nimefanya ziara Mkoa huo na nimebaini.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni hali ya miundombinu namna ya kufika na huduma kukosekana katika maeneo mengi ya mkoa huo. Naomba kwa niaba ya Waziri wa Elimu niseme kwamba Serikali kwa ujumla wake imejipanga vizuri sana. Baadhi ya kero zikiwemo nyumba za walimu na mambo mengine muhimu zimepewa kipaumbele na wewe mwenyewe ni shuhudi kiasi kikubwa cha fedha kimeelekezwa mkoa wa Mtwara.

Kuhusu tofauti ya taaluma kwamba wanafunzi hawapati mafunzo kama inavyostahili na hivyo kufanya mkoa huo uwe katika matatizo naomba niseme kwamba tunafahamu na tupo katika hali ya kufanya tathmini ili tuweze kubaini upunguf na dosari ili tujipange sawasawa.

Mheshimiwa Spika, vijana ambao tumewapatia nafasi kwenda kwenye mafunzo ya ualimu wanayo haki ya kuchagua kurudi kwao lakini vilevile ni vigumu kumzuia binadamu na maoni yake. Sisi tutawashawishi wabaki kule, lakini baadhi yao waliochaguliwa ni wanawake, kwa hiyo watakapokwenda kule wakiolewa mikoa mingine sisi tutakuwa hatuna la kuwazuia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa ni zamu ya Wizara ya Katiba na Mambo ya Sheria swali linaulizwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

Na. 184

### **Marekebisho ya Sheria ya Ndoa Mirathi na Watoto**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:

Kwa kuwa, Sheria ya Ndoa, Mirathi, na Watoto zina kasoro nyingi, na kwa kuwa Tume ya Kurekebisha Sheria imeshazifanyia utafiti na kuzipeleka Serikalini ili ziweze kufanyiwa marekebisho:-

### **WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo:

Ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba Sheria ya Ndoa, Sheria ya Watoto na Sheria ya Mirathi zimedhihirika kuwa na kasoro nyingi na ndiyo maana imo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Serikali iliagiza Tume ya Kurekebisha Sheria kutafiti Sheria hizo na kutoa mapendekezo ya kuziboresha kutokana na ukweli kwamba Sheria hizo zinagusa maisha ya kila siku ya wananchi.

Tume ya Kurekebisha Sheria iliwashirikisha wananchi walio wengi kutoa maoni yao kuhusu Sheria hizo, Serikali imefanyia kazi matokeo ya utafiti wa Tume na kukubaliana kwa sehemu kubwa, na matokeo ya utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyatafakari maoni ya wananchi wengi yaliyotolewa katika vyombo nya habari, makongamano, warsha na mikutano ya hadhara, mengine ya wananchi, watalaamu na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu, Serikali, imeanzisha mchakato wa kutayarisha Miswada ya Sheria katika maeneo hayo kupitia Nyaraka za Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, mchakato karibu unakamilika, Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba nyaraka kuhusiana na Sheria hizi ambazo ziko katika hatua ya kujadiliwa na vyombo vyake vinaapewa kipaumbele katika shughuli za Serikali kama nilivyoahidi wakati nikijubu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuwasilisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa George M. Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba baada ya kukamilisha nyaraka hizo na kwa kuwa Tume ya Kurekebisha Sheria imeshakamilisha utafiti. Je, Serikali itakuwa tayari kuleta Muswada huo Mkutano wa Kumi wa Bunge.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la swali la msingi kwamba Serikali inakubali kwamba Sheria hizo lazima zifanyiwe marekebisho. Siwezi kuahidi katika mkutano wa kumi wa Bunge lakini mara taratibu zingine zitakapokuwa tayari Miswada hiyo italetwa Bungeni.

Na. 185

#### **Waganga na Wauguzi katika Mikoa ya Pembezoni**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna tatizo la Waganga, Waganga Wasaidizi na Wauguzi kutopenda kufanya kazi katika Mikoa iliyo pembezoni:-

- (a) Je, kwa nini Serikali isitumie Vyuo kama Chuo cha Sumbawanga Mjini kutoa Watumishi watakaofanya kazi Mikoa ya Rukwa na Ruvuma?
- (b) Je, ni motisha gani imeandaliwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa watumishi watakaokubali kufanya kazi katika Mikoa ya pembezoni?
- (c) Kwa kuwa Chuo cha Waganga Sumbawanga hakuna vifaa na zana mbalimbali za kutosha, je, Serikali ina mpango gani wa kukipatia Chuo hicho vifaa vyta utawala, gari, kompyuta ili kiwe mfano mzuri katika mafunzo hayo?

#### **NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inavyo vyuo 7 vya kuwaendeleza RMA kuwa Maafisa Tabibu. Vyuo hivi ni Masasi, Songea, Sumbawanga, Kigoma, Maswa, Musoma na Bumbuli. Wanafunzi walio wengi wanaojiunga na vyuo hivi hutoka kwenye Kanda au Mikoa jirani. Kwa utaratibu huu chuo cha Sumbawanga hupokea wanafunzi kutoka Mikoa ya Rukwa, Mbeya na Iringa. Wanafunzi waliojiunga na chuo cha Sumbawanga katika miaka iliyopita yaani 2006/2007 kwa ujumla wake ni Rukwa walikuwa 83, Mbeya 68 na Iringa 45.

(b) Wizara inatambua ugumu wa mazingira ya kazi katika maeneo kadhaa ya nchi yakiwemo yale ya pembezoni na kwamba watumishi waliopo katika maeneo haya wanastahili motisha. Suala hili limewekewa mikakati kadhaa ikiwemo ya kuondoa usumbuwa wa kupata mishahara yao, kuwalipa madeni na stahili za watumishi hawa katika muda unaostahili, kuwapa kipaumbele wakati wa kutoa nafasi nafasi za kujiendeleza kielimu katika fani zao, kuboresha mazingira ya sehemu zao za kazi kwa kufanya ukarabati wa majengo, kutoa vitendea kazi na kusisitiza Halmashauri zilitahidi kuwapatia nyumba.

Suala la posho ya mazingira magumu ni la msingi lakini hili ni la Serikali nzima kwa vile kuna watumishi wengine wasio wa sekta ya afya wanaofanya kazi vijijini na maeneo ya pembezoni. Serikali kwa ujumla wake inalitafakari suala hili na hapo *formula itakapotayarishwa na pesa kupatikana basi utekelezaji utafuata mara moja.*

(c) Kwa kupitia bajeti yake ya kila mwaka, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina utaratibu wa kuboresha vyuo vyake ikiwa ni pamoja na kuongeza vifaa vya utawala na vya taaluma. Chuo cha Sumbawanga kimenunuliwa gari aina ya *Land Cruiser Hard Top* yenye namba za usajili STK 3016 katika mwaka wa fedha 2005/2006 na hivi sasa gari hilo limekwishafikishwa chuoni.

Aidha, katika mwaka 2004/2005 na 2005/2006, chuo kilinunuliwa jumla ya kompyuta tano (*Desktop 4* na *Lap top 1*). Wizara itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya taaluma na vya kufundishia kwa vyuo vyake vyote kikiwepo chuo cha Tabibu Sumbawanga.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyojatao lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabla ya hayo, jana wakati Mheshimiwa Naibu Waziri Celina Kombani akitoa majibu ya Mheshimiwa Anna Lupembe kuhusiana na Zahanati ya Batanga kulikuwa kidogo na kutolewana.

Mheshimiwa Spika, nimecheki mimi mwenyewe jana na leo asubuhi tumeshirikiana na Mheshimiwa Lupembe, tumeona kweli majibu aliyojatao Mheshimiwa Naibu Waziri yalikuwa ni sahihi na tumepata wauguzi wamekwenda pale na madawa yamepatikana, nashukuru Serikali kwa kujibu kwa ufasaha majibu hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa maswali mawili ya nyongeza. Hivi Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa nini hamji Rukwa kuja kujifunza utaratibu tuliuandaa namna ya kuweka vivutio kwa watumishi, tumeanza na walimu na tuna walimu wa kutosha kwa kujiwekea sisi wenyewe vivutio, tatizo liko wapi msije kujifunza namna ya kuweka vivutio pia kwa waganga? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, ningomba kwa sababu tumeanza sasa mpango wa kuwa na zahanati kwa kila kijiji kwa nini sasa utaratibu usiandaliwe kwa makusudi ile Mikoa ambayo ipo pembezoni wakapewa kipaumbele kupelekewa hawa watumishi haraka iwezekanavyo ili kuziba mapengo yaliyopo hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Kimiti naomba kwanza kumpongeza pamoja na Mheshimiwa Lupembe kwa kufuatilia ili kuweza kuweka sawa jibu alilotoa Mheshimiwa Celina jana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii lake la kwanza la kutokwenda Rukwa ili kwenda kujifunza namwahidi Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa kwamba nitakwenda Rukwa na tutakwenda kuzunguka na kuona jinsi gani tutafanya ili kuweza kuboresha na kuweza kuwaweka hawa watumishi waweze kukaa kule Rukwa na nitafuatana naye yeye, Mheshimiwa Lupembe na Wabunge wengine wote wa Rukwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii lake la pili, mpango wa zahanati katika kila kijiji tumeshauzungumzia kwa nchi nzima kila kijiji kupata zahanati yake. Kipaumbele tutakiweka kwa sehemu za pembezoni lakini vilevile kama tunavyojua kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi nchi nzima, tutakiweka kule zinapojengwa zahanati, mara zitakapokuwa tayari na watumishi watakapokuwa na wenyewe wameongezeka kwa

sababu tumeongeza idadi ya udahili, basi tutawapeleka kule ili kuweza kuziba mapengo kama inavyohitajika.

**SPIKA:** Naona ni vema nimalizie swali la mwisho. Sasa kwa swali hilo namwita Mheshimiwa Rosemary Kirigini.

Na. 186

### **Kurejesha Huduma za MCH**

**MHE. ROSEMARY KIRIGINI** aliuliza:

Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha Vyuo vya Afya na maendeleo ya mama na mtoto vijijini (*MCH*) ambavyo vilisaidia sana kutoa mafunzo kwa vijana?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Kirigini kwamba vyuo vya *MCH* siyo tu kwamba vilisaidia kutoa mafunzo kwa vijana, lakini vilevile wahitimu wake walitoa mchango katika kuboresha huduma ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoleza Bunge lako Tukufu wiki iliyopita wakati najibu swali Namba 68 la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambe, Sekta ya Afya imekuwa na mchakato wa mabadiliko tangu mwaka 1996. Msingi wa Mabadiliko hayo ni kuhakikisha kwamba huduma za afya zinazotolewa zinasogezwa kwa wananchi walio wengi na ni zenye ubora wa hali ya juu na endelevu. Pamoja na mambo mengine, eneo la stadi za watoa huduma liliangaliwa na ikadhihirika haja ya kuwaongezea ujuzi watumishi wa kada ya *MCHA* ili wawe na stadi zaidi katika utumishi wao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tathmini hiyo, kozi ya *MCHA* ilifutwa, *MCHA* waliopo wanaendelea kufanya kazi katika vituo mbalimbali na wamepewa nafasi ya kujiendeleza. Zoezi zima lilipelekea vyuo 11 vya *MCH* kati ya 15 kupandishwa hadhi na kuwa vyuo vya kufundishia Wauguzi Wakunga daraja B ngazi ya cheti. Vyuo vinne vya *MCH* vilivyoko Nzega, Kibondo, Nachingwea na Tunduru vilisimamishwa. Lakini kutokana na mahitaji makubwa ya watumishi yanayohitajika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi, ni mategemeo yetu kwamba vyuo hivi navyo vitakarabatiwa na kuimariswa ili viweze kutoa watalaa wa afya wa fani mbalimbali.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri bado ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba ni vyuo 11 tu ambavyo

vimepandishwa hadhi na kuwa vyuo vya kufundishia Wauguzi Wakunga Daraja B na kwa kuwa bado tatizo la Wauguzi Wakunga katika Mikoa yetu ni kubwa mno. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kufungua vyuo hivi katika kila Mkoa ili kukidhi tatizo hilo? Swali la pili, kwa kuwa vyuo hivi vilivyopo sasa vinaonekana kuchukua wanafunzi wachache sana kuliko mahitaji yaliyopo, je, kuna mkakati gani kabambe wa kuhamasisha wanafunzi ili waweze kujiunga na vyuo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tatizo hili ni kubwa kama nilivyosema, lakini kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, nimesema kwamba, vile vyuo ambavyo vilikuwa vimefungwa ambavyo nililitaja sasa hivi tutavifanya ukarabati na baadaye tutavifungua ili kuweza kuongeza udahili wa wanafunzi ili viweze kuchukua wanafunzi wengi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, nakubaliana naye kwamba wale wanaohitim u ni wachache lakini mkakati kabambe amba o tumeuweka kama Wizara au Serikali ni kwamba tunaongeza idadi ya wanafunzi amba o wanaingia katika vyuo vyote vilivyopo, lakini vilevile tunaongeza madarasa mengine ili tuweze kuongeza idadi ya wanafunzi. Pia mkakati mwingine uliopo ni kwamba, kama pesa itakuwepo basi tutaweza kuongeza katika vyuo vilivyopo katika Mikoa mingine ili kuweza kuongeza idadi ya wanafunzi amba o watachukua mafunzo ya uuguzi. Mkakati mwingine ni kwamba, hatuna haja ya kusema kwamba tuwashawishi kwa sababu sasa hivi wanafunzi wengi wanaohitim darasa la kumi na mbili na la kumi na nne wapo wengi sana amba o wanataka kujiunga na mafunzo ya *nursing*, lakini tatizo ni uhaba wa vyuo. Kwa hiyo, Serikali inajitahidi kuweza kuhakikisha kwamba inaweza kuwachukua wanafunzi hawa ili kuongeza idadi ya wahitim ili kuweza kukidhi mpango wetu wa maendeleo ya afya ya msingi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamekwishajibowi. Sasa ni matangazo, tukianza na wageni. Kwa heshima na taadhima kubwa na pia furaha napenda Waheshimiwa Wabunge nimtambulisse mbele yenu mgeni mashuhuri sana ambaye ni Spika wa Bunge la West Bengal Mheshimiwa Hashim Abdullah Halim, Mbunge na ndiye Mwenyekiti wa CPA. Amekuja kututembelea. (*Makofii*)

*Speaker Halim we feel so much honour to welcome you, you travel very long distance, is very pleasure and honour to have you here in the Parliamentary Chamber in Tanzania. Welcome and we hope you enjoying yourself after a long trip from abroad.*

Wageni wengine ni wageni wa Mheshimiwa Lazaro Nyallandu na mimi amba o ni wahisani amba o wanajitolea katika NGOs mbalimbali kule Marekani kusaidia miradi ya maji, kuongeza nguvu ya ule mradi wa maji wa Benki ya Dunia. Sasa hawa NGO yao inaitwa Tanzania Water Funds na nyingine inaitwa Acacia Capital. Sasa nitawaomba wasimame Bwana Daen Riesen, Bwana Rick Malouf, Bwana John Pearce, Bwana Mike Ebert, Bi Sara Ebsen, Bwana Stuart Graff, Bi Kayla Graff, Bwana Richard Foster, Bwana Chip Thor, Bwana Bill Hamilton na Bwana Humprey Buretta. (*Makofii*)

*We welcome you to the Chamber and we feel very please that you are participate with common people of Tanzania to improve our water supply, as you know water is a top priority for us. I am particularly happy that this morning you are going to Urambo, the authority is there waiting for you very eagerly. Lazima kujifagilia kidogo mambo haya. (Kicheko)*

*I talk to the District Commissioner last night and they have raised the really Tanzanian tradition welcome for you at Urambo. So, I wish you bon voyage and we will see you tomorrow.*

Wageni wetu wengine ni wageni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila, ni Makatibu kumi na sita wa siasa na uenezi CCM kutoka Jimbo la Kwimba. Naomba wasimame pamoa na kiongozi wao ambaye ni Redempter Majigwa. Namwomba kiongozi wa msafara Bi Redempter Majigwa, Katibu wa Siasa Mwenezi wa Wilaya anyooshe mkono tafadhali, yule pale. (*Makofi*)

Halafu watu wanasema akinamama hawawezi. Msafara wote huo unaongozwa na mwanamama. Ahsante sana Bi Redempter na ujumbe wako, tunawatakiwa mafanikio mema. (*Makofi*)

Vilevile kuna wageni wa Mheshimiwa Mariam Kasembe ambao ni watoto wake ambao ni Kulwa Omari na Doto Omari, wale pale, karibuni sana. (*Makofi*)

Vijana wetu wa TAYOA wameendelea kuwa nasi, naomba tena waweze kusimama. Karibuni sana.

Naomba tena nimtambulisse kwenu Bi Madanganya Bihoga ambaye ni mama mzazi wa Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga. Mama asimame pale alipo, yule pale, ahsante sana mama, tunafurahi sana kukuona baada ya safari ndefu kutoka Mwanza, tunatumaini unakaa vema hapa Dodoma kwa siku hizi utakazokuwa nasi.

Sasa ni matangazo ya kuhusu vikao na mikutano. Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw' amenitaka nitangaze kwamba saa 5.00 asubuhi, Kamati ya Huduma za Jamii wakutane ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Mgana Msindai, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) anaomba saa 5.00 hiyo hiyo asubuhi Wajumbe wakutane ukumbi Na. 219.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara anatoa wito kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuwa kutakuwa na kikao leo saa 7.00 mchana ukumbi Na. 133.

Mheshimiwa Jenister Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii anaomba nitangaze kwamba anaitisha kikao cha Kamati hiyo ya Huduma za Jamii,

kuanzia saa 5.00 asubuhi. Hii Kamati yake ni Maendeleo ya Jamii, wameandika hapa Huduma za Jamii, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, wakutane saa 5.00 katika ukumbi Na. 219.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi ananiomba nitangaze kwamba saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi Na. 432 jengo la utawala.

Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi wakutane saa 7.00 mchana katika ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Alhaj Mohammed Missanga ameniomba nitangaze kwamba saa 7.00 mchana leo katika ukumbi Na. 428, Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu wanaombwa kukutana humo.

Mwalimu msaidizi wa michezo, Mheshimiwa Mohammed Rajab anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wachezaji wa timu ya mpira wa miguu na wa mikono (*football and netball*) kwamba timu hizi wakutane saa 5.00 asubuhi kwenye ukumbi wa Pius Msekwa, ni mkutano mfupi tu hautachukua muda mrefu.

Nadhani katika hatua hii ningeomba nifafanue jambo moja ambalo mara nyingi Bungeni hapa wenzetu wanaoliangalia wanalisema. Ukifuatilia matangazo niliyoyatoa uthaona kwamba, zaidi ya nusu ya Wabunge watatoka nje ya ukumbi huu ili kwenda kuhudhuria mikutano ya Kamati. Naomba wananchi watuelewe, Wabunge wanapokuwa katika Kamati wanakuwa katika shughuli za Bunge.

Hawa wenzetu wanaopiga picha za upotoshaji za kuonyesha Wabunge hawapo humu kwa hiyo ni watoro hawatutendei haki. Hata matangazo haya tukiyasikia, Kamati tano zinakutana na kila Kamati ina Wabunge takriban ishirini, ni dhahiri watatoka na kazi ya Bunge inakwenda kupitia Kamati, shughuli hazivivi bila Kamati. Kwa hiyo ningeomba jamii ituelewe kwamba, wanapokuwa hawamo humu wanakuwa kwenye Kamati na wale wadadisi waende kwenye kumbi nilizozitamka, 428, 231,219 kama hawatawakuta Waheshimiwa Wabunge wakifanya kazi zao za Kamati. Niliona ni vizuri niliseme hilo kwa sababu tunatupiwa sana madongo kwamba ni watoro na kadhalika. (*Makofî*)

Nikumbushe tena Wajumbe wa Kamati ya *Richmond* tukutane saa 7.30 Ofisini kwangu leo mchana.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Katibu kwa shughuli zinazofuata, naomba nifafanue jambo moja la kikanuni. Katika mpangilio wa orodha za shughuli leo kuna mchanganyiko unaotokana na kutoku, naomba radhi hatukufuatilia vizuri matakwa ya kanuni.

Kinachoelezea namna ya kupanga shughuli za Bunge ni Kanuni ya 23, Fasili ya (4) inaendelea inazipanga. Sasa ukija kwenye Fasili ndogo ya (j) na (k), mambo yahusuyo haki za Bunge yanatangulia shughuli za Serikali. Nataka mwelewe hilo.

Katika mpangilio huu ilitakiwa shughuli za kanuni zipangwe kwanza kwa sababu kupidisha kanuni ni mambo ya haki za Bunge chini ya Ibara ya 89 ya Katiba.

Kwa hiyo mpangilio sasa utakuwa kama ifuatavyo: Kutakuwa na suala la kanuni halafu Muswada wa *NBC* kusomwa mara ya pili halafu azimio la kusamehe madai kwa Waziri wa Fedha na mwisho Azimio la Itifaki ya *NEPAD*. Kwa hiyo Katibu kwa mpangilio huo.

## HOJA ZA KAMATI

### **Taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Bunge (*Legislature*) ni chombo cha kikatiba kinachojumuisha sehemu mbili, yaani Rais akiwa ni sehemu ya kwanza na Wabunge wakiwa sehemu ya pili.

Sehemu ya pili ya Bunge ina wajibu wa kutekeleza majukumu makuu matatu ya kikatiba ambayo ni:-

- (a) Kutunga sheria (*legislative function*), kwa mujibu wa Ibara ya 64(1) ya Katiba;
- (b) Kuisimamia na kuishauri Serikali (*oversight function*), kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba;
- (c) Kuidhinisha fedha kwa ajili ya matumizi ya Serikali (*appropriation function*), kwa mujibu wa Ibara ya 137(2) ya Katiba;

Ili kuweza kutekeleza majukumu yake ya kutunga sheria, kuisimamia na kuishauri Serikali na kuidhinisha fedha kwa ajili ya matumizi ya Serikali kwa ufanisi unaotakiwa, Bunge linahitaji kuweka utaratibu mzuri wa utekelezaji wa majukumu hayo.

Kwa mujibu wa Ibara ya 100 ya Katiba ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge limepewa uhuru wa kuijiwekea utaratibu wa kutekeleza shughuli zake, katika maneno yafuatayo:-

“Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au Katika Mahakama au mahali penginopo nje ya Bunge”. Aidha, kwa kutumia uhuru huo, Bunge hutunga Kanuni kwa ajili ya kuweka utaratibu wa utekelezaji bora wa shughuli

zake, kwa mujibu wa mamlaka lililopewa na Ibara ya 89(1) na (2) ya Katiba ya nchi zinazotamka ifuatavyo, naomba kunukuu:-

“(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, Bunge laweza kutunga Kanuni za Kudumu kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutekeleza shughuli zake”.

“(2) Kanuni za Kudumu zilizotungwa kwa mujibu wa ibara hii zaweza kuweka utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa shughuli za sekretarieti ya Bunge na pia utekelezaji wa shughuli za Bunge ndani ya Bunge na zile za Kamati na Kamati ndogo za Bunge.”

Mheshimiwa Spika, kuhusu chimbuko la mabadiliko ya Kanuni za Bunge, tarehe 5 Mei, 2006, uliteua Kamati Maalumu ya Bunge na kuipa kazi ya kuzifanya uchambuzi Kanuni za Bunge zilizopo (Toleo la 2004) na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni hizo ili ziendane na wakati na kuliwezesha Bunge kutekeleza ipasavyo majukumu yake ya kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo Maalum ya Bunge iliundwa na Wabunge wafuatao:-

Mheshimiwa Job. Y. Ndugai - Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe - Mjumbe, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono - Mjumbe, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa - Mjumbe, Mheshimiwa Athuman S. M. Janguo - Mjumbe na Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo - Mjumbe.

Baada ya kukamilisha kazi yake, Kamati hiyo ilikabitih taarifa ya mapendekezo yake kwako, ili mchakato wa marekebisho ya Kanuni za Bunge uweze kufuata utaratibu uliowekwa na Bunge.

Mapema Julai, 2006 uliwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakala ya mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Bunge, sanjari na taarifa ya mapendekezo ya kufanya mabadiliko katika Katiba, Sura ya 2, Toleo la 2002, Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge, Sura 115, Toleo la 2002 na Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura 296, Toleo la 2002. Lengo lilikuwa ni kupata maoni ya Serikali juu ya mapendekezo hayo na pia kuifanya Serikali ifikirie na kuanzisha mchakato wa kufanya marekebisho yaliyopendekezwa na Bunge kufanya katika Katiba ya nchi, Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge, Sura 115, Toleo la 2002 na Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura 296, Toleo la 2002.

Tarehe 29 Aprili, 2007 na Mei, 2007, Katibu wa Bunge aliunda Kamati ya wataalam, iliojumuisha wataalam kutoka Ofisi ya Bunge na wataalam kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili kuipitia na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Bunge. Baada ya kukamilisha kazi yake, Kamati hiyo ya wataalam iliwasilisha mapendekezo na ushauri wake kwenye Kamati ya Kanuni za Bunge, katika vikao vyake vilivyofanyika tarehe 29 Aprili, 2007 na 24 Mei, 2007 hadi tarehe 29 Mei, 2007. Katika vikao hivyo, Kamati ya Kanuni za Bunge ilitoa

maelekezo kwa Kamati ya wataalamu kufanya marekebisho kadhaa katika Rasimu ya mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Bunge. Baada ya marekebisho yaliyoelekezwa na Kamati ya Kanuni za Bunge kufanywa, Rasimu hiyo iliwasilishwa kwenye Semina ya Wabunge iliyofanyika tarehe 15 na 16 Agosti, 2007 wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge, kwa lengo la kupata maoni na ushauri wa kuiboresha zaidi Rasimu hiyo kutoka kwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kanuni za Bunge inaundwa chini ya Kanuni ya 97 ya Kanuni za Bunge na majukumu yake yameainishwa chini ya fasili ya (2) ya Kanuni hiyo kuwa ni:-

- (i) Kufikiria na kutoa mapendekezo juu ya kufanya mabadiliko katika Kanuni za Bunge.
- (ii) Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya pendekezo lolote linalohusu Kanuni za Bunge ambalo limepelekwa kwa Kamati hiyo na Spika au na Mbunge yeoyote.
- (iii) Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya lalamiko lolote kuhusu uamuzi wa Spika ambalo limepelekwa kwake na Mbunge yeoyote.

Kwa kuzingatia majukumu haya, Kamati ya Kanuni za Bunge, ilikutana Dar es Salaam, tarehe 24 hadi 29 Mei, 2007 na tarehe 14 Novemba, 2007 hapa Dodoma, kupitia Rasimu ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, iliyozingatia maoni na ushauri uliotolewa na Wabunge kwenye Semina ya Wabunge kuhusu Kanuni hizo na kwa kauli moja Kamati hiyo iliipitisha Rasimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Bunge, naomba kwanza niwatambulisse wajumbe wa Kamati hiyo ambao ni wafuatao Mheshimiwa Samuel J. Sitta, Spika, Mwenyekiti na Mheshimiwa Anne S. Makinda, Naibu Spika, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Pindi H. Chana; Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki; Mheshimiwa Janet B. Kahama; Mheshimiwa Hassan R. Khatib; Mheshimiwa William V. Lukuvi; Mheshimiwa Hamad R. Mohamed; Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe; Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi; Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir; Mheshimiwa Dora H. Mushi; Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye; Mheshimiwa William H. Shellukindo na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa.

Mheshimiwa Spika, katika kuandaa Mapendekezo haya ya Marekebisho ya Kanuni za Bunge, Kamati ilihudumiwa na Maafisa wa Bunge ambao ni Ndugu Oscar Mtenda, Mwanasheria wa Bunge na Ndugu Emmanuel Mpanda, Katibu wa Kamati.

Mhesimiwa Spika, mabadiliko yanayopendekezwa kufanywa katika Kanuni za Bunge. Kwa muhtasari tu, Rasimu ya Mabadiliko ya Kanuni za Bunge ambayo rasimu

yake imegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge, kama Kiambatanisho “A”, inapendekeza mabadiliko mengi ambapo baadhi yake ni yafuatayo:-

Pendekezo la kwanza, Viongozi wa Bunge wanaokalia Kiti cha Spika, kuendesha Shughuli za Bunge kwa haki bila upendeleo. Hiyo itaonekana katika Kanuni ya 8. Pendekezo hili linalenga kuimarisha dhana ya *impartiality* ya Kiti cha Spika kwamba Spika anapokaa pale lazima asiwe na upande wowote.

Pendekezo la pili, Spika na Naibu Spika kuapa viapo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria, Kanuni za 9(20) na 10(4). Pendekezo hili linalenga kuwafanya Spika na Naibu Spika waape viapo vilivyowekwa na Sheria ya Viapo, Sura 266, Toleo la 2002. Mpaka sasa Naibu Spika alikuwa haapishwi, alikuwa anatumia kiapo cha Ubunge tu.

Pendekezo la tatu, Wenyeviti wa Bunge kuwa watatu badala ya wawili wa sasa na uchaguzi wao kuzingatia jinsia na pande za Muungano, hii ni Kanuni ya 11. Pendekezo hili linalenga kuleta uwiano wa kijinsia na uwiano kwa pande mbili za Muungano katika Uongozi wa Bunge.

Pendekezo la nne, Bunge kuwa na Mshauri Mkuu wa Mambo ya Sheria (*Parliamentary Legal Counsel*), hii ni Kanuni ya 21. Lengo la pendekezo hili ni kuliwezesha Bunge kutekeleza jukumu lake la Kikatiba la kutunga sheria kwa ufanisi zaidi kwa kuanzisha Idara ya Sheria chini ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria itakayotoa huduma zifuatazo kwa Bunge na kwa Wabunge:-

(i) Kutoa ushauri wa kisheria kuhusu Miswada yote ya Sheria inayowasilishwa Bungeni;

(ii) Kuchambua Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni na kuwasaidia Wabunge kupata uelewa mzuri wa Miswada hiyo ili kuongeza ubora wa Miswada inayopitishwa Bungeni;

(iii) Kutoa huduma za ushauri wa kisheria kwa Kamati za Bunge na Wabunge;

(iv) Kuandaa Miswada ya Sheria ya Kamati, Miswada Binafsi ya Sheria na Hoja Binafsi za Wabunge;

(v) Kuwasaidia Wabunge kutayarisha Marekebisho ya Miswada (*Schedules of Amendments*) inayowasilishwa Bungeni; na

(vi) Kutoa ushauri kwa Bunge kupitia Kamati ya Kanuni za Bunge kuhusu marekebisho yoyote yanayohitajika kufanyika katika Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mfano, Mabunge ya Nchi nyingi za Jumuiya ya Madola zinazofuata utaratibu wa Kibunge unaofanana na wa Bunge letu (*Westminster Parliamentary system*) kama vile Uganda, Kenya, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Australia, yana Idara kama hiyo ambayo ni muhimu sana katika kuliwezesha Bunge kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kutunga sheria.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tano, shughuli za Bunge kwa Kikao cha Kwanza cha kila Mkutano wa Bunge, tutakuwa tunaanza kwa Wimbo wa Taifa kabla ya kusoma Dua na kikao cha mwisho kufungwa kwa Wimbo wa Taifa, hii ipo katika Kanuni ya 27(2) na 29(3). Pendekezo hili linalenga kujenga Utaifa kwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla. Vile vile pendekezo hili linatoa ishara (*symbolic*) ya umuhimu Kitaifa wa shughuli zinazofanywa na Bunge.

Pendekezo la sita, Kanuni inayohusu kutosema uongo Bungeni kufanyiwa marekebisho, ipo katika Kanuni ya 62. Kutokana na fasili za Kanuni za sasa kuhusu jambo hilo kutokuwa na mtiririko mzuri na unaoelewaka vizuri, Kanuni mpya ya 62 inapendekeza kuwepo mtiririko mzuri zaidi kuhusu jambo hilo.

Pendekezo la saba, Kutambua haki ya raia ya kujitetea na kujisafisha kutokana na kauli zinazotolewa Bungeni, hii ipo katika Kanuni ya 70. Pendekezo hili linalenga kuweka utaratibu wa kutoa haki kwa raia wasio Wabunge kujitetea na kujisafisha kutokana na kauli zinazotolewa hapa Bungeni.

Pendekezo la nane, Bunge kuwa na uwezo wa kuamua iwapo Muswada wowote wa sheria unaowasilishwa kwa dharura unstahili kupitishwa na Bunge kidharura, ipo katika Kanuni ya 79(5). Pendekezo hili lina lengo la kulipa Bunge uwezo wa kuamua kama Muswada uliowasilishwa kwa Hati ya Dharura unstahili kupitishwa kwa dharura ama la. Pendekezo hili pia linalenga kuondoa uwezekano wa utaratibu wa kuwasilisha Miswada ya Sheria kwa Hati ya Dharura kutumika kama njia ya kuwanyima wananchi na wadau mbalimbali kushiriki katika kuboresha Miswada ya Sheria kupitia utaratibu wa ‘public hearing’ uliowekwa na Bunge.

Pendekezo la tisa, Kamati za Kudumu za Bunge kuwa na uwezo wa kuwasilisha Miswada ya Sheria ya Kamati Bungeni, Kanuni 80(1). Pendekezo hili linalenga kuziwezesha Kamati za Kudumu za Bunge ambazo zinafanya kazi zake kwa niaba ya Bunge, kuwa na uwezo wa kuwasilisha Miswada ya Kamati Bungeni badala ya utaratibu wa sasa ambao unaruhusu Serikali na Mbunge binafsi tu kufanya hivyo.

Pendekezo la kumi, Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango katika Mkutano wake wa mwezi wa Januari/Februari ili kujadili na kushauri kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa Fedha unaofuata, Kanuni ya 93. Pendekezo hili linalenga kuliwezesha Bunge kutekeleza jukumu lake la Kikatiba lililoainishwa katika Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba, yaani, kujadili na kuidhinisha

mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano.

Pendekezo la kumi na moja, Kamati za Bunge kufanya kazi zake kwa uwazi, Kanuni ya 111(9) na Nyongeza ya VII. Katika zama hizi za uwazi na ukweli na kwa kuzingatia utaratibu wa ‘*public hearing*’ kwa Miswada ya Sheria uliowekwa na Bunge, ni dhahiri kabisa kuwa utaratibu wa Kamati za Kudumu za Bunge kufanya kazi zake kwa usiri umepitwa na wakati. Aidha, kutokana na ukweli huo, pendekezo hili linalenga kubadili utaratibu uliokuwepo wa Kamati za Kudumu za Bunge kufanya kazi zake kwa usiri na badala yake kufanya kazi kwa uwazi na hivyo kutoa haki ya msingi kwa wananchi kupata habari, isipokuwa tu pale ambapo Kanuni na Taratibu zinaelekeza kuwa jambo hilo lisiwe wazi.

Pendekezo la kumi na mbili, Taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge kuwasilishwa na kujadiliwa Bungeni, Kanuni ya 112(15). Pendekezo hili linalenga kuzipa umuhimu unaostahili Taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge katika utekelezaji wa jukumu la Kikatiba la Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali. Aidha, pendekezo hili linalenga kuweka utaratibu bora, wa uhakika na wa lazima (*mandatory*) kwa Taarifa za Kudumu za Bunge kujadiliwa Bungeni katika Mikutano ya Bunge lengo likiwa ni mapendekezo na ushauri unaotolewa na Kamati hizo kwa Serikali uzingatiwe na kufanyiwa kazi na Serikali.

Pendekezo la kumi na tatu, kuweka mpangilio mzuri, kuunganisha baadhi ya Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na majukumu yake na kuziweka chini ya Nyongeza ya Sita, Kanuni ya 113 na 114. Lengo la pendekezo hili la kuweka mpangilio mzuri, kuunganisha baadhi ya Kamati na kuziweka chini ya Nyongeza ya Sita, Kamati za Kudumu za Bunge ni kuleta ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hizo na pia kumuwezesha Spika kufanya mabadiliko ya majina na majukumu ya Kamati hizo pale ambapo Serikali itafanya mabadiliko katika Wizara zake bila ya Kamati ya Kudumu ya Kamati za Bunge kulazimika kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge kila wakati mabadiliko ya Wizara yanapofanywa na Serikali

Pendekezo la kumi na nne, kuweka utaratibu mzuri kuhusu usalama wa maeneo ya Bunge, hii ni Kanuni ya 139 na 140. Pendekezo hili linalenga kuimarisha usalama kwa Wabunge na kwa maeneo ya Bunge ili vitendo vya kuhatarisha usalama wa Wabunge visiweze kutokea.

Pendekezo la kumi na tano, kuunda Kamati mpya za Kudumu ya Sheria Ndogo (*by laws*), masuala ya Ukimwi na Hesabu za Mashirika ya Umma, kifungu cha 1(1)(d)(e) na Kifungu cha 10(1)(c) cha Nyongeza ya VI. Sheria zote Ndogo hutungwa kutokana na mamlaka yaliyokasimiwa na Bunge kwa vyombo vinavyotunga sheria hizo, chini ya

Sheria Mama zilizotungwa na Bunge. Kwa kuwa mamlaka yote ya kutunga sheria yapo mikononi mwa Bunge, ni wajibu wa Bunge kuhakikisha na kujiridhisha kwamba, mtu au chombo chochote kinachotumia mamlaka yanatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuundwa kwa Kamati mpya ya Sheria Ndogo kutawezesha Bunge kutekeleza wajibu huo wa kupitia na kuhakikisha kuwa Sheria zote Ndogo zinazotungwa na mtu au chombo kilichokasimiwa madaraka ya kufanya hivyo havikiuki masharti na matakwa ya Sheria Mama au Sheria nyingine zilizopitishwa na Bunge. Vile vile pendekezo hili linalenga kuanzisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kuratibu Masuala ya Ukimwi na Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Mashirika ya umma.

Pendekezo la kumi na sita, Kamati za Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuwa na Wenyeviti kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Kifungu cha 10(1)(a) na (b) cha Nyongeza ya VI. Mabunge yote ya nchi za Jumuiya ya Madola zenye mfumo wa Kibunge unaofanana na unaofuatwa na Bunge letu, Kamati hizi ambazo zinajulikana kama ‘*watchdog committees*’ huongezwa na Wenyeviti kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Mantiki ya pendekezo hili ni kuhakikisha kwamba jukumu la Kikatiba la Bunge la kuisimamia Serikali na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake (*oversight function*), linatekelezwa ipasavyo pasipo hofu ya uwezekano wa jukumu hilo kuwa ‘*compromised*’ iwapo Kamati hizo zitaongezwa na Wenyeviti kutoka Chama Tawala. Vile vile pendekezo hili lina lengo la kuhakikisha kuwa, dhana ya uwajibikaji (*accountability*) ya Serikali kwa wananchi kupitia Bunge inaonekana wazi kuwa inatekelezwa.

Pendekezo la kumi saba, kuweka utaratibu mzuri wa kuendesha shughuli za Kamati za Bunge, Nyongeza ya VII. Pendekezo hili linalenga kuwa na utaratibu mzuri utakaotumika katika kuendesha shughuli za Kamati za Bunge ili kukuza ushiriki na ufuutiliaji wa wananchi na kuweka uwazi kwa shughuli za Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, ambaye kila alipoombwa, alitoa wataalamu kutoka katika Ofisi yake ambao walisaadiana na wataalamu wa Ofisi ya Bunge kuandaa Rasimu ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayowasilishwa hapa Bungeni leo kwa ajili ya kupitishwa. Aidha, ninawashukuru pia wataalamu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wa Ofisi ya Bunge ambao wamefanya kazi kubwa ya kuwezesha mchakato wa marekebisho ya Kanuni za Bunge kufikia katika hatua ya kuwasilishwa Bungeni ili zipate kibali cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ni matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge wataipokea na kwa kauli moja, wataikubali hoja iliyopo mbele yetu na kuipitisha ili tuweze kuboresha Kanuni za Bunge na kuimarisha uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofī*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hamkuelewa vizuri nini? Mnatakiwa kuunga mkono, hii ni hoja!

**MHE. JANET M. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.  
(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa kwa sababu imekwishatolewa na kuungwa mkono, sasa inaweza kujadiliwa. Lakini sijapata ombi lolote kwa maandishi la kutaka kuchangia. Nadhani ni kwa sababu suala hili linajieleza tu lenyewe au sivyo? (*Makofit*)

Wahesimiwa Wabunge, kwa hiyo nitamwita mtoa hoja kama ana jambo lolote la kuongezea kwa sababu hakuna mchango wowote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, ninaamini ni kwa sababu walishiriki wote katika ngazi mbalimbali, tulianza kwenye Kamati yenyewe, wataalam, halafu tukawa pia na semina ile ambayo Waheshimiwa Wabunge walitoa mawazo yao mengi zaidi na watayaona katika Kanuni zetu. Mheshimiwa Spika, lakini ombi langu kwa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba kazi ambayo inapaswa kufanywa ndani ya Bunge hasa tunapozungumza *impartiality* ya Kiti cha Spika ni kwa Waheshimiwa Wabunge kujua Kanuni. Waheshimiwa Wabunge wakijua Kanuni, uendeshaji wa shughuli zetu hizi utakuwa unaonekana unatenda haki. Wakati huo huo, wakumbuke kwamba Kanuni zetu zimeundwa na pande zote za Vyama vilivyopo humu ndani. Kwa sababu leo ni Kanuni zinazoendeshwa na Chama Tawala cha CCM, kesho inawezekana ikawa Chama kingine chochote ili kusudi Kanuni zisiwe na tofauti kwamba leo ni za upande huu na kesho za upande mwengine. Hizi ni kanuni za Watanzania na Bunge letu kwa wakati wote mpaka pale zikihitajika kufanyiwa marekebisho, tutayaleta kwa utaratibu unaohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili kuhitimisha suala hili rasmi, naomba nisome Azimio ambalo pia litapigiwa kura.

#### **AZIMIO LA KUFANYA MABADILIKO KATIKA KANUNI ZA BUNGE**

**KWA KUWA** kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2)(ii) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, moja ya majukumu ya Kamati ya Kanuni za Bunge ni kuchunguza na kutoa taarifa juu ya pendekezo lolote linalohusu Kanuni za Bunge;

**NA KWA KUWA** Kamati ya Kanuni za Bunge ilikutana Dar es Salaam tarehe 24 – 29 Mei, 2007 na Dodoma tarehe 14 Novemba, 2007 kuchunguza mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Bunge kama inavyoonekana kwenye Kiambatanisho cha “A” cha Kanuni tulizowagawia na kwa kauli moja kupitisha mapendekezo ya marekebisho hayo;

**KWA HIYO BASI** kwa mujibu wa Kanuni ya 125(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linalokutana katika Mkutano wa Tisa, linayapokea na kuyakubali kwa kauli moja mapendekezo ya mabadiliko katika Kanuni za Bunge kama yalivyowasilishwa kwenye Rasimu ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kiambatanisho “A”.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kutoa hoja. (*Makofî*)

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kuwasilisha hoja hii na Azimio lake vizuri sana. Sasa kilichopo mbele yetu ni pendeleko la Azimio kuzipitisha Kanuni Mpya za Bunge kwa maana ya mabadiliko hayo makubwa yaliyokwishafanyika kwenye Toleo la 2007. Toleo la Kanuni tunalotumia ni Toleo la Kanuni la 2004. Mabadiliko yaliyosomwa na Mheshimiwa Naibu Spika na kuungwa mkono kwa maana hakukuwa hata na mjadala, yanahusu sasa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 tulilolifanya kazi kwa miezi takriban 14. Kwa hiyo, sasa nitawahoji kwa maana ya kuafiki mabadiliko hayo na kutuwezesha sasa tuweze kuchapisha Kanuni za Bunge Mpya.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Bunge lilipokea na kupidisha Kanuni Mpya za Bunge*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Bunge Zima, limeafiki kupidishwa kwa Kanuni za Bunge Mpya, nawashukuru sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe tangazo la ziada. Kanuni hizi hazitaanza kutumika hadi katika Mkutano wa Kumi. Kwa mfano, Kanuni za Bunge, zimeruhusu kuval tarabushi lakini simtegemei Mheshimiwa Nimrod Mkono, kesho avae tarabushi hapa. Tumeruhusu mambo mengi tu. Tumeruhusu baragharia na yapo mengi ambayo Mheshimiwa Naibu Spika, hakuyasema. Napenda msome hizo Kanuni za Bunge, zina mabadiliko makubwa sana. Kuanzia kwenye Mkutano wetu wa Kumi, mwezi Januari au Februari, 2008 itakuwa ni sahihi kwa Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kuval kaunda suti nzuri na baragharia. Hayo yote ni mazuri tu ambayo yamepitishwa na Kanuni. Niliona nilisema hilo ili tuelewane kwa sababu bado tuna siku ya kesho kuhitimisha Shughuli zetu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninahitajika kukutana na mgeni wetu Mwenyekiti wa CPA na kwa hiyo, namwomba Mwenyekiti, Jenista Mhagama, aje aendelee kusimamia shughuli za Serikali zilizobaki.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Baada ya kumaliza ajenda ya kupitisha Kanuni zetu za Bunge, sasa tuendelee na ajenda inayofuata inayohusu Serikali, Katibu!

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho katika Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara wa Mwaka 2007 (*The National Bank of Commerce Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities*) (Amendment) Bill, 2007.**

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara wa Mwaka 2007 (*The National Bank of Commerce Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities*) (Amendment) (No.2) Act, 2007 pamoja na marekebisho yake, sasa Usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imezingatia kwa dhati michango ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambayo imesaidia sana katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada uliopo mbele yako, unakusudia kuifanyia marekebisho Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara, Sura ya 404 yaani “*The National Bank of Commerce (Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities) Act, Chapter 404*” ili kuweka utaratibu wa kisheria utakaowezesha Shirika Hodhi la Benki yaani *Consolidated Holding Corporation* kwa kifupi *CHC* kutwaa na kuendeleza shughuli ambazo hazikukamilishwa na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma yaani *Presidential Parastatal Sector Reform Commission* kwa kifupi *PSRC* baada ya muda wa Tume hiyo kufikia ukomo wake tarehe 31 Desemba, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma yaani *PSRC*, iliundwa mwaka 1993 baada ya kufanya marekebisho Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992 kupitia marekebisho ya mwaka 1993 yaani *The Public Corporation (Amendment,) Act 1993*. Sheria hii iliipa *PSRC* kipindi cha miaka 10 hadi

mwezi Desemba, 2003 iwe imekamilisha majukumu iliyopewa ikiwa ni pamoja na kurekebisha na kubinafsisha Mashirika ya Umma yapatayo 400.

Hata hivyo, hadi kipindi hicho kinaisha mwishoni mwa mwaka 2003, Tume pamoja na majukumu mengine iliyopewa ilikuwa bado haijaweza kukamilisha kurekebisha na kubinafsisha Mashirika 77. Kutokana na hali hiyo, Serikali iliridhia kuongeza muda wa shughuli za *PSRC* kwa kipindi kingine cha miaka minne baada ya muda wake kumalizika tarehe 31 Desemba, 2003.

Aidha, Serikali iliwasilisha Bungeni Azimio Na.21/2003 kwa ajili ya kupatiwa idhini ya Bunge. Azimio hilo lilipitishwa na Bunge kwa kurekebisha Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura namba 257 na hivyo *PSRC* ikaongezewa muda wa kutekeleza majukumu yake yaliyosalia kuanzia tarehe 1 Januari, 2004 hadi tarehe 31 Desemba, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuongezewa muda huo wa miaka minne bado yapo majukumu ambayo *PRSC* haijaweza kuyakamilisha. Majukumu hayo ni pamoja na:-

- Kusimamia mashauri yaliyopo Mahakamani ambayo ni takriban 129;
- Ukamilishaji wa urekebishaji na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma yapatao 35;
- Uratibu wa mauzo ya hisa za Serikali kupitia Soko la Mtaji na hisa yaani *initial public offering*;
- Ukusanyaji wa madeni kuhusiana na mikataba ya mauzo yenyeye thamani ya shilingi bilioni 8,151,000,000/=;
- Kusimamia na kulipa madeni ambayo Tume inadaiwa yenyeye thamani ya shilingi bilioni 7,223,000,000/=;
- Ufuatiliaji wa Hatimiliki za Mashirika ya Umma ambayo yapo katika mchakato wa ubinafsishaji, hadi mwezi Oktoba, 2007 zaidi ya Hati 70 zilikuwa zinafuatiliwa.

Aidha, *PSRC* ilikuwa na jukumu la ufuatiliaji na usimamiaji wa uanzishwaji wa Mamlaka ya Udhibiti yaani *Regulatory Authorities* ikiwa ni pamoja na kuzijengea uwezo

wa kitaaluma yaani *Capacity Building*. Mamlaka za Udhibiti hizo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (*EWURA*), Tume ya Ushindani wa Haki za Kibiashara (*FCC*), Baraza la Rufaa na Ushindani wa Haki za Kibinadamu (*FCT*) na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) ambazo zipo katika hatua mbalimbali za uanzishwaji na ukamilishwaji wake.

Vilevile Wizara ya Fedha inawasiliana na Benki ya Dunia kuhusu fedha zilizotolewa kwa ajili ya Mradi wa *Privatization and Public Sector, Development Project and ACDP* ambazo zingesimamiwa na *PSRC* ili waweze kupewa *Consolidated Holding Corporation* ili kukamilisha majukumu yaliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa kuna shughuli ambazo zitakuwa hazijakamilika kama zilivyotajwa hapo juu, Serikali imeamua kuwa *PSRC* imalize muda wake ifikapo tarehe 31 Desemba, 2007, muda ambao uliridhiwa na Bunge lako Tukufu. Shughuli zitakazobakia zitahamishiwa *Consolidated Holding Corporation*.

Aidha, katika kutekeleza maamuzi ya Serikali, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, *Consolidated Holding Corporation* pamoja na *PSRC*, zimeunda Kamati Maalum inayoendelea kufanya uchambuzi wa kina wa shughuli ambazo hazitakuwa zimekamilika na kubainisha uwezo wa kitaaluma ilionao *CHC* ili kabla ya tarehe 31 Desemba, 2007 uamuzi uwe umefanyika ikiwa ni pamoja na kuainisha aina ya wataalam wanaopaswa kuhamishiwa *CHC* kutoka *PSRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu. Ili kuiwezesha *CHC* kutekeleza majukumu mapya ya kuchukua shughuli zitakazoachwa na *PSRC*, inapendekezwa kuifanyia marekebisho Sheria ya Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara, Sura ya 404, kama ilivyorekebishwa ili kuiwezesha *CHC* kutwaa na kuendeleza shughuli ambazo hazitakamilishwa na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma baada ya muda wa Tume hiyo kufika ukomo tarehe 31 Desemba, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu katika Muswada huu. Baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na kuhamishia kwa *CHC* majukumu ya Kisheria iliyopewa *PSRC* chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura 257 yaani *The Public Corporation Act, Chapter 257* na pia kubainisha marekebisheso yanayopaswa kufanyika chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma katika kuhakikisha *PSRC* inafikia ukomo wake tarehe 31 Desemba, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpangilio wa Muswada, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwenza, yenye kifungu cha 1, inayohusu masuala ya utangulizi inayojumuisha jina la sheria na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii.

Sehemu ya Pili ya Muswada, ina kifungu cha 2 - 5. Kifungu cha 2 kinaongeza tafsiri ya neno “Commission” yaani “*Presidential Parastatal Reform Commission*” katika sheria hii. Kifungu cha 3 kinapendekeza kurekebisha kifungu cha 6(d) na (e) na kifungu kidogo cha 1(a) cha Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara, Sura ya 404 kwa kuongeza neno “Commission” ili kuhuisha majukumu ya PSRC na CHC. Aidha, katika kifungu cha 4 inapendekezwa kuongezwa kifungu kipyta cha 6A ambacho kitabainisha majukumu mapya yaliyoongezewa CHC kuhusiana na kutwaa na kuendeleza shughuli ambazo hazikukamilishwa na PSRC baada ya muda wa Tume hiyo kufikia ukomo. Vile vile kifungu cha 5 kinapendekeza kurekebisha kifungu cha 8 kwa kuongeza neno “Commission”.

Sehemu ya Tatu na ya mwisho ya Muswada yenyewe kifungu cha 6 - 8. Inapendekeza kufanya marekebisho Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura 257 yaani “*The Public Operations, Act, Chapter 257*”. Kwanza chini ya kifungu cha 6 kuondoa majukumu yote katika sheria hii yanayohusu Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma na kuyahamishia CHC.

Pili, kifungu cha 7 kinapendekeza kurekebisha kifungu cha 3 cha sheria hii ili kufuta tafsiri ya maneno “*Commission, Chairman, General Fund* na *Member* ambayo hayatatumika tena katika sheria hii. Aidha, kifungu hicho kinapendekeza kuongeza tasfiri ya neno “*Corporation*” yaani “*Consolidated Holding Corporation*”.

Tatu, kifungu cha 8 kinapendekeza kurekebisha vifungu vya 14, 15, 16, 18, 20, 38, 39(1)(2), 40(1)(2) na (3), 42(b) na (d), 43(1)(2), 44(1)(2), na 45A(1)(2) vya Sheria ya Mashirika ya Umma ili kuondoa rejea yaani *reference* zinazohusu Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma na kuweka *substitute corporation*. Aidha, kifungu hicho, kinapendekeza kufuta sehemu zifuatazo 5, 6, na 7 vya sheria hii ili kuondoa PSRC pamoja na majukumu yake katika sheria hii.

Kifungu cha 40A(1)(a) na (c) kinafuta rejea ya neno “*Commission*” na kuweka *substitute* neno “*Responsible Minister*”

Kifungu cha 40A(1)(c) kinafuta inayojitokeza mara ya pili na kuweka neno “*Corporation*” na neno “*Commission*” linalojitokeza mara ya 3 kwa kuweka neno “*Responsible Minister*”.

Vifungu vya 41 na 45 vya Sheria hii vinafutwa. Kifungu cha 42(c) kinapendekezwa kufuta “*Commission*” under the hands of the Chairman” na kuweka maneno “*The Board of the Corporation*”. Aidha katika kifungu hiki cha 8 kinapendekeza kuongeza kifungu kipyta cha 45B(1)(2)(3)(4) na (5), kitakachohusu kuwepo kwa “*special fund*” itakayotumika kukusanya fedha zote za mauzo na urekebishihi wa Mashirika ya Umma Mfuko ambao utasimamiwa na Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada uliopo mbele yenu na hatimaye likubali kuitisha kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

## **WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki**

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwasilisha Muswada huo mbele ya Bunge na baada ya kutoa hoja yako na kuungwa mkono, Waheshimiwa Wabunge sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, naona ni Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati, tafadhali na baadaye basi Msemaji wa Kambi ya Upinzani ajiandae.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi baada ya kukamilisha kazi ya kuchambua na kujadili Muswada wa Sheria ya kufanya Marekebisho kwenye Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara (Na.2) ya Mwaka 2007 (*The National Bank of Commerce (Re-organisation And Vesting of Assets and Liabilities)(Amendment) (No.2) Bill,2007*) kwa Mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha maoni ya Kamati, naomba niungane na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia ya marehemu Salome Joseph Mbatia na Taifa kwa ujumla kwa kumpoteza kiongozi wake mahiri na shupavu. Mungu amlaze mahali pema peponi, amen.

Aidha, kwa niaba ya Kamati, naomba kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum kwa ajali walizopata mwaka huu 2007. Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopata madhara mbalimbali pamoa na misiba ya kuondokewa na ndugu zao kwa mwaka huu 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa Nane wa Chama cha Mapinduzi uliomalizika hivi karibuni pale Kizota – Dodoma, kwa kazi kubwa na nzuri waliofanya ya kumchagua kwa kura nyingi Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa. Pia nawapongeza kwa kufanya kazi kubwa ya kumpa kura nyingi Rais Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kuwa Makamu wa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar. Vile vile niwapongeze kwa kumchagua kwa kura nyingi, Mheshimiwa Pius Msekwa, kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Tanzania Bara. Niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa za uongozi katika Chama chetu baada ya uchaguzi uliopita wa CCM. (*Makofî*)

Aidha, naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wa Kamati yangu, Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Waziri wa Fedha, kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu naye kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru sana Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM, Mkoa wa Tanga, kwa imani walionyesha kwangu kwa kunipa kura nyingi sana hata nikafanikiwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri ya Taifa wa Chama cha Mapinduzi. Vile vile nawashukuru Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (*NEC*) kwa kunichagua kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi. Nawashukuru sana na nawaahidi utumishi ulio adilifu wa Chama chetu lakini pia kwa faida ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kilichofanyika tarehe 25/10/2007 na kuhudhuriwa na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha, pamoja na Menejimenti ya *PSRC*, kilitafakari kwa undani hatma ya *PSRC* kuhusu kumalizika kwa muda wa utekelezaji wa majukumu yaliyosalia baada ya *PSRC* kufika ukomo wa uhai wake ifikapo tarehe 31 Desemba, 2007. Hoja ya hatima ya *PSRC* ilijadiliwa na Kamati yangu mwaka jana, wakati ikipitia Taarifa ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Mwaka 2005/2006. Kamati iliomba Serikali kuanza kuifanyia kazi suala hili la ukomo wa *PSRC* na Kamati ilipendekeza masuala mbalimbali ya kuzingatiwa ikiwa ni pamoja na kuboresha utekelezaji wa zoezi la ubinafsishaji wa Mashirika yaliyosalia ili matatizo yaliyojitokeza katika Mashirika yale yaliyobinafsishwa yasijirudie.

Aidha, Kamati iliishauri Serikali na *PSRC* ifanye tathmini ya Mashirika yaliyokwisha binafsishwa ili kubaini mafanikio, matatizo na utekelezaji wa makubaliano kulingana na mikataba ya ubinafsishaji huo. Kamati ilipendekeza *PSRC* ifanye kazi hii ya *Post Privatization Monitoring* ili kubaini ukiukwaji wa makubaliano ya misingi na kupendekeza hatua stahili ili kuongeza mchango wa ubinafsishaji kwa uchumi wa Tanzania na maslahi ya jumla kwa wananchi wa Taifa letu. Katika suala hili, Kamati ilitoa ushauri wa kuzingatiwa na Serikali ili kazi zilizosalia zitekelezwe kwa ukamilifu na hivyo suala la ukomo au la wa *PSRC* lizingatie utekelezaji kwa ukamilifu wa majukumu yaliyosalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imetafakari kwa kina hoja hii na inatoa ushauri na maangalizo yafuatayo kwa Serikali. Kamati inaelewa kuwa zoezi la ubinafsishaji kama mkakati wa kuboresha uchumi wa nchi yetu (*economic reform*) ni mkakati endelevu na utachukua kipindi kirefu kijacho, hata baada ya Taasisi ya *PSRC* hivi sasa kuongezwa muda wake uliopendekezwa. Hoja iliyopo mbele yetu inajitokeza sasa kwa mara ya tatu tokea *PSRC* ilipoanza shughuli zake mwaka 1993. Mara kwa mara kipindi hiki kinapofika huwa kinaleta majadiliano mazito kati ya Bunge na Serikali kama

muda wa *PSRC* uendelee au la, mara pale unapofika ukomo wake. Hivi sasa ni mara ya tatu kwa maombi kuletwa kama muda wa *PSRC* uongezwe au la, baada ya kufanya kazi zake kwa muda wa miaka 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tokea *PSRC* kuanza kazi zake hadi sasa, utaalim mkubwa wa utendaji kazi wa kiufundi (*technical expertise*) umepatikana; uzoefu mkubwa umepatikana; ujuzi mkubwa umepatikana pamoja na tija na ufanisi. Aidha, *PSRC* umejenga uwezo mkubwa katika eneo la Teknohana pamoja na uwekaji wa taarifa na takwimu (*data bank*). Hatuwezi kukataa kuwa, pamoja na *PSRC*, kufikia ukomo wake, imetujengea hazina kubwa ya yote hayo katika uchumi wetu. Kwa mfano tu katika kipindi cha 1999 hadi 2003 yalirekebishwa Mashirika yaani viwanda 90 na mali nyingine 215 na kutoka mwaka 2003 hadi 2007 yamerekebishwa Mashirika 44 pamoja na mali nyingine 389.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu wetu umetuonyesha kuwa utaratibu tuliojiwekea hususan unaohusu uhai wa *PSRC*, unakifanya chombo hiki kisiwe cha kudumu. *Hansard* ya tarehe 13/11/2003 nanukuu:-

*“...Tume si chombo cha kudumu, ni chombo ambacho kimeridhiwa kutekeleza Sera ya Taifa ya Ubinafsishaji ...”*

Hali hii ndiyo iliyotifikisha hatua hii tuliyopo sasa ya kutaka kuongeza muda wa uhai wa *PSRC* kwa ridhaa ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepukana na hali hii, hasa tukizingatia kuwa mkakati wa ubinafsishaji na shughuli zinazoambatana nazo ni endelevu na za muda mrefu, Kamati yangu inashauri kuwa umefika wakati sasa Serikali iunde kisheria chombo cha kudumu au taasisi ya kudumu kuendeleza urekebishaji wa uchumi wetu kupitia utaratibu wa ubinafsishaji wa Mashirika yetu ya Umma ili kiendelee kukamilisha kazi ya urekebishaji wa Mashirika yaliyobakia pamoja na majukumu mengine. Hili ni suala la lazima hasa ikizingatiwa kuwa yapo majukumu muhimu yanayohitaji kutekelezwa:-

Kwanza, katika mchakato wa ubinafsishaji bado yapo Mashirika muhimu ambayo urekebishaji wake haujakamilika. Mashirika haya yanayofikia 41 ni pamoja na *NIC*, *TRC*, *NMB*, *TANESCO*, *TAZARA*, *GENERAL TYRE* na kadhalika;

Pili, yapo mashauri 129 yanayoendelea hivi sasa Mahakamani ambayo bado hayajapata ufumbuzi wake;

Tatu, *PSRC* inayomaliza ukomo wake tarehe 31/12/2007, ilikuwa na jukumu la kusimamia uundwaji wa Mashirika ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Madini (*EWURA*), Tume ya Ushindani Haki za Biashara (*Fare Trade Competition - FTC*) na Baraza la Rufaa la Ushindani Haki Kibiashara (*Fare Competition Tribunal - FCT*) ambazo hadi hivi sasa ziko katika hatua za mwanzo za utendaji kazi. *EWURA* ilianza kufanya kazi Juni 2006, *FCC* Machi, 2007 na *FCT* inategemewa kuanza Novemba 2007.

Kwa kuwa dhana nzima ya Udhibiti (*Regulatory Authorities*) ni ngeni, *PSRC* ilipewa jukumu la kuratibu mipango ya kujenga uwezo wa Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*), Mamlaka ya Usalama wa Anga (*TCAA*) na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*); na

Nne; *PSRC* pia ilikuwa inasimamia fedha za mkopo wa Benki ya Dunia kuitia mradi wa *Privatisation and Private Sector Development Project (PPSDP)*, chini ya makubaliano ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Mkopo huu utaendelea kufadhili Mamlaka hizi hadi mwaka 2009 mradi utakapofungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu haya ndio yaliyoishawishi Kamati kuishauri Serikali sasa iunde kisheria chombo cha kudumu kwani hata huo muda wa uhai unaoombewa *PSRC* hautatosha kukamilisha majukumu hayo yote yaliyoorodheshwa, hasa ikizingitiwa kuwa *CHC* ni chombo cha muda ambacho kinatarajiwa kukamilisha majukumu yake katika kipindi cha miaka mnne ijayo. Aidha, majukumu yote hayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu na hatuwezi kujifanya hatuoni umuhimu huo na kwamba tutakoma kutekeleza majukumu hayo. Majukumu haya kama yanavyoonekana ni mazito hivyo chombo hicho cha kudumu kitakachoundwa kuendeleza kufanya kazi zilizokuwa zikifanywa na *PSRC* hakina budi kuwa chombo huru kinachojitegemea na kilichofungasha wataalam muhimu waliokuwa *PSRC*, kabla ya mwisho wa uhai wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Serikali, ni kupendekezwa kutungwa kwa Sheria ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara, Sura ya 404. Lengo kubwa ni kutaka: -

- (a) Shirika Hodhi la Benki (*CHC*) kutwaa na kuendeleza baadhi ya shughuli za *PSRC* na;
- (b) Kuweka masharti yatakayowezesha Wizara zinazosimamia Mashirika ambayo hayatakuwa yamebinafsishwa hadi tarehe 31 Desemba, 2007 yabinafsishwe chini ya usimamizi wa Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu haina pingamizi na wazo la Serikali la kutaka *CHC* kutwaa na kuendeleza shughuli za *PSRC* inayofikia ukomo wake. Hata hivyo, Kamati inadhani ni vyema utaratibu utakaofanyika kufikia lengo hilo uwe ni ule wa-convenience tu na usio wa kudumu (*temporary*) na uruhusu chombo hicho kipyta kitakachoundwa kuwa ni idara (*division*) au sehemu (*appendage*) chini ya mwamvuli wa *CHC* itakayoshughulikia kwa ukamilifu shughuli zote zilizokuwa zinafanywa na *PSRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ina sababu kadhaa za kuishauri Serikali kwa njia hii kwanza, *CHC* hivi sasa ina majukumu mengi na hivyo haitakuwa busara kuitwisha mzigo wa ubinafsishaji na urekebishaji uliokuwa ukifanywa na *PSRC*. *CHC* bado inashughulikia masuala ya *NBC*, Simu 2000, *LART* na *ATC* na kadhalika. Mzigo huu ni mkubwa na *CHC* kuongezewa moja kwa moja mzigo mwingine bila ya utendaji

huru wa chombo hicho kipyä kitakachokuwa na majukumu ya kubinafsisha na yote yaliyokuwa yakifanywa na *PSRC* ambayo yalikuwa cha yanatarajiwa yaendelee kutekelezwa na *PSRC* inayofikia ukomo wake 31 Desemba, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa tahadhari kwa Serikali ili tusije tukadumaza tija na ufanisi wa mkakati wa ubinafsishaji uliochangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wetu. Kati ya mafanikio makubwa yaliyopatikana kupitia zoezi la ubinafsishaji ni pamoja na kukuza ajira na kupanua wigo wa makusanyo ya kodi (*widening of tax base*) ambao umesaidia sana Bajeti ya Serikali. Hivi sasa TRA inakusanya takribani Sh.230 bilioni kwa mwezi, ikilinganishwa na Sh.25 bilioni kwa mwezi katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Pili, kwa kuwa Kamati yangu inasimamia shughuli za *CHC* pamoja na zile zilizokuwa za *PSRC* na inazifahamu kwa mapana, Kamati inatoa tahadhari kuwa uamuzi wa kuiweka *PSRC* chini ya *CHC* ufanywe kwa namna ambayo haitakwaza utekelezaji wa majukumu yote muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa *PSRC*, *CHC* pia ni chombo cha muda ambacho ukomo wa uhai wake utafikia mwaka 2011. Kulingana na majukumu ya *CHC*, sasa na yale yaliyoainishwa ya *PSRC* ambayo yote yanahamishiwa *CHC*, ni dhahiri kuwa hata ifikapo 2011 *CHC* haitakuwa imekamilisha majukumu yake yote, hasa ilizingatiwa shughuli zote zitakazofanywa na *CHC* pamoja na zile zilizokuwa *PSRC* zina uhusiano wa moja kwa moja na ujenzi wa uchumi wetu wa Taifa. Kwa hiyo, Kamati yangu inaona na kuishauri Serikali kuwa kuhamishia majukumu ya *PSRC* (mzigo mkubwa) kwenda *CHC*, ni kutafuta ufumbuzi wa tatizo la muda mrefu, kwa hatua za muda mfupi na zisizoendelevu. Kamati inaamini kuwa kama tunavyojikuta sasa katika majadiliano mazito kati ya Bunge na Serikali ya kuongeza muda wa taasisi fulani au la, suala hili au hali hii itajiruidia tena muda si mrefu kuanzia sasa pale tutakapotakiwa tuongeze muda wa *CHC* au la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii, Kamati yangu inaishauri Serikali kuanzia sasa ijikite katika mkakati wa kuunda muundo mpya na wa kisheria wa chombo cha kudumu ambacho kitaunganisha/kitajumuisha kazi na majukumu ya Taasisi au vyombo vyote viwili *CHC* na *PSRC* pamoja na yale majukumu ya ziada yaliyopendekezwa na Kamati yangu ya *Post Privatisation Monitoring and Follow up* na lile la *Public – Private Partnership Agency*. Chombo hicho kitengenezewa utaratibu wa kudumu na wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, Kamati yangu inaishauri Serikali katika kipindi cha miezi sita kuanzia 31 Desemba, 2007 hadi tarehe 01 Agosti, 2008 uwe ni wakati kwa Serikali kujiandaa na uanzishwaji wa chombo hicho kipyä cha kudumu, kisheria, kitakachojuisha majukumu ya *CHC* na *PSRC*. Wakati huo huo, Taasisi hizi mbili (*PSRC/CHC*) zikijiandaa kwa utaratibu wa kuunganisha majukumu yao, pamoja na kufunga shughuli zake (*winding up*) ambazo hazitaendana na utaratibu mpya wa *superstructure* huo mfumo mpya unaopendekezwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya muda huo, Kamati inaishauri Serikali kuleta Muswada mbele ya Bunge lako hili Tukufu ili liridhie chombo hicho kipyä na kiweze kuendeleza shughuli zake kama chombo cha kudumu kama tulivyopendekeza. Utaratibu huu utawezesha Serikali kufanya kazi zake kwa tija na ufanisi katika kutekeleza majukumu haya muhimu yenye mchango wa moja kwa moja katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama angalizo kwa Serikali, Kamati yangu inashauri kuwa mapungufu makubwa yatakayojitokeza na kuwa changamoto kwa zoezi zima la ubinafsishaji linaloendelea ni uamuzi wa Serikali wa kutokurithi wafanyakazi muhimu, utaalam, uwezo hazina ya uzoefu na ujuzi pamoja na ile teknohama na benki ya takwimu/taarifa (*data bank*) vyote vilivyokwisha jengeka katika chombo cha PSRC kinachomaliza ukomo wake tarehe 31 Desemba, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na pendekezo la pili la Muswada, Kamati kwa nguvu zote inaishauri Serikali ifute pendekezo lake la kutaka yale Mashirika ambayo hayatakuwa yamebinafsishwa hadi tarehe 31/12/2007, yabinafsishwe chini ya usimamizi wa Wizara zinazohusika. Pendekezo hili la pili halikuishawishi Kamati kuwa litaleta ufanisi na tija katika mkakati mzima wa ubinafsishaji. Kamati inasisitiza ujenzi wa uadilifu, uwazi (*transparency*) na uwajibikaji (*accountability*) na kuepusha matatizo yatokanayo na urasimu ambayo yatasababisha uendeshaji na ufanisi wa usimamizi zoezi zima la ubinafsishaji kuwa na matatizo. Kamati haikupendekeza na haikubaliani na uamuzi wa Serikali kuhamishia majukumu ya ubinafsishaji wa Mashirika husika Wizarani kwa sababu za msingi zifuatazo:- Kwanza, utaratibu huu utaathiri eneo la uwazi na uwajibikaji au kwa dhahiri au kwa dhana tu. Utaratibu huu unaweza kujenga dhana nyingi zisizo sahihi baina ya Umma na Serikali yetu. Hali hii haiwezi kuleta tija kwa utendaji wa Serikali;

Pili, kwa kufanya hivyo hali hii moja kwa moja italeta mgongano wa matakwa/matarajio/maamuzi (*conflict of interest*) katika Wizara husika; na tatu, athari kubwa inayoweza kujitokeza chini ya utaratibu huu ni mmomonyoko wa misingi ya utawala bora (*erosion of good governance concept*) hata kwa dhana tu baina ya Umma na Serikali kuititia hisia za rushwa sifa ambazo hazongezi imani, tija na ufanisi kwa utendaji wa Serikali yetu, na nne, ni dhahiri kuwa kwa kufanya hivyo itachukua muda mrefu kwa Serikali, kuititia Wizara husika, kujenga mfumo na uzoefu uliopatikana na uliozoleka kama ule wa PSRC. Kamati inaona kuwa badala ya kupiga hatua mbele, tutajirudisha nyuma na tutadumaza zoezi la urekebishaji wa Mashirika yetu ya umma kama mkakati wa kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa Kamati yangu inapenda kuipongeza Serikali kwa kukubaliana na ushauri wetu huu muhimu tulioutoa, tunaipongeza sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto lililolikumba zoezi zima la ubinafsishaji pamoja na Serikali, kadri tunavyoendelea, ni lile la ufuutiliaji wa utendaji

kazi wa Mashirika yaliyokwisha kubinafsishwa – (*post privatization monitoring and follow up*). Kamati ilitoa mifano ya baadhi ya Mashirika yaliyobinafsishwa ambayo hayaonyeshi kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Kitengo hiki cha *Monitoring and Evaluation* kinatakiwa kuanzishwa ili kufanya tathmini ambayo itaruhusu hatua stahili kuchukuliwa na kupata ufumbuzi wa suala hili. Adha, ni muhimu Serikali pia ikaangalia na kuendeleza azma yake ya kuanzisha kitengo cha *Public Private Partnership Agency* ambacho kitasimamia urekebishaji wa programu na miradi ya sekta ya umma itakayoshirikisha na sekta binafsi, kwa mfano miradi mikubwa ya miundombinu ambayo mingine Serikali haiwezi kujiweka kando au ile ambayo ina ghamama kubwa kwa mfano ujenzi wa barabara (*Built Operate and Transfer - BOT*) na kadhalika. Kimsingi, azma ya Taifa ni kuona kuwa Mashirika yaliyobinafsishwa yanafuatiliwa kwa ukaribu utendaji kazi wake na ushiriki wa sekta ya umma na binafsi unaimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Dunia imekubali kutoa mkopo wa kuendeleza kazi za *PSRC* ambazo zimebakia hivi sasa baada ya tathmini ya pamoja iliyofanywa na wataalamu wa Wizara ya Mipango Uchumi na Uwezeshaji, Wizara ya Fedha na Uongozi wa *PSRC*. Kwa kuwa inashauriwa kazi hizo ziendelee chini ya chombo kipyga na muundo mpya, Kamati inaiomba Serikali na kuishauri iwasiliane na Benki ya Dunia ili iridhie kuendelea kufadhili kazi hizi zilizosalia za *PSRC* chini ya chombo kipyga cha kudumu kinachopendekezwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nisisitize kuwa yote haya yaliyoletwa na Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa niaba ya Bunge lako Tukufu, ni ushauri kwa Serikali. Wabunge kama Wawakilishi makini wa Wananchi, tunao uwezo wa kupima na kutafakari hali halisi iliyopo kwa faida na mustakabali wa nchi yetu, hivyo basi kujenga dhana ya umakini na Bunge katika kutoa ushauri baada ya ku-review hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa niaba ya Bunge lako Tukufu, inaunga mkono Muswada ulio mbele yetu na kuliomba Bunge lako nalo liunge mkono hoja hii baada ya kuzingatia ushauri huu kama tunavyowasilisha ili Serikali iendelee na shughuli zake za urekebishaji wa Mashirika yaliyobakia kwa tija na ufanisi, pamoja na majukumu mengine yaliyokuwa yatekelezwe na kuendelezwa *PSRC* inayofikia ukomo 31 Desemba, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia H. Meghji na Manaibu wake Mheshimiwa Abdisalaam I. Khatib na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Ndugu Gray Mgonja na Menejimenti ya *PSRC* ikiongozwa na Ndugu Ali Karavina, kwa kuisaidia Kamati kufanikisha kujadili na kuitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu, kwa michango yao makini ambayo kwa kiwango kikubwa imesaidia kuboresha Muswada huu. Kama ilivyo ada, naomba nitumie

fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Adam K. Malima, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmukh S. Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediane M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Hamad R. Mohammed, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar S. Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa Mzee N. Zubeir. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunamshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa taarifa yake ya Kamati. Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI NA SEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kunipa nguvu na uwezo wa kusimama hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba uniruhusu nitoe pole kwa wale wote waliofiwa na wapenzi wao na ndugu zao katika familia na katika Bunge letu hili. Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi.

Vile vile, naomba kuwapa pole wale wote waliopata ajali mbalimbali na Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nguvu na afya njema. Naomba pia nitoe pole kwa Kiongozi wangu wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, namuombea Mungu ampe nafuu na apone haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema naneno haya, kwanza naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya

NBC ya mwaka 2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Na.43(5)(c) na 70(2), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inatoa pongozi zake za dhati kwa Serikali, kwa kusikiliza kilio cha Watanzania wengi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamika kuhusu utendaji kazi usioridhisha wa *PSRC* ikiwa ni pamoja na kuwataabisha wafanyakazi walio wengi walioondolewa kazini toka mashirika na viwanda mbalimbali na wasipate mafao yao, aidha ikiwa ni pamoja na kuuza mali za Watanzania kwa bei ya karibu na bure na taratibu za ubinafsishaji zilizogubikwa na giza nene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana na madhumuni ya Muswada huu, ni mazuri kabisa kwa manufaa ya Watanzania wote. Kambi ya Upinzani, inasema haya kwa kuzingatia taarifa nzuri ya kiutendaji inayohusu Shirika Hodhi la Benki (*Consolidated Holding Corporation*) ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri aliitoa hapa Bungeni tarehe 12 April, 2007 wakati akiwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho inayohusu Shirika Hodhi la Benki. Naibu Waziri alilieleza Bunge hili utendaji wa kujivunia wa shirika letu la wazalendo linavyofanya kazi na mafanikio yake toka lianzishwe, pamoja na kuwa wanalipwa mishahara na marupuru kidogo zaidi kuliko yale ya *PSRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuweka kumbukumbu sawa, wakati Bunge hili linapitisha Azimio la Kuongeza muda wa Kufanyakazi kwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, (*PSRC*), Kambi ya Upinzani tulipinga kuongezwa kwa muda kwa Tume hiyo, pamoja na sababu tulizozitoa ni kuwa Tume hiyo ilikuwa ikifanya kazi zake kama vile watendaji wake sio Watanzania wenyе kulipwa kwa fedha za kigeni badala ya fedha za Tanzania na hivyo kuonekana kutokuwa na uchungu katika kuuza mali ambazo Watanzania walifunga mikanda katika kuzifanya ziwepo. Ieleweke hapa suala si kupinga ubinafsishaji au ukodishaji lakini utaratibu usiozingatia maslahi ya Taifa na ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili imetulazimu kulisema kwa kuangalia ukweli kuwa kwa kipindi cha miaka Tume hii ilichofanya kazi imetumia kiasi cha dola za kimarekani 26 milioni na fedha hizi ni mkopo kwa Tanzania. Kama chombo hiki ni cha Watanzania, ni chombo gani kinaratibu mishahara na marupurupu yao? Je, sisi Watanzania huo mkopo toka Benki ya Dunia tutaulipa kwa njia zippi, wakati uuzwaji na ukodishwaji wa mali zetu unafanya katika mazingira na mikataba yenye utata isiyokuwa na maslahi kwa nchi na wananchi wake? Suala hili si geni, kwani *PSRC* imekuwa ikipigwiwa kelele za mara kwa mara katika vyombo vya habari, mfano hai ukiwa huu wa karibuni wa kuuza mali yenye thamani ya soko ya zaidi ya 1.8 bilioni ambayo wao wameng'ang'ania kuiza kwa Tshs. 400 milioni tu. Ni dhahiri hapa hakuna uzalendo wowote, kama hakuna ajenda iliyofichika nyuma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limekujadhihirika pia pale Tume hiyo ilipokuwa inauza mali za Shirika la Bima la Taifa pale Tume ilipotathmini mali za Shirika la Bima la Taifa kwa bei ya kutupa kwa kulinganisha na mali zenyewe na pahali mali hizo zilipo

katika maeneo mbalimbali ya nchi hii. Waheshimiwa wote kwa hili ni mashahidi kwani ililazimu Kamati ya Fedha na Uchumi kuingilia kati kwani tathmini iliyotolewa ilikuwa ni ya kuwapa bure wageni mali za Watanzania. Bei hiyo ilikujathibitika kuongezeka mara mbili baada ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuingilia. Ni vigumu kulielewa hili, kwani Tume hiyo haina kazi nyingine isipokuwa kulinda mali ya Watanzania na bado ilionekana kushindwa kabisa kutimiza azma hiyo, mpaka Kamati ya Bunge ilipoingilia kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuna mifano mingi ya malalamiko ambapo watendaji wake na viongozi kadhaa Serikalini wamelaumiwa kujineemesha kwa kugawiwa mali ambazo zilikuwa zinamilikiwa na viwanda au mashirika mbalimbali ambayo Tume imebinafsisha, jambo linaloleta hisia kuwa viongozi hao waandamizi ndani ya *PSRC* na hata ndani ya Serikali kuhakikisha kuwa Tume hiyo inaendelea kuwepo ili waendelee kujichukulia mali za Watanzania kwa bei ya bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malalamiko mengi yanahu su mathalani mashamba ya *NAFCO* sehemu mbali mbali au mashamba ya mifugo ya Taifa (*NARCO*). Wananchi waliovu ja sho kuunda makampuni hayo kwa kodi zao wamepata nini kutokana na mashamba hayo na mashamba hayo kwa sasa yako mikononi mwa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inadhani sasa wakati umefika kabla Tume haijamaliza muda wake na shughuli zake kukabidhiwa chombo kingine, ikafanyika tathmini ya kina ya utendaji kazi wa *PSRC*, ili hali iliyojitokeza huko nyuma isije ikajitokeza tena kwa chombo kipyka kitakachopewa shughuli ya kumalizia ubinafsishaji wa mashirika yaliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kitu ambacho mpaka sasa bado hatujakielewa ni kuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRC*) ilikuwa inawajibika kwa nani? Ni kwa Serikali au Taasisi za fedha za Kimataifa? Kambi ya Upinzani inauliza swalii hili kwa kuwa fedha za kuwalipa watendaji wake zili kuwa zinatolewa na Taasisi za Fedha za Kimataifa, japo kuwa ni sehemu ya mkopo kwa Tanzania ambao hatima yake ni kulipwa na Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hizo za Kimataifa za Fedha ndizo zilizokuwa zinalazimisha kubinapisha viwanda vyetu na wale wanaouziwa wengi ni washirika wa taasisi hizo hizo. Kwa mtindo huo, je, Watanzania wakilalamika kuwa watendaji hawa walikuwa wamenunuliwa ili kuifilisi nchi yetu na kuwa wanalinda zaidi maslahi ya wageni au matajiri wachache watakuwa wamekosea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu, Kambi ya Upinzani inaona itakuwa ni busara kama kutakuwa na kifungu kuwa mbali na kuchukua kazi zilizokuwa zikifanywa na *PSRC* vile vile Shirika Hodhi la Benki (*CHC*) liwe na mamlaka ya kuendelea na kazi ya kuchukua mali na madeni ya mashirika yote ya Serikali ambayo yatabinafsishwa ili kuondoa gharama kwa Serikali za kuanzishwa kwa Mashirika Hodhi ya Reli, *TANESCO*, Bima na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Serikali ikafanya mpango haraka wa kuifanyia marekebisho makubwa sheria inayounda *CHC* hasa ikizingatiwa kuwa kazi iliyobaki ya kusimamia ubinafsishaji au ukodishaji ni ya muda mrefu na inahitaji mikakati imara zaidi. Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha atoe mpango mkakati wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu wa shughuli zilizobaki za ubinafsishaji ili Bunge hili lisiwe linafanya kazi ya zima moto kila wakati. Kukosekana kwa mipango mizuri yenye mwono wa muda mrefu pia kunaweza kuwa msingi mkubwa wa tatizo tulilonalo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *Hansard* ya tarehe 13.11.2003, Waziri Mkuu mstaafu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, alinukuliwa akisema kuwa:-

“Kazi ya kuangalia mikataba iachiwe Serikali, ni kazi ya kitaalam, wanafanya wataalam kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na wale wanaohusika na eneo linalohusika. Kama kuna tatizo, ndiyo kazi ya Bunge kuhoji Serikali”.

Majibu hayo yalitokana na hoja ya kutaka Waheshimiwa Wabunge waone *draft* za mikataba kabla ya kusainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla tuliwaamini sana wataalam hao wa Serikali. Lakini wataalam hao hao wametufikisha katika mahali ambapo nchi na wananchi wake wanashindwa kutoka kwenye hali ngumu tuliyofikishwa. Mkataba wa *IPTL*, *CITY WATER*, ubinafsishaji wa *TTCL*, *ATC* na mengine mengi ni mifano hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi wawakilishi wa wananchi tukae tuangalie wakati mali za Watanzania zinachukuliwa/zinaibiwa, eti tuwaachie wataalum, kazi yetu ni kuhoji tu? Tena wakati mali hizo zimekwisha? Ni kwa msingi huo, Kambi ya Upinzani, inaipongeza sana Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kwa kuingilia kati mkataba wa mauzo wa mali za Bima uliotaka kufanya kwa bei ya kutupwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inadhani kuwa Serikali pia hapa imejifunza kuwa Wabunge kama wawakilishi wa wananchi wana uchungu na mali na rasilimali za nchi hii kama walivyo viongozi na wataalam walioko Serikalini. Kinachotakiwa ni sehemu hizi mbili kuwa wazi moja kwa mwingine ili kuleta changamoto kwa manufaa ya maendelo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani kwa dhana hii, kamwe haitakubali daima na hivyo tunaishukuru Serikali ya sasa kwa kuliona tatizo hilo la Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma. Jambo la muhimu kwa sasa ni kuhakikisha kuwa Shirika Hodhi la *NBC (CHC)* halifanyi makosa ambayo yalifanywa na Tume kwenye kulinda mali, kwa maana nyingine uzalendo ndio utangulie katika utendaji kazi, badala ya maslahi ya wageni au ya kundi la watu au hata ya Serikali. Serikali ijione daima iko kwa ajili ya Wananchi walioiweka madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kambi ya Upinzani, inashauri kuwa kiundwe chombo au Idara ndani ya Shirika Hodhi la *CHC*. Idara hiyo iwezeshwe kwa kupewa wataalamu, ikiwezekana wasiwe waliotoka *PSRC* kwani wataleta uzoefu wao mbovu katika chombo hiki kipy. Wawezeshwe kwa kulipwa mishahara mizuri ili wasishawishike kujibinafsishia au kupokea rushwa lakini kwa vyovyote vile mishahara hiyo iwe na uwiano na mishahara katika mashirika mengine yanayofanana na hilo. Tusianguke tena kwenye mtego wa kulipa kundi la watu kwa fedha za kigeni ndani ya nchi yetu na hivyo kutengeneza matabaka yasiyo na lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa moja ya matatizo ambayo yalikuwa yakipigwa kelele na Watanzania kuhusu mashirika yaliyobinafsishwa ilikuwa ni kwa wamiliki wapya kushindwa kufanyakazi ambazo viwanda vilikuwa vikifanya na badala yake kuvifunga au viwanda kufanya shughuli nyingine kabisa, kwa mfano, kiwanda kuwa ghala ya kuwekea malighafi toka nje badala ya kuzalisha, kiwanda cha *Tanganyika Packers* sasa hivi hata haijulikani nini hatima ya kiwanda hicho. Hili lilikuwa likitokana na kukosa chombo cha kufuatilia utekelezwaji wa makubaliano baina ya Serikali na wanunuzi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuwa na Idara ya Kudumu itakayokuwa inashughulikia suala hili la ubinafsishaji na ufuatilaji wa utekelezwaji wa makubaliano yaliyomo katika mikataba. Hii ni Kutokana na ukweli kuwa hata hilo Shirika Hodhi la Benki na lenyewe liko kwa muda maalum na muda huo ukimalizika kisheria, kazi zake zinatakiwa zimalizike. Idara ya Kudumu itasaidia ili isiwe kila mara Bunge linafanya kazi ya kuwaongezea muda jambo ambalo linasababisha usumbu na kuleta hisia mbaya kwa watendaji wenyewe kuhusu matumizi ya mali ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaamini kabisa kuwa uundwaji wa chombo/idara ya kudumu ya Serikali ndio itaondoa upungufu ambao tumeeleza hapo awali na kuleta uwazi na uwajibikaji katika suala zima la ubinafsishaji na ufuatilaji wa mali ambazo tayari zimebinafsishwa na vile ambazo zitabinafsishwa kwa siku za baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ania Chaurembo, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ahsante sana!

Waheshimiwa Wabunge, kulingana na muda tulio nao kwa siku ya leo na kazi ambazo tunazo Mezani ambazo ziliwasilishwa kwenye *Order Paper*, kwa hiyo, nitaomba tu mkubaliane na mwongozo wa Kiti changu kuendesha shughuli hizi kadri nitakavyoona inafaa. Kuna wachangiaji wengi wa Muswada na kuna wachangiaji wengi wa Maazimio. Sasa, naomba niseme kwamba kwenye suala hili la Muswada, nitawaruhusu wachangiaji watatu mpaka pale saa 7.00 mchana na tutaanza na Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na atafuatia Mheshimiwa Adam Malima. Wale wengine walioleta baadaye maombi yao, nitaangalia muda unaendaje katika kikao chetu cha leo. Kwa hiyo, naomba tuanze na Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Siraju ajiandae, halafu tutaendelea na Mheshimiwa Adam Malima.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niwe wa kwanza katika kuchangia Muswada ulio mbele yetu. Nisije nikasahau kabisa, Muswada huu nauunga mkono asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi nichukue nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kabisa kusimama katika Bunge lako hili la Mkutano wa Tisa na kuzungumza hapa mbele yako, nitoe rambirambi zangu kwa familia ya marehemu, Mbunge mwenzetu wa Viti Maalum, ndugu yetu, mpendwa wetu Salome Mbatia. Naiombea familia yake na tumwombee kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapa pole kaka zangu wote wawili, Mheshimiwa Mudhihir na Mheshimiwa Waziri wetu Kapuya kwa ajali mbaya ambazo walizipata. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awape afya njema ili warudi hapa Bungeni tuweze kuendelea nao katika kuamua maamuzi ambayo tumetumwa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi niende moja kwa moja kwenye Muswada wetu. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Tume hii inayomaliza muda wake tarehe 31 Desemba, 2007. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza wazi *PSRC* wazi kwa kazi nzuri ambayo walituonyesha Watanzania kwa muda wa miaka 14, ni mashirika mengi ya umma yalikuwa yamekufa kabisa, Watanzania wengi hawakuwa na nafasi ya kufanya kazi, Watanzania wengi hawakuwa na mapato ambayo yangeweza kuwasaidia baada ya mashirika haya kukosa kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasikitika sana Mtanzania yejote yule ambaye atawabeza ndugu zetu wa *PSRC* kwa sababu wamefanya kazi nzuri na inaonekana. Kazi mojawapo, ndugu zangu, mapato yameongezeka sana. Bila hawa *PSRC*, *TRA* wasingeweza kufikia makusanyo ya kiwango hiki. Tulikuwa kwenye milioni 23 kwa mwezi sasa hivi tuna milioni 230 kwa mwezi. Ni faida mojawapo ambayo imetekelezwa na *PSRC*. Hivyo lazima tuwape pongezi zao, lazima tuwaeleze Watanzania wenzetu, hii

Tume ilikuwa inaongozwa na Watanzania ambao waliweza kusimamia mashirika haya na hatimaye *TRA* imeweza kukusanya mapato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine iliyoletwa na *PSRC* ni kusimamia kubinafsisha mashirika haya na Watanzania wengi wamepata ajira. Mashirika ambayo yalibinafsishwa na yakaanza kufanya kazi yameajiri Watanzania wengi. Hatuwezi kusema kwamba wote wangepata kazi lakini kwa mashirika ambayo yamesimamiwa na Tume hii, wengi wamepata ajira na wengi familia zao maisha yao yameboreshwa. Kwa kweli nazungumza wazi kabisa, hali zao zimekuwa nzuri. Kwa hiyo, naomba nizungumze wazi, *PRSC* wamefanya kazi yao nzuri. Pia wao si malaika, nao ni binadamu, ambayo wamekosea, tusichukulie tu upande mmoja kwamba wamefanya vibaya, wamefanya vibaya bali na mazuri tuyahesabu. Naomba basi nichukue nafasi hii kuipongeza sana *PSRC* kwa kazi nzuri na leo tunaomba tuwaage rasmi, lakini bado nitatoa huku mwishoni ushauri wangu, tusiwaache hivi hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipopata Muswada ule wa kwanza ambao haukuwa na marekebisho, ilinishtua kidogo. Mashirika haya ya Umma huko nyuma kabla ya kuunda hiki chombo yalikuwa hayafanyi kazi, leo tena Muswada ulikuja na kuleta mapendekezo kwamba turudishe kwenye Wizara husika. Iliniwia vigumu sana kuona kwamba tunarudi mwaka 47. Tulikuwa na chombo ambacho kilisimamia masuala haya na yakaenda vizuri, leo tena mashirika ambayo yamewezeshwa, bado kazi *PSRC* ilikuwa haijakamilisha, tunarudisha tena kwenye Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali na Kamati ya Fedha na Uchumi, walikaa pamoja na wakakubaliana. Pongezi hizi nazipitisha kwako, Serikali ikakubali ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi, hatimaye sasa tunapeleka kwenye chombo kingine cha *CHC* cha kusimamia masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *PSRC* tunawalaumu, taarifa iliyosomwa na wenzetu wa Upinzani kwamba Watanzania wengi walisikitika, si kweli! Tuliwapa kisheria wabinafsishé lakini hatukuweka kipengele cha kuhakikisha kwamba wanafuatialiae baada ya ubinafsishaji. Tulipowapa kazi ya kubinafsisha peke yake, tukawanyima ule utaratibu kisheria kwamba wafuatilie kiwanda hiki walichobinafsisha kinatakiwa kifanye hivi, hatukuwapa. Lakini sasa nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali baada ya kushauriana sana na Kamati ya Fedha na Uchumi kuongeza kipengele ambacho kitatumwa sasa na *CHC* kuhakikisha kwamba baada ya kubinafshisha mashirika yaliyobaki bado sasa *CHC* ifuatilie mwenendo mzima wa mashirika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshukuru sana kuona kwamba Serikali na Kamati ya Fedha na Uchumi, imekaa pamoja na kukubaliana na masahihisho yote ambayo nafikiri kila mtu amepewa ya kufuta maeneo yote ambayo majukumu yalikuwa yamepelekwa kwenye sekta, sasa yanapelekwa kwenye chombo hiki ambacho tunakizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshukuru sana kupeleka kwenye *CHC*. Lakini, nina wasi wasi. Chombo hiki kama taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi ilivyozungumza, kina majukumu makubwa. Bado na mimi nasisitiza pale pale, naishauri Serikali, Kitengo hiki cha *PSRC*, wataalamu tunao na uzoefu wanao, tusiuache utaalamu ambao tayari walipatiwa Watanzania wenzetu kwa sababu tunawafunga tarehe 31 ili waweze kusaidia tena kwenye *CHC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CHC* kama ilivyoonyeshwa kwenye taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi, wana *LRT*, kuna Simu 2000, kuna *ATC* na bado sasa tunawaongeza tena mzigo wa *PSRC*, ni kazi ngumu, lazima tuiombe Serikali kama Bunge kwamba hao wataalamu wasipotee hivi hivi tu. Pale *PSRC* kuna wataalam hata ukimwamsha saa nane za usiku, unamuuliza kiwanda cha *MOPROCO* kiko wapi, anafahamu kiko wapi, kiko Mkoa gani lakini sasa unapopeleka shughuli hizi kwenye hiki chombo cha *CHC*, itabidi wajifunze wajue *MOPROCO* iko wapi. Ndiyo maana bado ninawaomba wataalamu hao walioko *PSRC* tuwahamishie *CHC*, mimi sisemi wote, ni ninyi Serikali mtakavyoona ambao ni Watanzania wenzetu, ni wazalendo ambao wanawenza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kusisitiza na kuiomba Serikali kuunda Tume ya Kudumu. Tume ya Kudumu haitatusumbua kama Kamati ya Fedha na Uchumi ilivyozungumza, hata Upinzani wenyewe wanaunga mkono. Nitashukuru sana kwa muda ambao Kamati ya Fedha na Uchumi imetoa wa kuhakikisha kwamba hiyo Tume ya Kudumu inawasilishwe hapa Bungeni. Napenda kusema kwamba sisi Wabunge tuko tayari. Nina uhakika, Kamati ya Fedha na Uchumi tutakuwa wa kwanza kabisa kuunga mkono ili tuweze kuhakikisha kwamba chombo cha kudumu ambacho kinasimamia masuala haya Tanzania kinaanzishwa, hatuzezi tena kuwa tunakuja kuomba kila wakati. Mimi sipingani kabisa na Mfuko wa Pamoja, tena ndiyo umewekwa mahali pazuri ile *Special Fund*, Wizara ya Fedha ni muhimu sana iusimamie huo Mfuko, naunga mkono asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa na mchango mkubwa sana lakini naomba sasa niitumie nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu kwa kuteua Tume ya Kusimamia Masuala ya Madini. Wajumbe walioteuliwa ni mahiri sana, ni Watanzania. Lakini kwa kupitia Waziri Mkuu, naomba kilio akifikishe kwa Mheshimiwa Rais, ingawaje labda mimi nimepitija tu, suala la jinsia halikutiliwa maanani. Hata kwenye Tume ya Mheshimiwa Spika, jinsia ametupa mtu mmoja, si haba, lakini kwenye Tume hii ya Madini, mwanamke sijasikia. Ninavyomfahamu Rais wetu, wanawake anatujali na anatupenda na sisi tunampenda na hili akilisikia, nitaomba atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi kwa kumalizia kabisa, nilikuwa mionganoni mwa wagombea kwenye Chama cha Mapinduzi. Ninawashukuru sana Wabunge wenzangu wa CCM, kura mlinipa, lakini bahati mbaya hazikutosha. Niwaombe ndugu zangu wajumbe wa *NEC* wote, Wabunge mlolioingia mle kwenye Halmashauri Kuu, mkiona tena jina la Nyawazwa, msipate kigugumizi cha kulipitisha ili nije tena niombe kura siku yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na ninaunga mkono Muswada huu upite kwa asilimia mia moja, ahsante. (*Makofî*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Waziri wa Nchi, Taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ile aliounda Mheshimiwa Rais ya Kushughulikia masuala ya Madini, kuna wanawake katika Kamati ile. Kwa hiyo, naomba wananchi wajue kwamba Mheshimiwa Rais wetu yuko *gender sensitive!* (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru kwa taarifa hiyo. Nafikiri imepokelewa na wananchi wameisikia!

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie japo kwa uchache tu mawazo yangu kwenye Muswada huu muhimu ulio mbele yetu asubuhi hii unaohusiana na Marekebisho ya Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nikubaliane kwa kiasi kikubwa sana na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi, kuhusu mada iliyo mbele yetu. Kwa kuongezea, napenda kusositiza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Consolidated Holding Cooperation*, ilipoundwa kwa mara ya kwanza, ni wakati nchi yetu ilipokuwa imefanya uamuzi wa kuziunda upya benki zake za *NBC*, *CRDB*, *TIB* na kadhalika ambapo huko nyuma ziliwu ni Benki za Umma kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ilipotoa uamuzi wa kuzirekebisha na hususani baada ya kukaribisha wawekezaji binafsi ndani ya benki hizi, kulifanyika kitu kinaitwa *diagnostic study* ya *capital adequacy* yaani uwezo wa mtaji wa mabenki haya. Mabenki haya yalikutwa yana madeni zaidi kuliko amana kwa lugha za kitaalamu ni kwamba mabenki haya yalikuwa mufilisi. Kwa hiyo, Serikali ililazimika kuwekeza pesa zingine katika mabenki hayo ili yaweze kuwa na mtaji wa kuweza kufanya kazi. Kwa kufanya hivyo, ndipo kiliundwa chombo kinachoitwa *LART* (*Loans and Advances Recovery Trustee*). Chombo hiki ndicho kilichopewa jukumu la kukusanya madeni sugu ambayo yalifanya mabenki yetu yayumbe kimtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni haya ambayo badala yake Serikali ilitoa *long term bonds* na zikaingia katika *balance sheet* za mabenki yetu, *NBC*, *NMB*, *TIB* na kadhalika, kilichokuwa kinatakiwa kufanyika ni kwamba *LART* ilitakiwa ifuatilie madeni yale ili kila wanapokusanya yale madeni pesa zile zinakwenda Hazina na zinaiwezesha

Hazina ku-service zile *bond* ambazo zilitumika kutengeneza mitaji ya *NBC*, *CRDB*, *TIB* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, nilidhani nianzie hapo ili niweze kuonyesha kwamba kulikuwa na umuhimu wa kuunda *LART* ili ikusanye madeni sugu yaliyofanya mabenki yetu yawe mufilisi na badala yake Serikali ikatoa *bonds* ili ku-*capitalise* mabenki yale, kwa maana ya kwamba *LART* ilikuwa inakusanya zile pesa na kuiwezesha Hazina ku-service zile *bonds*. Kwa bahati mbaya, kazi hii ambayo *Consolidated Holding* walipewa, hawajaifanya vizuri. Matokeo yake ni kwamba Serikali inalazimika ku-service *bond* zilizotengeneza mitaji ya *NBC* na *CRDB* na kadhalika kwa kutumia kodi za wananchi. Leo hii tunafahamu kwamba *CHC* wamepewa kazi za iliyokuwa Shirika la Simu, wamepewa kazi za iliyokuwa *Air Tanzania*, kana kwamba haitoshi walipewa kazi ya *LART* na hawajaifanya vizuri, leo tunataka kuwapelekea kazi za *PSRC*.

Mheshimiwa Mwenyekitki, ndipo nipoanza kwa kusema kwamba hawa jamaa wa *CHC* hawana hiyo *capacity* ya kuifanya kazi hii nyeti na muhimu sana. Lakini sina maana ya kusema kwamba Serikali isitafute namna au mahali pa kupeleka au kuhamishia shughuli za *PSRC*. Kwa kuwa muda wa *PSRC* unakwisha na Serikali inalazimika kuzitafutia mahala shughuli hizi za *PSRC* kwa sababu ni endelevu, shughuli ambayo ilikuwa inafanya, kwanza ya kubinafsisha haijamalizika, pili ya kufuatilia mashirika ambayo yalibinafsishwa ndiyo kwanza inaanza. Tunahitaji chombo ambacho kitakuwa makini na chenyeye uwezo wa kufanya kazi hizi ambazo sasa *PSRC* inamaliza muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba chombo hicho siyo *CHC*. Kwa mawazo yangu, ni kwamba huko nyuma, tunaofahamu *economic history* ya nchi hii, tulikuwa na shirika linaitwa *National Development Cooperation (NDC)*. Kazi ya *National Development Cooperation* katika kujenga mashirika makubwa ya uchumi wa nchi hii tulio wengi tunaifahamu, ndiyo iliyotuundia viwanda vingi vya nguo, ngozi na viwanda vingi ambavyo siwezi kuvitaja vyote, kwa bahati mbaya au nzuri ilifika wakati viwanda vile vikaanza kutoka vikawa *independent*. *TEXCO* iliundwa ikachukua viwanda vyote vya nguo vilivyoundwa chini ya *NDC* ikaendeleza viwanda vya nguo. Viwanda vya *leather* viliondoka chini ya *NDC* vikawekwa chini ya *Tanzania Leather Association* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii *NDC* bado ipo as a shell institution. Kazi yake bado ni kubwa ya kuendeleza uchumi wa nchi hii. Masuala ya *PSRC* na yale yaliyobakia na yale yaliyokwishwafanya kwa maana ya *Private Public Partnership*, tutafika mahali hata kama tutabinafsisha mashirika yote, Serikali yetu bado itakuwa inawajibika kuona kwamba mashirika yanayoanzishwa chini ya utaratibu mpya yanafanya kazi kwa taratibu za Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti nafikiria kwa nini tusipeleke shughuli hizi *NDC* na kuipa *NDC mandate* mpya kwa sababu chombo hiki bado kipo, wataalamu wapo. *PSRC*

shughuli zake zikienda *NDC* ni kuhuisha tu na kuifanya *NDC* iendelee kuwa na shughuli zake zile ambazo huko mwanzo tulitaka ifanye kwa maendeleo ya uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo haliwezekani, nataka nikubaliane na ushauri wa Kamati ya Uchumi na Fedha kwamba hata kama tutakwenda kule kwenye *Consolidated Holding Cooperation*, twende kwa muda tu lakini kazi kubwa bado ipo mbele yetu kutazama muundo mpya wa *CHC* ambao utajibu matatizo mapya tunayoyapeleka kule kwa sababu kadri *CHC* ilivyo sasa haina *capacity* ya kufanya kazi hizi tunazozipeleka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, kadri nitakavyoeleza, nitakuwa nazunguka humo humo ambapo wenzangu wa Kamati ya Uchumi na Fedha wamesema. La msingi, nakubaliana nao na ninasema naishauri Serikali itafakari vizuri zaidi ushauri huo kwa sababu ndio utakaotupatia jawabu zuri la kitendawili kilichopo mbele yetu baada ya muda wa *PSRC* kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda wa kuchangia mada hii. Ahsante sana (*Makofi*)

**MHE. ADAM K. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii muhimu ambayo iko mbele yetu ya *PSRC* na *CHC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli, yaliyosemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, yalitokea kwenye Kamati yetu na sisi tumehusika kwa dhati kabisa kwa muda mrefu siku tatu, nne, tumekaa tunayafanya kazi. Kwa hiyo, yale yote yaliyosemwa, tunaungana nayo mkono kwa dhati kabsa na tunaomba Serikali iyachukulie kwa makini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii, kusema machache kama aliyyoyasema mwenzangu jana Mheshimiwa Simbachawene alipokuwa anazungumzia ya kwake ya ufundi na mimi niyaseme haya ambayo yapo mbele yetu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa huzuni kidogo kwa sababu kimsingi, tunafanya maamuzi leo ya haraka haraka kwa jambo ambalo ni zito sana na ambalo kama Bunge hili kwa kushirikiana na Serikali tungeyafanya maamuzi ya kina, tungeweza kupata kitu kizuri sana kikawa na manufaa zaidi kwa Watanzania ambao tunakuja kuwawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nzungumzie suala la *PSRC*. Suala hili lilikuja kwetu kwa misingi ya kwamba linaombewa kuongezewa muda. Mimi Mwenyekiti sikuona tatizo la kuongezewa muda kwa sababu ya hali ya *PSRC* iliyokuwa nayo lakini vile vile sikuona tatizo la kutokuongezewa muda kwa sababu *PSRC* ni chombo kinachokua hatutarajii ubora wa *PSRC* uliokuwepo mwaka 1994 ndio huu uliokuwepo

mwaka 2007. Ni chombo ambacho kinakwenda kinakua, kinatambaa kinaanguka na sasa kimejijengea uzoefu ule ambao tunaamini unaweza ukawa na maslahi kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa sababu suala lenyewe la *PSRC* linakuja mara kwa mara na naamini ndani ya nafsi yangu kwamba ufumbuzi uliokuwa bora zaidi unaweza ukapatikana, naomba nitamke kwamba naunga mkono hoja ya kumaliza kipindi cha *PSRC* kwa sharti kwamba Serikali inaridhia kwamba kuna umuhimu wa kina kabisa wa kukaa na wataalamu wake na kupokea ushauri huu wa kwamba huwezi kuichukua *CHC* yenye ambayo ina uwezo wa kubeba kilo 20 ikichechemea, unachukua mzigoto wa kilo 50 unawapakiza juu, unasema tembea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachofanya kama alivyosema Mwenyekiti wangu ni kwamba tunatafuta ufumbuzi wa jambo ambalo litakuwa la muda mfupi na hivyo baadaye tutakuja humu ndani tushauriane. Naiomba Serikali iangalie kwa kina kabisa ushauri huu wa kwamba tunachukua *CHC*, *PSRC*, tunawaunganisha kwa muda huu lakini kwa lengo la kuweka *super structure* ambayo itakuja na muundo mkubwa zaidi na *terms of reference* kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tatizo la ubinafsishaji ni nini? Lengo la ubinafsishaji ilikuwa kuondoa zile mali ambazo tulikuwa tunazimiliki katika sekta ya umma, kuwapa sekta ya binafsi lakini kwa ajili ya kurudisha kwa manufaa ya Watanzania hao hao. Kwa hiyo, kuna mikataba ya ubinafsishaji iliyoingiwa ambayo naamini Serikali na *PSRC* mlifanya kwa *good faith* lakini haina manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti nina maana ya kuwa kuna *element* ya *post privatization monitoring* ambayo haikuwepo na kama ilikuwepo haikusimamiwa kwa ufanisi unaotakiwa. Maana yake ni kwamba watu wamejichukulia haya mashirika wamekwendwa kule wamefanya walichofanya lakini hayana manufaa kwa Watanzania. Kwenye Kamati tuliomba na kusisitiza Serikali kwamba ubinafsishaji usiokعوا na mafanikio au maslahi kwa Watanzania walio wengi, si ubinafsishaji ambao tunatakiwa tuendelee kuui-entertain.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba *CHC* wana utaalamu wa kutosha ambao wame-*accumulate* kwenye *financial sector* na *PSRC* wana utaalamu huo walio-*accumulate* kwenye masuala ya ubinafsishaji. Ukichukua taaluma hizi mbili, ukaunga kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya fedha, *super structure* moja, zito, kubwa kisheria na kiwe ni chombo ch kudumu kwa sababu tusipofanya hivyo baada ya miaka miwili mitatu tutakuja kujadili hatima ya *CHC* ambayo inamalizika baada ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *it is high time* sasa hivi Serikali ije mbele ya Bunge na *super structure* moja na mapendekezo ya kuwa na chombo cha kudumu kwa sababu majukumu ambayo yanapewa *CHC* na majukumu ambayo yanatoka *PSRC* bado ni majukumu ya muda mrefu, si majukumu yatakayokwisha kwa miezi 18. Kwa hiyo, tukubaliane basi kwamba hii tunayofanya hapa ni *temporary solution* tukijua wazi kwamba tunalenga kufikia huko mbele ambapo tunataka siyo zoezi la ubinafsishaji tu isipokuwa ubinafsishwaji ambao utakuwa unasimamiwa na una mwelekeo wa kuwa na mchango mkubwa zaidi kwa uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati yangu, kuna mambo kama uzoefu uliojumuisha utaalamu, *data bank* na kadhalika lakini Mwenyekiti naomba nitambue hapa kwamba kuna suala lingine ambalo limezungumzwa hatujaliangalia kwa kina na lenyewe ni zito sana, hili suala la utaalamu ambao umekuwa *accumulated*. Kuna suala la *NIC* bado limebaki, ambalo lina thamani ya mabilioni ya mapesa, kuna suala la *TRC* ambalo ndiyo kwanza wameanza kuchechemea sasa hivi, tunachotaka ni kwamba jamaa zetu wa *RITES* ambao tumekubaliana nao mkataba baada ya miaka miwili ama mitatu *if they are not doing well* tuwe na mtu mwenye utaalamu wa kusema huku siko tulikotaka kwenda. Mimi kwa nafsi yangu nawajua *CHC* kwa sababu wako chini ya Kamati yangu, nawajua *PSRC* kwa sababu wako chini ya Kamati yangu, kazi hii hawaiwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Kamati inaomba kwamba hii *bulk* ya utaaluma na utaalamu ambayo iko huku iungane na *CHC* tuunde kitu kimoja ambacho majukumu yale yataendelea kutekelezwa. Kama kuna tatizo la kumaliza kikomo, mimi sina tatizo la kumaliza kikomo, ushauri wangu ni kwamba zile kazi *under whatever umbrella* ziendelee kusimamiwa kwa dhati kabisa na Serikali hii na *PSRC* ili baadaye tusije tukaulizana maswali mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *Private Partnerships Agencies*. Mheshimiwa Siraju amelizungumza kwa mapana na marefu na mimi nilikuwa naomba niligusie kidogo tu. Hii ndiyo njia ambayo wenzetu wote huko nje ukifanya *research* ndiyo wanakokwenda kwa kutambua kwamba Serikali peke yake haiwezi kuendeleza baadhi ya miradi mikubwa mikubwa ambayo ina manufaa ya moja kwa moja kwenye uchumi na wananchi wake. Kwa hiyo, kuna masuala ya kuwa na *public partnership* hizi ambazo *is the way forward* kila mtu anakwenda huko. Imani yangu ni kwamba kuna *accumulated experience* ya mambo haya ambayo yameanza kuwa *accumulated* na *PSRC*. Ninaiomba Serikali badala ya kuchukua hii na kuipeleka kwenye *function* nyingine, itambue kuwa *super structure* ambayo inapendekezwa na Kamati inaweza ikachukua hili jambo kama ni jambo ambalo linaweza likapatiwa utaratibu wake mahsus, si mambo madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulikuwa safari kule South Africa kwenye semina, kila mmoja anayekuja anakuja na suala hilo ya kwamba *that is the way forward*. Nadhani si jambo la kuangaliwa kwa wepesi ni jambo la kuangaliwa kwa mapana sana na Mwenyekiti ninaiomba Serikali kwa kujituma kabisa, izingatie ushauri wetu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ninaomba niwaambie Wabunge wenzangu na Serikali kwamba kuna mtu alisema *a good Parliament is going to force a good government* yaani Bunge linalofanya kazi vizuri kwa kujituma maana yake ni kwamba na Serikali itafanya kazi vizuri *in that same manner*. Sisi kama Wabunge tunaamini kwamba kuna mambo makini ambayo ni lazima tudai kwa Serikali na Serikali itakapojielekeza kwenye kuyajibu yale kwa kina *will become a better government*. Sisi wajibu wetu ni kuyasema haya kwa dhati kabisa. Naamini kabisa kwamba Serikali yangu imeyapokea haya na itachukua ushauri wa kitaalamu kwamba taasisi hii ikifanya kazi vizuri maeneo mengine kama ya *financial sector* ya *stock exchange*, ya *tax revenue*, yote *they form part and parcel of this*, ni *technical* siyo mambo ya kubuni. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali izingatie suala la kuleta chombo cha *super structure* haraka iwezekanavyo ili lisibaki kama ni suala ambalo mmelipokea halafu ikapita muda mrefu sana vikaingia na vitu vingine hapo katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba kwa dhati ya moyo wangu, niishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri iliyofanywa na Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango ndani ya Kamati. Haikuwa rahisi lakini tumefikia *consensus* ambayo ninaamini kama tutaifanya kazi kila mmoja kwa upande wake tutapata kitu kizuri zaidi kuliko hiyo *PSRC* na *CHC* iliyopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naomba niunge mkono hoja kwa angalizo hilo na ninaitakia kila la kheri Serikali katika kutekeleza na kukamilisha makubaliano ya Muswada huu, nashukuru. (*Makofifi*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nitazungumza kwa kifupi sana kama Mheshimiwa Laizer anaweza kuzungumza kwa dakika tano, naweza kumpa nafasi na yeye akasema kwa sababu katika Bunge hili, mimi na Laizer ni wafugaji lakini ni Wabunge wazoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kuzungumza yale ya pongezi na mengine, nataka niende moja kwa moja kwenye Muswada na ningeomba tu Katibu aweke dakika tano zinanitosha ili Mheshimiwa Laizer naye aseme dakika tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo msemo wa zamani unaosema mzigo mzito mpe Mnyamwezi hata siku moja hawajawahi kusema mzigo mzito mpe Mzaramo. Sasa leo nimeshangaa Serikali inatoa mzigo mzito inampa Mzaramo. *CHC* ninayoijua ni ile iliyokuwa inarekebisha Benki za Serikali na juzi tumeiongezea *ATCL*, Simu na *LART*,

sasa leo unatoa mzigo mzito wenyewe mashirika makubwa zaidi ya 40 unampa mtoto ambaye anadumu kwa miaka mitatu, hili jambo kwa kweli Serikali ingetafuta mbadala sisi kama Wabunge tunashauri, acheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kwamba ni kweli ninakubali *PSRC* inafikia hatima yake Desemba, kama ni matanga tayari wameshajiandaa Desemba waondoke, lakini kwa nini Serikali haitaki kukubali ushauri ambao Wabunge wanatoa? Sisi tunadhani *PSRC* kwa kazi nzuri ambayo imeifanya na sisi lazima tukubali, ‘mnyonge mnyongeni haki yake mpeni’ kazi hiyo ichukuliwe na ifanywe na chombo cha kudumu, hii ya kuongeza muda kila siku haina maana. Tunaiomba Serikali ikubali kwa sababu *PSRC* imeshafikia kiundwe chombo kipycha cha kudumu ambacho kitaundwa na sheria ya Bunge, watatuletea hesabu zao lakini pia kitakuwa cha uwazi na kuongeza uwajibikaji wakichukua uzoefu wa walionao *PSRC* na *CHC*, tukaunganisha, kitakuwa chombo kizuri ambacho kitakuwa na manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu na la mwisho, hivi kwa nini Serikali mnakuwa wabishi hivi? Tunapumzika saa saba, saa kumi na moja mkirudi muwe mmeshakaa mkubaliane moja kwa moja na maoni ya Kamati kama ilivyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Seleli kwa mchango wako mfupi kabisa wa aina yake, Mheshimiwa Laizer ameniambia na yeze anaweza akatumia dakika kama sita tu.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niongelee hoja iliyopo mbele yetu. Ninapenda kusema kwamba mnisamehe kama nikienda tofauti kwa sababu mimi sio mjumbe wa Kamati, kwa hiyo nimeanza kumsikia Naibu Waziri akiongea pale na nimemwelewa kidogo lakini nimemwelewa sana Mwenyekiti wa Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema kwamba hiki chombo cha *PSRC* ni chombo kilichofanya mengi mazuri na kama kuna mengine kwa sababu kulikuwa na mashirika mengine wanasema yameuzwa kwa kutupwa lakini napenda kwanza ifanyiwe tathmini ya hilo shirika. Napenda kusema kwamba kama muda wake umeisha, uongezewe, nakumbuka tuliongeza muda, kama ubinafsishaji bado haujafikia kikomo, waongezewe muda kuliko kuwapa tena watu wengine ambao hatuwafahamu (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba huu utaratibu wa kuhamisha *PSRC*, siuungi mkono kabisa na hata kama nitabaki mimi mwenyewe iandikwe tu kwamba mimi sikuunga mkono, kwa sababu kwanza mashirika haya yalikuwa ni mashirika ya umma yalikuwa ya Serikali, Serikali ikashindwa ndiyo ikaunda chombo cha

kutafuta namna ya kubinafsisha, ubinafsishaji haujaisha mnataka kupeleka kwingine ambapo hata wale watumishi waliopo pale sijasikia watakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni madai kama ya *East Africa Community* mpaka leo bado wanatudai, hawa wa *PSRC* nao bado watadai. Napenda kusema kwamba wamalizie kazi yao kama kuna sababu ya kuunda chombo kingine kiundwe, ila *PSRC* iwe chombo endelevu kitakachoendelea kufanya kazi zingine kama zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hawa ndiyo wachangiaji ambao waliomba kuchangia Muswada huu wa Wizara Fedha na kwa kuwa sasa tumbakiwa na dakika tano, nafikiri hazitutoshi na si muafaka kutoa nafasi kwa Serikali kuendeleza mahojiano ya Muswada huu na hatimaye kufikia hitimisho la Muswada wenywewe. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane, nisitishe Bunge mpaka saa kumi na moja jioni tutakapomalizia Muswada huu na kuendelea na agenda nyingine.

(*Saa 6.58 mchana Bunge lilifungwa  
mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

## **MCHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa ushauri. Nami napenda kuiomba Serikali ikubaliane na maoni ya Kamati. Mashirika ambayo hayajabinafsishwa yasipelekwe Wizarani. Serikali ikubali kuunda chombo cha kudumu cha ubinafsishaji. Chombo hicho kipewe wajibu wa kuwa ni cha ufuatiliaji.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu kama nilivyosema kabla sijasitisha Bunge walikuwa wameshakamilika na wote wameshachangia sasa tunaendelea na hatua inayofuata, nitamuuta sasa mtoa hoja ili aweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizoletwa mbele yetu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Naibu Spika, kwa jinsi mlivyosimamia na kuongoza Bunge wakati wa majadiliano ya hoja ya Serikali niliyoitoa leo asubuhi kuhusu mapendekezo ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara (*The National Bank of Commercial Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities (Amendment) Bill, 2007*). Aidha, nawashukuru kipekee Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge

ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuwasilisha kwa ufasaha maoni yake. Vile vile namshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwashukuru wote waliochangia kwa njia mbalimbali wakiwemo wale waliota maoni yao kwa kuzungumza hapa Bungeni na pia waliota maoni yao kwa maandishi kwa michango yao mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwataje Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni amba ni wafuatao:- Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mbunge Viti Maalum, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Adamu Kigoma Malima, Mbunge wa Mkuranga, Mheshimiwa Lucas Selelili, Mbunge wa Nzega na Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mbunge mmoja tu ambaye alichangia kwa maandishi naye ni Mheshimiwa Lucas Selelili, Mbunge wa Nzega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe maelezo kuhusu hoja mbalimbali zilizotolewa. Hoja ya kwanza ilikuwa hoja ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Walipendekeza kwamba Serikali iunde chombo cha kudumu ili kusimamia ubinafsishaji. Napenda kukuhakikishia kwamba Serikali imeupokea ushauri huo na itaufanyia kazi. Kuunda chombo kipyä ni machakato, Serikali itaangalia mapendekezo yote yaliyotolewa na tutayafanyia kazi ili chochote kitakachoamuliwa kiwe ni kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipendekeza pia kwamba wataalam walioko *PSRC* wahamishiwe *CHC*. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu, utaalam uliojengeka *PSRC* na baadhi ya watalaam walioko *PSRC* watachukuliwa ili kuimarisha *CHC*. Suala la uwezo wa *CHC*, *CHC* imeweza kutekeleza vizuri majukumu yake iliyopewa na kwa ufanisi mkubwa, hivyo Serikali imeridhika na utendaji wake na ndiyo maana imependekeza kwamba kazi za *PSRC* zihamishiwe *CHC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ufuutiliaji wa mashirika yaliyobinafsishwa yaani *Post Privatization Mortaring and Evaluation*, Serikali inatambua umuhimu wa suala hili. Hivyo ushauri wa Kamati umezingatiwa na Serikali katika Muswada huu ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa jukumu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hoja za Kambi ya Upinzani, ninamshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa kuiunga mkono hoja hii. Hata hivyo, hakuna asiyefahamu mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana ubinafsishaji kupitia *PSRC*. Lakini lazima tukubali kuwa kwa vile uhai wa *PSRC* unaisha tarehe 31/12/2007, hatuna budi kuhamishia shughuli zake kwenye shirika lingine kuanzia tarehe 1/1/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia Muswada huu. Wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Viti Maalum. Tunapokea pongezi za Mheshimiwa Nyawazwa kuhusu kazi nzuri iliyofanywa na *PSRC* katika muda wa uhai wake wa Miaka 14. Pia Serikali itazingatia ushauri wa kuunda chombo cha kudumu cha kushughulikia masuala ya ubinashaji na ufuutiliaji wa mwenendo na utendaji wa mashirika hayo.

Kuhusu namna bora ya kutumia utaalam na uzoefu uliojengeka *PSRC*, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kama nilivyosema awali itazingatia suala hilo kama nilivyoeleza katika hotuba yangu wakati wa kuwasilisha Muswada huu. Wafanyakazi wengi amba ni wataalam walioko *PSRC* kwa sasa watahamishiwa *CHC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa pili, alikuwa Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini. Mheshimiwa Kaboyonga alihaja uwezo wa *CHC* na kushauri kuwa ingefaa majukumu ya *PSRC* yangepelekwa *NDC*. Madai haya siyo ya kweli. Mwaka 1997, *CHC* ilitakiwa kuuza nyumba 443, imeuza nyumba 440 na zimebaki nyumba tatu tu. Haya ni mafanikio. Madeni yaliyokabidhiwa *CHC* mwaka 1997 yalikuwa 5282 na yamebaki 1800 nayo pia ni mafanikio. Kesi zilikuwa 1000, mpaka sasa hivi zimebakia 168 hatuwezi kusema kwamba *CHC* haikufanyakazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunda chombo cha kudumu kama ilivyopendekezwa, Serikali itaangalia njia mbalimbali pamoja na hii iliyopendekezwa na Mheshimiwa Kaboyonga. Aidha, kama nilivyoikuwa najibu hoja ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, *CHC* imeonyesha uwezo mkubwa wa kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa na Serikali kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *bonds* ambalo Mheshimiwa Mbunge alilizungumzia, Serikali kweli ilitoa *bonds* kwa ajili ya mikopo ya mashirika ambayo Serikali ilikuwa imeyadhamini kama Vyama vya Ushirika, *Rungwe Tours, Tanganyika Parkers* na kadhalika. *Bond* hizi zilitolewa kwa mabenki ambayo yalikuwa yameyakopesha mashirika hayo. Benki hizi ni *CRDB, National Bank of Commerce* na *Peoples Bank of Zanzibar*. Madeni hayo baada ya kutolewa hizo *bonds* kwa mabenki husika, yalihamishwa *LART* kwa ajili ya kuyakusanya. Utaratibu huu ulifanyika kabla ya kuundwa kwa *CHC*. Itakumbukwa kuwa mapema mwaka huu Bunge lako Tukufu, lilidhiria kuwa kazi za *LART* zihamishiwa *CHC* baada ya *LART* kumaliza muda wake. Hivyo, kazi zote za *LART* zilihamishiwa *CHC* kuanzia tarehe 1/7/2007. Kwa hiyo, *CHC* imefanya kazi ya *LART* kwa miezi mitatu tu. Kwa hiyo, madhambi au matatizo ambayo ilikuwa nayo *LART* si sahihi kuyashuku kama ni matatizo ya *CHC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa tatu, alikuwa Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, Mbunge wa Mkuranga, tumepokea ushauri wake kuhusu masuala ya ufuutiliaji wa mashirika yaliyobinafsishwa, uundwaji wa chombo cha kudumu, wataalam wa *PSRC* kuhamia *CHC* na ushauri wa kuangalia uwezekano wa kuanzisha chombo kitakachoshughulikia utaratibu wa uanzishwaji na utekelezaji wa miradi mikubwa kati ya

sekta binafsi na Serikali, *Public Private Partnership Agencies, PPPA*. Ushauri huo tumeupokea na Serikali itaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa nne, alikuwa Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega. Ninamshukuru kwa mchango wake wa maandishi na kwa kuzungumza. Aidha, hoja ya kutopeleka mashirika yanayobinafsishwa Wizarani, imezingatia katika Muswada, kazi zote zinazofanywa na *PSRC* zitahamishiwa *CHC*. Kazi zilizokuwa zinafanywa na *Planning Commission* na baadaye Wizara ya Mipango zitahamishiwa kwenvye Wizara mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa tano, alikuwa Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido. Ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa mchango wake. Aidha, alishauri *PSRC* ipewe muda zaidi. *PSRC* kwa mujibu wa sheria inamaliza muda wake tarehe 31 Desemba, 2007. Kama tulivyosema Bunge hili tulishatoa Azimio mwaka 2003 kwamba tusirefushe tena muda. Kwa hiyo, Serikali imeona kwamba kazi zilizobaki zinaweza zikafanywa na *CHC* kama tulivyopendekeza katika Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

### KAMATI YA BUNGE ZIMA

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Kamati ya Bunge Zima ili tuweze kuupitisha Muswada huu kifungu kwa kifungu. Katibu tuongoze.

Ibara ya 1

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na  
Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote*)

Ibara ya 2

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na  
Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 3

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote*)

Ibara ya 4

**MHE. JUMA S. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha nne ambacho chini yake kuna kifungu cha 6(a) sijui kama tuko pamoja?

**MWENYEKITI:** Tuko pamoja Mheshimiwa.

**MHE. JUMA S. KABOYONGA:** Sawa sawa. Sasa hapa kwenye 6(a) yale madhumni au *functions* ambazo zitafanywa na hili shirika sioni lile la kubinafsisha mashirika ambayo bado hayajabinafsishwa, halijitokezi moja kwa moja.

Halafu lingine ni la kufanya *follow up* na *evaluation* ya mashirika yaliyobinafsishwa. Inawezekana kabisa yakawa yamekuwa *captured* na (*d*) *doing any other act as the Minister may direct* lakini hizi ni *substantial functions*, kwa nini zisijitokeze dhahiri kwa maana ndiyo *functions* za PSRC ambazo tunazihamishia CHC? Naomba ufanuzi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimueleweshe Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna *Schedule of Amendment* ambayo imesambazwa. Ukiangalia *Schedule of Amendment* hiyo, hiyo *clause* imefanyiwa mabadiliko. Tumeongeza sehemu mbili (a) na (b), ambayo ya kwanza inasema, *determine the means by which the restructured specified public corporation is to be diversified*. Halafu la pili, *is to conduct post privatization monitoring and evaluation*. Kwa hiyo, hayo yote aliyoyaeleza yameshazingatiwa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nafikiri tukiangalia ile *Schedule of Amendment, page 1*, Mheshimiwa Kaboyonga, inajionyesha vizuri pale. Kwa hiyo, ukifuatilia vizuri utaona kwenye ile *page 1, clause 4(a)* na (b), zote zimejieleza vizuri.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 5

Ibara ya 6

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote*)

Ibara ya 7

Ibara ya 8

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima, imepitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa (*The National Bank of Commercial Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities (Amendment) Bill, 2007*, kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja ili amuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa  
Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu umeshapitia hatua zote zinazotakiwa ndani ya Bunge na baada ya Bunge kumaliza kazi yake, sasa naomba kuwatangazia kwamba Muswada huu wa Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara wa mwaka 2007 (*The National Bank of Commercial Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities (Amendment) Bill, 2007*, umeshapitishwa na Bunge hili na utasubiri sasa hatua za mwisho ambazo mara nyingi zinamhusu Mheshimiwa Rais mwenyewe. Kwa hiyo, baada ya kazi hiyo tunaendelea na kazi nyingine ambayo iko mbele yetu.

## MAAZIMIO

**Azimio la Bunge Kuridhia Waziri wa Fedha Kufuta  
na Kusamehe Madeni, Madai na Hasara Zitokanazo na Upotevu  
wa Fedha, Vifaa vyta Serikali, Malipo Batili, Madai ya Kodi  
pamoja na Maduhuli Yasiyokusanyika kwa Kipindi Kinachoishia  
Tarehe 30 Juni, 2006.**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Azimio la Bunge Kuridhia Wizara ya Fedha Kufuta, Kusamehe Madeni, Madai au Hasara ambazo hazilipiki zitokanazo na upotevu wa fedha, vifaa vyta Serikali kwa kipindi kilichoishia 2006 kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura namba 348 (*The Public Finance Act, Chapter 348*). Aidha Azimio hili lilijadiliwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaani PAC katika kikao chake cha tarehe 8 Novemba, 2007 kilichofanyika Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John M.

Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki (*UDP*) na Makamu wake Mheshimiwa Estherina Kilasi Mbunge wa Mbarali CCM, pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo, kwa maoni yao mazuri yenye lengo la kuboresha udhibiti na uimarisaji wa usimamizi wa fedha na mali za Serikali kwa lengo la kupunguza au kuepuka upotevu wa mali na vifaa vyta Serikali. Serikali kwa kiasi kikubwa imezingatia ushauri wao katika kuboresha Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali ianze utaratibu wa kutoa taarifa za upotevu Bungeni, kumekuwa na mafanikio yafuatayo katika utendaji kazi Serikalini. Moja, kupungua kwa hasara zilizowasilishwa na Maafisa Wahasifu kutoka shilingi bilioni 72,850,017,122.3 katika mwaka ulioishia tarehe 30/6/2002 hadi kufikia shilingi bilioni 9,803,637,777.63 katika mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2006 kama ilivyoonyeshwa katika kabrasha ambalo Waheshimiwa Wabunge, mmepewa.

Pili, kuongezeka kwa uelewa kwa Maafisa wa Wahasibu, kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa za potevu na hasara kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali mara tu zinapogundulika kwa mujibu wa kanuni za fedha na maelekezo ambayo wamekuwa wanapewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ya kuziwasilisha Hazina taarifa na potevu mara baada ya hesabu za mafungu yao kujadiliwa na Kamati.

Tatu, kupungua kwa mlundikano wa hoja za ukaguzi sugu ambazo ziliwuwa zinajirudia mwaka hadi mwaka kutohakana kutofanyika kwa marekebisho katika vitabu vyta Serikali. Aidha, taswira ya Serikali imeanza kupendeza siyo tu kwa wananchi bali hata kwa wadau wa maendeleo.

Nne, vitabu vyta hesabu vimeendelea kuwa safi kwa sababu hoja nyingi za hasara zimefutwa au ziko katika hatua za kufutwa.

Tano, utaratibu huu umeonjeza uwajibikaji na uwazi zaidi wa jinsi Serikali inavyoshughulikia upotevu wa mali zake. Pia utaratibu huu unawafanya Maafisa Wahasibu kuwa makini zaidi katika usimamizi wa mali za umma yaani fedha na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasara, potevu za fedha na vifaa vyta Serikali. Ifuatayo ni taarifa ya upotevu ambayo imegawanyika katika sehemu mbili kwa mwaka unaoishia tarehe 30/6/2006, inaombewa kibali cha kufutwa na Bunge lako. Mgawanyo wa potevu hasara hizo ni kama ifuatavyo:-

Moja, fedha, vifaa na malipo batili:-

- (a) Fedha tasilimu (*cash*) shilingi 569,500,064.53;
- (b) Vifaa yaani *stores* shilingi milioni 336,280,771; na
- (c) Malipo batili (*nugatory expenditure*)shilingi bilioni 9,897,060 jumla yote ni shilingi 915,182,895.53

Pili, mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanya shilingi bilioni 8,888,454,882.40 jumla yote ni shilingi bilioni 9,803,637,777.93.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoe maelezo kwa kila aina ya potevu au hasara hizo. Moja, hasara zinazohusu potevu za fedha, vifaa na malipo batili ya shilingi milioni 915,182,895.53. Kiasi cha shilingi milioni 915,182,895.53 ni hasara zinatokana na upotevu wa fedha taslimu, upotevu au uharibifu wa vifaa na malipo batili na ndizo zinazowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, ili kuombewa kibali zifutwe. Hasara zinazohusika hapa zinajumuisha chache zilizotokea katika miaka ya 80 na 90 lakini nyingi zikiwa ni za kati ya miaka ya kuanzia Julai, 2000 na Juni 2005 na nyingine ni za kipindi kinachoishia Juni, 2006. Kiasi kikubwa cha hasara hizi kimetokana na sababu mbalimbali zikiwemo:-

(a) Wizi kwa njia ya watumishi kudokoa maduhuli badala ya kuyapeleka benki, wizi wa majambazi kuvunja na kupora mishahara ya watumishi wa Serikali kama vile Walimu au kuvunja *store* na kuiba vifaa, udokozi wa fedha ambazo ni kielelezo cha Mahakamani, ajali ya moto kuunguza vifaa na kadhalika. Kwa upande wa wizi wa mishahar,a tatizo limepungua kwa kiasi kikubwa kufuatia uamuvi wa Serikali wa kupitishia benki mishahara ya watumishi wake.

(b) Ubadhilifu wa watumishi kula njama katika kuhujumu fedha za umma mfano halisi ni wizi uliotokea katika Ofisi ya Waziri Mkuu wa shilingi milioni 326,736,856 katika mwaka 2000/2001 uliofanywa na watumishi 8 kwa njia ya kushirikiana. Hivi sasa kesi hiyo ilikwishatolewa hukumu tarehe 13/11/2006 na watumishi 7 waliachiwa huru na Mahakama na mmoja ndiye ambaye alitiwa hatiani na kuhukumiwa kifungu cha miaka 10. Hukumu haikumtaka mhukumiwa alipe kiasi hicho cha fedha akitoka hivyo kuwa hasara kwa Serikali.

(c) Vifaa kupitwa na wakati au kwisha kwa muda wa kutumika na hivyo kutofaa kwa matumizi.

(d) Uzembe (*negligence*) kama vile vifaa kuachwa bila kuangaliwa na mwisho wake kuharibika hasa katika bohari za Serikali.

(e) Kufanya malipo bila ya Serikali kupata faida ya huduma ya vifaa au bidhaa.

(2) Mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanya ya shilingi 8,888,454,882.40. Aina ya hasara hii inatokana na Serikali kushindwa kukusanya mapato na; au maduhuli iliyokusudia kukusanya kutokana na sababu mbalimbali kama vile:-

(a) Kupatikana kwa mapato kutokana na kutopatikana kwa mapato kutokana na makampuni au mashirika ya umma kubinafsishwa badala ya kulipa mapato ya Serikali yanayodaiwa kabla ya kulipa mapato ya Serikali yanayodaiwa kutoka kwenye makampuni au mashirika hayo. Mifano ya makampuni hayo ni Kampuni ya *Kiwira Coal Mines* inayodaiwa na Serikali deni la shilingi 556,963,118. Ranchi za Taifa zinadaiwa

shilingi 3,790,056,725. Mashamba ya *DAFCO* shilingi 171,351,250 na hoteli ya Saba Saba ina deni la shilingi 436,068,865 na kufanya jumla ya shilingi zinazodaiwa kufikia shilingi 4,954,436,988.

(b) Gharama za ukusanyaji kuwa kubwa kuliko kiasi kinachotarajiwa baada ya kukusanywa.

(c) Maamuzi mbalimbali ya Mahakama dhidi ya Serikali au dhidi ya wadau wanaodaiwa na Serikali.

(d) Madeni ambayo Serikali ilikuwa inayadai mashirika ambayo sasa yamefilisika kwa mfano kodi au gawio au faida (*dividend*).

(e) Baadhi ya wadaiwa kutojulikana waliko baada ya kuhamisha au kufunga shughuli zao kutokana na kukosa kuendelea kupata ufadhili kama vile vyama vya hiari, *clubs association* na kadhalika. Au Asasi Zisizokuwa za Kiserikali (*NGOs*) zilizosajiliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kiasi hicho cha hasara kuna maeneo ambayo yamechangia kuongezeka kwake. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2000/2001 hadi 2004/2005, Mamlaka ya Mapato Tanzania inalidai Shirika la Posta kodi ya mapato ya jumla ya shilingi 1,914,333,646. Shirika hili limeshindwa kulipa kiasi hicho cha kodi kwa sababu liko katika harakati za kufanyiwa marekebisho kimfumo na kimuundo (*reforms and restructuring*) na hivyo kuhamishia Serikalini madeni yote yasiyolipika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwengine ni katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambako Serikali ilikuwa inadai vyama vya hiari (*clubs, association*) na kadhalika au Asasi Zisizokuwa za Serikali zilizosajiliwa na Wizara hiyo jumla ya shilingi 153,965. Serikali imefuatilia madai hayo lakini ufuatilaji huo haukuleta mafanikio yoyote kwa sababu ya kushindwa kujua asasi na vyama hivyo vilipo. Kwani asasi nyingine zimebadilishana majina na anwani zao. Baadhi ya asasi zimehama nchini na nyingine zimefilisika kutokana na kukosa ufadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwengine ni pale kulipofanyika makosa ambayo yalipelekea Serikali kushindwa kukusanya maduhuli kwa kutokata kodi ya mapato yaani *payee* ya jumla ya shilingi 121,388,140 kwa Waheshimiwa Wabunge katika kipindi cha mwezi wa Novemba na Desemba, 2005 kwa Wabunge waliomaliza muda wao. Imeonekana itakuwa vyema kuomba kibali cha kufuta kodi hiyo kwa sababu Serikali haitaweza kukusanya pesa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwengine unaofanana ulioelezwa hapo juu ni ule ambao wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wanaombewa kufutiwa deni

linalofikia jumla ya shilingi 1,503,213,159 ikiwa ni bakaa ya mikopo ya magari waliokopeshwa katika kipindi kinachoishia 1996/1997.

Makato ya mikopo hiyo yalisimamishwa tarehe 28 Februari, 2006 baada ya malalamiko ya wanajeshi hao kukubaliwa. Sababu ya kusitishwa kwa makato hayo ni kutokana na thamani ya magari hayo kuwa zaidi kuliko ilivyokuwa imetarajiwa na wapiganaji. Ongezeko hili lilitokana na *exchange rate* iliyotumika katika kubadilisha thamani ya magari kutoka dola kuwa shilingi za Kitanzania kuwa kubwa kuliko ilivyokuwa imetarajiwa nawapiganaji.

Aidha, baada ya kuchambua zaidi ilionekana kwamba wengi wa wadaiwa hao walikuwa wamestaafu jeshini bila kukatwa bakaa ya mikopo katika mafao yao kwa vile makato yalikuwa yamesimamishwa wakati wanastaafu. Kwa vile ni vigumu kuwafuatilia wastaaafu hao kwa lengo la kuwataka walipe bakaa za mikopo, kwa kuwa ni kweli *exchange rate* iliyokuwa imetumika ilikuwa kubwa kuliko ilivyotarajiwa. Imeonekana ni busara kupendekeza kuwafutia bakaa ya mikopo wadaiwa wote ili kuleta usawa na haki badala ya kuendelea kuwakata wale wanaoendelea na ajira ya jeshi na kuwaacha wale waliostaaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kati ya mashirika niliyoyataja hapo awali kuna ambayo Serikali ilikopa fedha au kupata fedha kutoka nje ya nchi ili kuyapatia mitaji au fedha za kuendeshea shughuli zao kwa makubaliano kwamba mashirika hayo yatailipa Serikali. Kufilisika au kubinafsishwa au kuvunjwa kwa mashirika hayo kunasababisha deni kutolipwa na hivyo ni sehemu ya hasara inayoombewa kufutwa.

Mfano wa asasi ya aina hiyo ni kampuni ya *Kiwira Coal Mines* ambayo ilibinafsishwa mwanzoni mwa mwezi wa Juni, 2005 ikiwa na mzigo wa madeni Serikalini ya kiasi cha shilingi 556,963,118 ambayo ni pamoja na leseni za madini, mirabaha (*mines royalties*) na kodi mbalimbali za Serikali.

Maafisa Wahasibu kuwajibika kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2004. Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 inaeleza wazi jinsi ya kushughulikia potevu au hasara za Serikali. Sheria hii inawawajibisha Maafisa Wahasibu katika kuhasibu hasara na potevu hizo kwa vile wao ndiyo wasimamizi wakuu wa mapato na matumizi wa fedha za Serikali. Kwa mujibu wa Kanuni za tozo na adhabu (*penalties and surcharges regulations 2005*), Serikali kuitia Kamati ya *PAC* imepewa uwezo wa kuwawajibisha Maafisa Wahasibu wanaokiuka Sheria ya Fedha na kusababisha hasara.

Aidha, Kanuni hizi zinaainisha aina ya adhabu zinazopaswa kutolewa pale Sheria na Kanuni za Fedha zinapokiukwa. Ni mategemeo yetu kuwa hasara zitaendelea kupungua zaidi kama dalili zilivyojionyesha zinavyoashiria. Serikali itaendelea na juhudzi za kuzuia hasara, potevu zisitokee kwa kuhakikisha kila Afisa Masuhuli anazingatia Sheria ya Fedha na Sheria ya Manunuzi pamoja na kanuni zake wakati wa kukusanya na; au kutumia fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa zao za potevu wanazowasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, Maafisa Wahasibu wanapaswa kuelezea jinsi hasara hizo zilivyojitokeza na juhudzi zilizofanywa katika kupunguza au kuepuka hasara hizo.

Aidha, kila Afisa Mhasibu anapaswa kuelezea hatua zilizochukuliwa dhidi ya mtumishi yeoyote aliyesababisha hasara hizo. Mhasibu Mkuu wa Serikali baada ya kupokea taarifa hizo anatayarisha Jedwali linaloonyesha potevu zote zilizoletwa na Maafisa Wahasibu kama kabrasha walilopewa Waheshimiwa Wabunge linavyoonyesha, na ni taarifa hiyo ya potevu ambayo sasa inawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuombewa kibali cha kufutwa.

Mapendekezo ya kufuta hasara na kusamehe madai ambayo hayalipiki. Serikali inapendekeza kufuta hasara na kusamehe madai ambayo hayalipiki ya kiasi cha shilingi 9,803,637,777.63 kama ilivyoainishwa katika kabrasha walilopewa Waheshimiwa Wabunge ambalo limeambatishwa pamoja na Azimio hili ili kuonyesha hali halisi. Kufutwa kwa hasara hizi kunasaidia kupungua kwa kiasi kikubwa hoja za ukaguzi na kutoa picha iliyo sahihi ya vitabu vya hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kufuta na Kusamehe madai na hasara itokanayo na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2006 kama ifuatavyo:-

KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Usimamizi na Udhhibit wa Fedha za Umma Sura Na. 348, Waziri wa Fedha amepewa mamlaka ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kugawa na kuidhinisha matumizi ya fedha hizo baada ya kupata idhini ya Bunge;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Usimamizi na Udhhibit wa Fedha za Umma, Sura Na. 348, Bunge linaweza kuazimia kutoa idhini kwa Waziri wa Fedha kufuta hasara na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali, madai ya kodi pamoja na riba itokanayo na malimbikizo ya kodi;

NA KWA KUWA vitabu vya Hesabu za Serikali vionyeshE kuwepo na upotevu wa fedha za Serikali pamoja maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa;

NA KWA KUWA kutokana na upotevu na upungufu huo wa fedha vifaa na maduhuli ya Serikali upo umuhimu wa kusawazisha kumbukumbu katika vitabu hivyo vya Serikali;

KWA HIYO BASI, kwa mujibu wa kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma, Sura Na. 348, sasa Bunge hili katika Mkutano wake wa Tisa, Linaazimia kumuidhinisha Waziri wa Fedha asamehe na kufuta upotevu wa fedha, vifaa na malipo batili, maduhuli yaliyoshindikana kukusanya na kwa ajili hiyo kusawazisha kumbukumbu katika vitabu vyta Serikali kama ifuatavyo:-

- (a) Upotevu wa fedha, vifaa na malipo batili ya shilingi 915,182,895.53.
- (b) Mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanya ya shilingi 8,888,454,882.40. Jumla kuu ni shilingi 9,803,637,777.63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusu upotevu huu yapo kwenye kabrasha ambalo naamini Waheshimiwa Wabunge wamepata nakala yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, naomba kuwasilisha Azimio la kumwezesha Waziri wa Fedha kufuta hasara itokanayo na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia Juni 30, 2006. Kwa mujibu wa Kanuni ya 88(11) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa ya Kudumu ya Hesabu za Serikali inayohusu upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati naomba kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Salome Mbatia, aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, aliyesariki dunia kwa ajali ya gari tarehe 24 Oktoba, 2007 huko Wilayani Njombe, Mkoani Iringa. Taarifa ya msiba huo ilipokelewa kwa masikitiko makubwa sana. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina. Aidha, Kamati inawapa pole Waheshimiwa Wabunge wote waliopata majanga mbalimbali bila kuwasahau Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Juma Kapuya na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir kufuatia ajali walizopata katika vipindi tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 94(1) ya mwaka 2003, Kamati hii iliundwa na Wajumbe 13 wafuatao:-Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Zubeir A. Maulid, Mheshimiwa Fatma A. Fereji, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami,

Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu na Mheshimiwa Felister A. Bura ninayesoma Taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa shukrani zangu kwa Wanakamati wenzangu kwa kazi nzuri walioifanya ya uchambuzi wa kina wa taarifa ya upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2006. Ni imani ya Kamati kwamba mapendekezo waliyoyatoa yatazingatiwa na Serikali ili kupunguza upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 8 Novemba, 2007 Kamati ilipata maelezo ya jumla kutoka kwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji juu ya ombi la Serikali la kufuta hasara iliyotokana na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2006 yenye thamani ya shilingi 9,803,637,777.93.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliridhirika kuwa kiasi cha 9,803,637,777.93 kinachohusu upotevu wa fedha na vifaa kifutwe hasa ukizingatia kuwa Serikali haiwezi kupata tena fedha na vifaa hivyo kutokana na sababu mbalimbali kama vile upotevu wa fedha taslimu, upotevu wa vifaa, majanga ya moto na malipo batili kama ifuatavyo:- Jumla ya shilingi 659,005,064.54 zilipotea kama fedha taslimu ambapo jumla ya shilingi 336,280,771 ni upotevu wa vifaa na jumla ya shilingi 9,897,060 zilikuwa ni malipo batili yaliyofanywa na Serikali katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2006. Kwa upande wa maduhuli ya jumla ya shilingi 8,888,454,882.40, hazikukusanywa kutokana na sababu mbalimbali kama vile gharama za ukusanyaji wa mapato na maduhuli hayo kuwa makubwa kuliko kiasi kilichotarajiwa kupatikana baada ya kukusanywa. Maamuzi mbalimbali ya Mahakama dhidi ya Serikali au dhidi ya wadau wanaodaiwa na Serikali. Madeni ambayo Serikali inayadai mashirika yaliyofilisika kutopatikana kwa mapato kutokana na makampuni ya umma kubinafsishwa kabla ya kulipa mapato ya Serikali. Mifano ya makampuni hayo ni Kampuni ya *Kiwira Coal Mines* inayodaiwa na Serikali jumla ya shilingi 556,963,118 na Hoteli ya *Seventy Seven* inayodaiwa shilingi 436,068,895. Ranchi za Taifa zinazodaiwa shilingi 3,790,056,725. Mashamba ya *DAFCO* yanadaiwa shilingi 177,351,250 na malipo ya *Pay As You Earn* ya shilingi 121,388,140 yaliyoshindikana kukusanywa kutokana na Waheshimiwa Wabunge kutokuwepo kwenye *Pay Roll* baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 kuahirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mambo yaliyoainishwa hapo juu Kamati inaishauri Serikali itilie mkazo mambo yafuatayo ili kupunguza kiwango cha hasara inayotokana na upotevu wa fedha na mali za Serikali.

Moja, Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka nidhamu ya hali ya juu katika usimamizi wa mali za umma. Kamati imebaini bado kuna tatizo la upotevu wa fedha za Serikali kwa kisingizio cha upotevu wa nyaraka na sababu nyingi ambazo zinaweza kuzuilika. Pili, kuajiri wataalamu wa kutosha wa ugavi na uhasibu kwenye Idara zote za Serikali. Kamati imeliona tatizo la kutokuwepo kwa wataalamu wenye ujuzi unaotakiwa katika fani hizi.

Tatu, Kamati inashauri Serikali iwe na mfumo wa bima ambao utasaidia katika kupunguza au kuondoa kabisa hasara inayotokana na upotevu wa mali za Serikali. Kamati pia inashauri Serikali kuhimiza Maafisa Wahasibu kufuatilia kesi zote za upotevu wa mali za Serikali zilizopo Mahakamani, kwani imebaini uwepo wa kesi nyingi za upotevu wa fedha za Serikali na mali za Serikali. Naomba kurudia hapo. Kamati inaishauri Serikali kuhimiza Maafisa Wahasibu kufuatilia kesi zote za upotevu wa mali za Serikali zilizopo Mahakamani kwani imebaini kuwepo kwa kesi nyingi za upotevu wa fedha na mali za Serikali ziko Mahakamani kwa kipindi kirefu kutokana na Maafisa Wahasibu kutofuatilia kwa karibu miendo ya kesi hizo.

Kamati inaishauri Serikali kuwa na mpango madhubuti wa kuzuia na kupambana na majanga yanayotokana na moto. Hatua zinazopendekezwa ni kama vile kuimarisha kwa Kikosi cha Zimamoto na nyumba za Serikali ziwe na vifaa na mifumo ya kuzimia moto. Kamati inaishauri Serikali kuleta Bungeni taarifa ya upatikanaji wa fedha na vifaa vya Serikali au hatua iliyochukua kufuatilia madai ya hasara hizo zilizofutwa na Bunge kwa kipindi cha miaka ya nyuma. Kazi hii ya Kamati ya kupitia Taarifa ya upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2006 isingekamilika kama wafuatao hawakuchangia kwa namna moja au nyingine. Kwa namna ya pekee ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Kamati ya PAC, Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S.L. Foka, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji na Naibu wake, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo ambaye alishirikiana na Kamati yetu wakati wa kuchambua Taarifa hii.

Pia napenda kutoa shukrani zangu kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali na Makatibu wa Kamati za Hesabu za Serikali, Ndugu James Warbug na Ndugu Brown Gideon Mwangoka ambao wamewezesha kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiiti, baada ya Kamati yetu kuchambua Taarifa ya Serikali ya Upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2006 imeridhika kuwa kiasi cha shilingi 9,804,307,777.93 kifutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Azimio la kufuta jumla ya shilingi bilioni 9,804,307,777.93 zikiwa ni upotevu wa fedha, vifaa na malipo batili pamoja na mapato na maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa katika kipindi kinahoishia tarehe 30 Juni, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unawasilisha, hutoi hoja katika ajenda hii. Waheshimiwa Wabunge baada ya Mheshimiwa Felister A. Bura kwa niaba ya

Mwenyekiti wa Kamati kuwasilisha hoja yake sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani ili naye aje kutoa maoni ya Kambi. (*Makof*)

**MHE. CHACHA Z. WANGWE (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMADI WA UPINZANI WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni ya 45(5)(c), Toleo la 2004. Wananchi wanafuatilia Azimio la Bunge la Kuridhia Kufutwa Upotevu wa Fedha na Vifaa vyta Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2006 jumla ya shilingi za Kitanzania 9,804,307,777.93. Kwanza naomba kulipongeza Bunge lako kwa utaratibu ambao liliweka kwa Serikali kutoa taarifa juu ya upotevu wa fedha na vifaa katika Taasisi mbalimbali za Serikali ikiwa ni sehemu ya kutekeleza majukumu yetu ya Kikatiba ya kusimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Hazina inaonyesha kwamba kati ya upotevu huo, upotevu wa fedha, vifaa na malipo batili ni jumla ya shilingi za Kitanzania shilingi 9,915,182,895. Naomba kurudia kumradhi. Jumla ya pesa za malipo batili ni jumla *T.Sh.* 915,882,895.93. Hizi ni fedha nyingi kulinganisha na hali halisi ya Watanzania na kwamba kuna miradi mingi ya uzalishaji na ya kijamii ambayo imekwama kutokana na kukosa fedha. Kati ya fedha hizo upotevu wa fedha taslimu (*cash*) ni shilingi za Kitanzania 659,564.54, sawa na fedha za kujenga madarasa ya *MMES* 94.

Upotevu wa vifaa vyta shilingi 336,280,771 sawa na fedha za kujengea nyumba za walimu 37. Upotevu huu kwa lugha ya uwazi unajulikana kama ni wizi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa makini zaidi kwani wizi sehemu za kazi hasa katika Idara ya Fedha na Manunuzi umekuwa ni tatizo sugu ndani ya Serikali. Hali hii inachangiwa sana na usimamizi hafifu ndani ya Serikali. Hali hii inachangiwa sana usimamizi hafifu wa rasilimali za umma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hasara iliyopatikana na kutokana na kushindwa kukusanya mapato yaani maduhuli ambayo ni jumla ya shilingi 8,888,454,882.40. Hili kwa kweli ni suala ambalo linahitaji kuangaliwa kwa undani zaidi ili kuepusha hasara kama hii. Serikali kwa kweli inahitaji kuwa na uadilifu katika siku za usoni. Kati ya hasara hiyo imesababishwa na makampuni au mashirika kutokuwa na hali nzuri ya kibiashara jambo linaloilazimu Serikali kufuta madeni na pia kuwaongezea mtaji wa uendeshaji wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani kufuta madeni siyo kama utakuwa ni uhakika wa kampuni hiyo kwamba itaweza kujidesha. Jambo la msingi ni je, kampuni hiyo iko katika mazingira ya ushindani? Kama ikisaidiwa inaweza kujidesha? Mfano mzuri ni Shirika la Posta. Tuna uhakika Shirika hili liko katika nafasi nzuri ya kuwa shindani kama utawala na uendeshaji wake utakuwa nzuri. Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa usimamizi na *internal control* ndani ya Taasisi za Serikali uimarishwe na pale dalili za ubadhirifu na wizi zinapojitokeza hatua za haraka zichukuliwe mara moja. Kuoneiana

haya ndiko kunakotufikisha hapa kwani maofisa wanapoona kuwa wenzao wameiba na hawakuchukuliwa hatua yoyote nao hupata pia kishawishi cha kutekeleza wakiamini nao pia hawatachukuliwa hatua yoyote. Na Bunge litafuta kama tunavyofanya sasa kuhusu upotevu huu. Hii ni hali ya hatari sana katika kujenga Utawala Bora (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, haijaridhishwa na sababu zilizotolewa kuhusiana na upotevu wa shilingi 121,388,140.00 uliosababishwa na kushindwa kuwakata kodi Waheshimiwa Wabunge baada ya kuwalipa *honorarium* katika kipindi cha mwezi Novemba na Desemba, 2005. Ilishindikana kwa sababu eti baadhi yao walipoteza viti vyao katika Bunge jipya hivyo ingekuwa ni vigumu kuwafuatilia mahali walipo. Hivyo maamuzi yakawa kuwaacha kuwakata Wabunge wote (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaanua kuwa *pay as you earn* inakatwa kabla ya fedha hazijafika kwa mwenyewe, kwa maana hiyo inatufanya tuamini kuwa fedha hizo wenyewe Waheshimiwa walioshindwa hawakulipwa. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi wa kina kuhusu jambo hili kwani iwapo mshahara haujalipwa hata *pay as you earn* nayo inapoteza maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walilipwa huo ni uzembe ambao tunadhani Bunge hili likikubaliana nao basi ina maana hata wale wastaifu au wanaoachishwa kutokana na ubinafsishaji hawatakiwi kukatwa katika mishahara yao katika miezi wanayokubaliana na mwajiri kuwa wasikatwe *pay as you earn*. Kambi ya Upinzani inapenda kukumbushia kuwa sheria ni sheria na isibague. Kwani Wabunge wakishatunga sheria hiyo na wao wanatakiwa kuitekeleza na inawafunga pia sawa kama mwananchi yejote. Wabunge ni kioo cha Jamii katika kufuata sheria vinginevyo wananchi watashindwa kufuata sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hasara nyingi kusababishwa na wizi ambao wahusika wakienda mahakamani huachiwa huru kwa kukosekana kwa ushahidi wa kutosha, hili kwa upande wetu tunakuwa na wasiwasi kuwa wizi huo unahuisha watendaji walio katika ngazi za utawala, *Managerial Positions*. Jambo linalosababisha kuvuruga ushahidi au kuharibu ushahidi na kusababisha watuhumiwa kuachiwa huru. Tunaitaka Serikali iwe makini sana katika kufuatilia upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali. Wahusika katika fani ya Uhasibu, Ukaguzi na Uboharia waboreshewe mazingira yao ya kufanya kazi ili wasishawishike kuihujumu Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha (*Makofi*).

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chacha Wangwe, kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema pale asubuhi kwamba bado tuna kazi mbili kwenye Meza ya Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitaomba kwenye hoja hii niwaite wachangiaji kulingana na muda nitakaoona unatosha. Na nitangaze tu kwamba siendelei tena kupokea maombi ya kuchangia hoja yoyote ambayo ilikwishawekwa Mezani toka asubuhi.

Kwa hiyo, naomba nianze kumwita Mheshimiwa Dr. Slaa na Mheshimiwa Estherina Kilasi ajiandae. Maamuzi ya uchangiaji yatabakia kwenye Meza ya Spika. Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa!

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nichangie hoja iliyooo mbele yetu. Nitangaze toka mwanzo kwamba siungi mkono wa kufuta shilingi bilioni 9.8 kwa sababu zifuatazo:-

Ingelikuwa tunaletewa tu hoja ya kufuta yale maeneo kwa mfano ya watu waliokufa, kwamba mtu amekufa hawezu kulipa madeni yake, ningelewa. Yako machache sana. Wale ambao mahakama imewahukumu na hikuelekeza kwamba baada ya kifungo chao walipe pia, ningeweza kuvumilia. Ninaelewa vizuri kwamba shilingi bilioni 1.5 wanazodaiwa Wanajeshi wetu kwa ajili ya mkopo wa magari ambazo zimetokana na *exchange rate*, yaani kiwango cha dola kilichobadilika, ninakielewa. Ninaweza nikavumilia, pia kiwango kinachohusisha makampuni yaliyobinafsishwa ambayo hakifiki kama shilingi milioni 700 kwa hesabu za harakaharaka. Lakini kufuta jumla ya shilingi bilioni zaidi ya 7 bila maelezo ya kuridhisha, mimi siafiki kabisa.

Mwaka 2002 wakati tunajadili Azimio kama hili Waziri wa Fedha alituambia kwamba sasa tumetunga sheria ya manunuzi na kwamba mambo haya ya kufuta sasa yatakoma. Leo ni mwaka wa 5 na kwa uzoefu wangu kwa miaka yote mitano kila mwaka tumeletewa kufuta mabilioni. Na yote ni mabilioni zaidi ya 10 kwenda juu. Hii ni hali isiyoweza kukubalika. Mwaka huo huo 2002 aliyezeka Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mramba, alitutangazia kwamba wanaandaa wahasibu, akatutajia hata idadi ya wahasibu wanaosomeshwa kwa kodi ya wananchi. Leo ni mwaka wa 5 bado tunaendelea kusema kwamba wataalamu waandaliwe, inachukua miaka mingapi mpaka hao wataalamu waandaliwe? Nina mambo ya msingi hapa. Kuna suala la wazi kabisa la uzembe, Serikali inafuta haijatuambia hawa wazembe wamechukuliwa hatua gani. Haiwezekani fedha za umma zikachukuliwa kwenye ofisi mtu akaondoka nazo baadaye hakuna ushahidi kesi inafutwa eti kwa sababu umekosekana ushahidi. Kwa nini Ofisi ya umma ikose ushahidi wakati ushahidi unapaswa kutunzwa na huyu ni mtu aliyesoma, na tuliamiwa na Waziri wakati ule kuwa anawasomesha na wametumia kodi yetu ili waweze kutunza hizi kumbukumbu, kwa nini mpaka sasa inashindikana? Waziri lazima atujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezi kuelezeza kwa mfano, Ubalozi wetu wa Afrika Kusini, siku wizi umetokea Ubalozini wamekutwa na thamani ya fedha, ilikuwa kwa *Rand* karibu milioni 14,793,740. Hivi hizi milioni 14 kwa nini zimekaa kwenye ofisi, na bahati nzuri nimefika mara nyingi Pretoria, benki haiko hata zaidi ya kilomita kutoka kwenye Ubalozi wetu. Ni utaratibu wa Serikali kwamba fedha za umma zinawekwa kweli kwenye ofisi? Serikali haijatueleza maelezo ya kina. Huu ni uzembe usioweza kuvumilika, na Bunge lisipokemea haya kila mwaka tutafuta haya mabilioni, wananchi wetu wataendelea kuumia, tutaenda kukopa nje asilimia zetu za fedha kutoka kwa wafadhili bado ni arobaini na kitu. Sisi tunaendelea kuomba lakini wakati huo tunafuta hela za kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezi kuelezeza Serikali inapoeleza kwamba eti hizi *NGOs* na *club* zilizochukua hizi hela anuani zao hazijulikani. Serikali itangaze imeshindwa! Kuna ofisi kazi yake ni kusimamia *NGO*. Kila mwaka *NGO* zinajaza fomu

zinazoitwa *returns*, kwenye *return* ukijaza ile fomu unaambiwa eleza anuani yako, *sponsor* wako, simu yako na *physical address*. Leo Serikali inautangazia umma kwamba eti anuani hazijulikani tufute mamilioni ya fedha. Haiwezi kukubalika na Tanzania hatuwezi kuendelea kuvumilia na Bunge hili tutalaumiwa, tutaonekana sisi wenyewe Wabunge ni wazembe kuruhusu vitu vya namna hii. Kama yuko anayetaka kukubali hivyo mimi naomba niondolewe kwenye orodha ya Wabunge wanaokubali kufuta, sitaki kupokea lawama kwa Watanzania kwa sababu ya namna hii. (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuelewa unaponiambia suala la Wabunge, limeelezwa vizuri kwenye taarifa ya Upinzani sitaki kuirudia. Lakini siwezi kuelewa kwamba sisi tunaotakiwa kuwa kioo, kuwa mfano, Wabunge eti ndio tumeshindwa kulipa, watu wa kawaida anayekuwa na kipato kidogo analipa kodi mimi Mbunge eti nasamehewa! Siwezi kuelewa ni sababu gani ya msingi itakayofanya Serikali inisamehe kulipa kodi. Wasamehewe Watanzania wote wanaopata angalau hata laki moja basi. Lakini tunashindwa kuwasamehe hawa amba hata sukari wanashindwa kununua, sabuni wanashindwa kununua, lakini sisi tunasamehewa, Serikali inaleta hiki kitu! Yule ambaye alifanya hawa wasiweze kukatwa ameachwa na Serikali haina majibu ya kuridhisha. Serikali haina maelezo na ninasema kwa sababu hii siwezi kuunga mkono (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ili niwaachie na wenzangu waseme, ninapenda niseme ifuatavyo:-

Sitaunga hili lakini kwa safari ijayo pia ningependa Bunge hili liweke Azimio kwamba inawezekana azimio hili likaletwa kwa sababu kuna sheria kweli inaruhusu Bunge kufuta katika mazingira ambayo ni ya kweli. Lakini katika mazingira kama haya ni lazima Bunge sasa liweke Azimio kwamba Serikali isilet mbele ya Bunge kitu cha aibu kama hiki bila kuleta tathmini ya hatua zilizochukuliwa kudhibiti hali hii, hatua gani zimechukuliwa kwa wale waliofanya uzembe na kwa namna gani wale amba wamesababisha uzembe huu wamekwisha kuchukuliwa hatua. Hayo waliyoyasema kwamba yako yamefanyika kule ofisini, hapa sisi hatuwezi kuyaona. Bunge linatakiwa ndio litoe Azimio, hatuwezi kutoa Azimio kwenye kitu tusichojuwa. Haiwezekani kabisa mtu anachukua shilingi milioni 5 halafu eti unaniambia amepotea! Hivi nchi hii kuna mtu anaweza kupotea? Unaenda wapi? Mabalozi wa nyumba 10 wako kila mahali.

Mtu anachukua shilingi milioni 164 halafu tunaambiwa kwamba hilo limeachwa, kesi imefutwa, hakuna ushahidi, tena kwenye Ofisi ya Polisi. Ingekuwa ofisi ya kawaida unaelewa! Wizi huu, upotevu huu, umehusisha Polisi, Magereza, umehusisha vyuo vyetu vya shule, maeneo ambapo unategemea ndio mfano, ndio wanaokamata wahalifu, sasa nani atawakamata wao? Kama kesi iliyotokea fedha zilizopelekwa kwa ajili ya mirathi na watu wetu wanaodai mirathi wanateseka. Fedha ya mirathi inapotea mikononi mwa Polisi, hakuna maelezo ya Serikali kuwahurumia watu wa aina hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ya kusikitisha lakini kwa ajili ya manufaa ya muda, naomba nimalizie kusema narudia siungi mkono hoja na naomba suala hili likemewe kwa uzito unaostahili na Wabunge wote bila kujali itikadi yetu. Nashukuru.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache kutokana na hoja hii ya kuridhia kufutwa kwa hasara ya fedha na upotevu wa vifaa. Mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya PAC, lakini nimesimama hapa kuchangia kwa baadhi ya mambo ambayo mwenyewe nimeyaona ni muhimu nichangie katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba tulipofuta madeni kipindi kilichopita Kamati yetu ilipendekeza kwamba tunavyoju tunasafisha vitabu baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuitia kwa undani kuona kwamba haya yote ambayo yamejonesha katika vitabu hivi hayatakusanya kabisa au yamepotea kabisa, yaani yatakusanya baada ya muda mrefu. Kwa hiyo, tuliiomba Serikali au Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii kwamba tunaomba kipindi kijacho unapokuja kuleta Azimio kama hili tena, utuletaa *progress report*. Kwamba pamoja na kwamba Wabunge walikuwa wanafuta madeni haya au hasara hii lakini katika bilioni mlizofuta kipindi kilichopita, Serikali imejitahidi kukusanya kiasi hiki na hiki kimeshindikana kabisa. Kwa hiyo hii tumeshindwa kuipata na sisi Kamati tulipitia, lakini tukakubaliana kwamba kipindi kijacho watafanya hivyo.

Lingine Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa upande wa wizi amba o umekuwa ukitokea kila wakati, hasa kesi zinapotolewa. Kwa kweli mtu anaonekana ameiba, nachukua mfano wa ofisi ya Waziri Mkuu. Ni huyu Mhasibu akishirikiana na wenzake 8 waliiba shilingi milioni 326.7. Lakini huyo huyo akahamishwa kwenda Wizara nyininge. Kukatokea wizi wa shilingi milioni 700 ambazo tulizifuta wakati wa kipindi kilichopita. Sasa kesi mwezi wa sita imekwisha, wale wengine wameachiwa huru na wamerudishwa kazini. Lakini huyu mmoja ndio amepatikana na hatia. Sasa kidogo na mimi linanipa shida, tunapunguza au tunaongeza changamoto watu waendelee kuiba kwamba nikiba ushahidi usipopatikana nitaendelea kuwa kazini. Kwa hiyo, nilichokuwa nakipendekeza kwamba kama ni sheria inatubana basi turudi kwenye sheria tuangalie au ikibidi kabla hujaipeleka kesi mahakamani huyu mtu afukuzwe kazi kwanza ndio akashitakiwe akakabidhiwe kwenye vyombo vya sheria, kusudi isimpe ari mtu mwingine kuendelea kuiba (*Makofi*).

Kwa hiyo, nilitaka niliseme hili Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu limekuwa likinigusa kwamba kwa nini mtu anarudi, kweli wamerudi na kila kitu kinajulikana kwamba huyu mtu kaiba kwenye vyombo ambavyo angalau vinahusika kabisa tunavitumia katika kufanya upelelezi. Na ukiangalia jedwali hili wizi mwangi umetokea kwenye vyombo vya Polisi, sefu zimevunjaw, mishahara ya watu shilingi milioni 24, kwa mfano, ofisi ya Dar-es-Salaam, Msimbazi, shilingi milioni 24 ziliibiwa lakini napo ushahidi haukupatikana na watu wakarudishwa kazini.

Sasa kwenye upande wa vifaa Magereza ni vyombo ambavyo angalau ni vya askari wetu vya usalama. Wizi mwangi unaouona kwenye *schedule* ni wa kupotea kwa vifaa kwa mfano vyakula vya wafungwa, vya mahabusu, karibu shilingi milioni 197. Na mimi katika Kamati yangu tumekuwa tukiwahoji Maafisa Masuhuli ambao wanashughulika na mafungu haya, tunawaambia hivi inakuwaje? Ni kweli mtu

anasafirisha mahindi kutoka Dar-es-Salaam kwenda Mtwara yananyeshewa halafu unaambiwa yameoza. Ni chakula kweli mahindi? Yangkuwa ya mtu binafsi ya kwako kweli mahindi yamenyeshewa huwezi hata ukayatumia kwa mbinu nyingine. Hata ukayasaga basi unga ukatumika kwa wafungwa wengine, lakini ndio maana yanamwagwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali imetuambia au Waziri ametuambia kwamba upotevu umekuwa ukipungua, lakini mkikaa kutafakari kwenye hizi tunapowahoji Maafisa wahasibu unaona kama hili jambo mara mwaka huu linapungua, mwaka unaofuata linaongezeka.

Lakini nije kwenye hili la maduhuli ambayo hayakusanyiki. Sasa hivi labda Waheshimiwa Wabunge na wenzangu waliochangia kwamba shilingi bilioni 8 ni makadirio ambayo yaliwekwa kama kodi kwenye makampuni haya ili yalipwe. Na tunaamini makadirio unategemea kukusanya. Na unategemea makampuni yafanye vizuri, lakini kwa bahati mbaya imetokea na wenyewe tumejionea mashirika ya umma mengi hayakufanya vizuri. Na ikafikia kwamba haya madeni yachukuliwe na Serikali. Kwamba unayemuuzia kampuni huwezi ukamuuzia na deni la kodi. Kwa hiyo, Serikali ingeweza kulipa. Sasa sisi kwenye Kamati yetu tulipokaa tuliona ni muafaka kabisa tulifute kwa sababu tukibaki nalo kwenye vitabu hayatakaa yalipwe. *NARCO* haipo, *DAFCO* haipo utamurai nani? Aidha, Serikali mkono huu iichukue ikawalipe *TRA* ambapo pesa zinarudi tena kwenye Serikali hiyo hiyo. Kwa hiyo nafikiri hili katika kusafisha vitabu hivi tukubaliane kwa pamoja kwamba hili ambalo linasema mapato hayakusanyika kwa sababu ni mashirika na hayapo, basi ifutwe ili kusafisha kitabu lakini tusikubali tena wakati mwingine yaje haya, kwamba makadirio yawe *realistic*. Ukadirie kile kitu ambacho unafikiri kitakusanyika.

Kwa upande wa milioni 125 ilitupa shida sana kutokana na melezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tuliposoma tukaambiwa *payee* haikulipwa kutoka kwenye mishahara ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa tukamuuliza kwamba, kwanza *payee* ni *withholding tax* ambayo Mbunge anapata *net salary* au mfanyakazi yeoyote, ilikuwaje? Lakini nasema tuliridhika na maelezo na nafikiri labda Waziri anapoitoa hapa angekuwa ameirekebisha kama tulivyokubaliana pale. Kwamba hiyo miezi miwili, mshahara wa Mbunge ni mwisho mwezi wa 10, na mara nyingi *pay role* yetu inaishia mwezi wa 10 tarehe 30 uchaguzi unapofanyika wanaanza Wabunge wengine.

Sasa baada ya pale uchaguzi ulahirishwa, Wabunge hawakulipwa mshahara kwa kipindi hicho. Kwa hiyo, kilichoonekana ni posho kwa ajili ya Wabunge kujikimu kwa kipindi hicho yule ambaye anajua sitapata au atapata. Kwa hiyo, wenzetu wa *TRA* walipofika walitathmini kama ilivyo kawaida kwenye vitabu vyao wakajua hii ilitakiwa ilipwe na Wabunge wakaingiza kwenye vitabu vyao. Lakini baadaye ikaonekana kwamba haikuwa imekatwa kwenye *basic salary* ya Mbunge. Ilikuwa ni kama posho ya kumfanya huyu Mbunge aishi, kama mnapolipwa posho zingine. Na iko kwenye sheria kwamba zinakatwa posho za Wabunge. Kwa hiyo, ndio maana na sisi Kamati yetu iliridhika kabisa kwamba hili deni liingizwe kwenye kufutwa. Sasa kama ni maelezo yametolewa hapa, nafikiri Mheshimiwa Waziri angeweza kuyarekebisha hayo maelezo (*Makofi*).

Lingine ni kwa upande wa Wahasibu. Kwa kweli tumekuwa tukilisema muda mrefu na Maafisa Ugavi. Ni tatizo kubwa sana kwenye mafungu mbalimbali. Kuna watu wamekaa miaka 20 Afisa Ugavi, namuuliza uko tayari kwenda shule? Lakini ukimuangalia kwenye miaka 60 au miaka 55 anangojea kustaaful. Hata ukimwambia aende akasome, hawezo na anafanya kazi kwa mazoea. Sasa hii imetuletea tabu sana. Kwenye upande wa utunzaji wa vifaa vyta Serikali imekuwa sio rahisi kupata takwimu safi, haiingizi aidha kwa uzembe au kwa kutokujua. Kwa hiyo, tukasema Serikali hili iliangalie.

Lakini tulisema kwa upande wa wahasibu wapangwe kutokana na mafungu, ukubwa wa mafungu na uzito wa fungu. Sasa unamkuta mtu wa *CPA* labda yuko Ofisi ya Bunge hamna *transaction* nyingi. Lakini Mhasibu ana *ADA* yuko Ngome, yuko Wizara ya Maliasili na Utalii, mapato ni mengi, matumizi ni mengi, sio rahisi akaweza *ku-manage* mafungu hayo. Kwa hiyo, tukafikiri wenzetu angalau wangepitia sasa. Wawe na muda muafaka wa kupitia kila fungu waangalie Afisa Mhasibu, waangalie *Accountants* wale, kwamba huyu anafaa akae wapi na huyu akae wapi. Kwa hiyo, hili liende sambamba na Maafisa wa Ugavi (*Makofi*).

Mwisho, anayewasilisha hapa ni Mheshimiwa Waziri, kwa kweli sisi Kamati ya *PAC* mara nyingi tunakuwa na wataalamu, tunakuwa na Maafisa Wahasibu, sasa yanayofanyika huko inawezekana Waziri wewe unakuja unaomba bajeti hapa lakini ikawa sio rahisi ukajua zile pesa zimetumikaje huko. Siku moja moja basi angalau inapotokea tunajadili mafungu ambayo mwenyewe Waziri unaona kabisa fungu lako au Wizara yako imepata hati chafu, ina matatizo, tunafikiri si vibaya ukija ukahudhuria tunapokaa na *accounting officers* hawa ili ujionee kile ulichoomba kama kweli kimetumika vizuri. Na ninafikiri itatoa motisha kidogo kwa wafanyakazi kuwa na woga. Kwa hiyo, hilo nataka nipendekeze Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba ni kitu muhimu sana kwa sababu unakuja unaomba tu hapa lakini hujui kimetumikaje, na vifaa ulivyoomba vinunuliwe kama vimenunuliwa au havijanunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kuhusu Maafisa Wahasibu kuhamishwa kwenda Fungu lingine. Imekuwa ikitupa shida, kwa maana ya Makatibu Wakuu maan yake ndio wanaokuwa *appointed* kuwa Maafisa Wahasibu. Anakaa kwenye Fungu, mahesabu yake yamekuwa ovyo, anahamishwa kwenda kwenye Fungu lingine ambalo ni safi. Sasa napendekeza kwamba kabla, ingawa sio Waziri ambaye ana wajibu huo lakini anayetangaza kwamba awe Afisa Mhasibu kuangalia utendaji wake kule alikokuwa ulikuwaje ili tusimpeleke kwenye fungu lingine aende akaharibu na huko. Kwa hiyo, hilo naomba liangaliwe sana, na ninamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa sababu ameliona hili kwamba Afisa Mhasibu ye yote atakayeharibu hapo alipo maana yake ataondoka na fungu lake. Naamini hilo sasa Mheshimiwa Rais ameliona na tunakwenda vizuri (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono kwa asilimia mia.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Azimio lililoletwa mbele ya Bunge lako. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Azimio hili lakini napenda kumwambia siliungi mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge, tunazo kazi nyingi lakini mbili kubwa ni kutunga sheria na kupitisha bajeti. Tunapofanya kazi hii ya kupitisha bajeti katika Wizara na Mikoa, tunategemea kabisa bajeti hizi zitasimamiwa ili ziweze kukidhi malengo ambayo yamekusudiwa. Lakini kwa haya yaliyoletwa katika Azimio hili inaonesha kabisa jinsi watendaji wetu wanavyoshindwa kusimamia fedha zile ambazo walipa kodi wa Tanzania wametoa na nyingine ni misaada ili waweze kutimiziwa yale mahitaji yao muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekwishasema wenzangu, lakini ningependa kuchukua mmoja tu ambaa nimesoma nikashindwa kuuelewa. Kuna Ofisi ya Ubalozi *DRC*. Kuna pesa zilizotolewa shilingi 900,887,000 kwa ajili tu ya kusafirisha mizigo ya aliyekuwa Balozi wa kule. Hivi ni Watanzania wangapi ambaa wanashindwa kulipa mizigo yao wanalipiwa na Serikali? Je, huu ndio utendaji? Ndio tunawajibika? Wananchi wanatuelewaje sisi viongozi? Huu ndio utaratibu? Ningependa Mheshimiwa Waziri anipatie majibu, vinginevyo Watanzania hawatatuelewa, hii kazi tunayoifanya leo ya kufuta madeni ndio maana nimesema siungi mko....! mkono hoja hii. (*Makofi/Vicheko*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Samahani! Nimesema siungi mkono hoja hii!

Lingine ninalopenda kulisemea ni upotevu wa shilingi milioni 112 za mchele ambazo anatuhumiwa askari. Hivi kweli tunaweza kuwaambia watanzania tunashindwa kumkamata huyu mtanzania mwenzetu aliyechukua kiasi hicho cha pesa? Je, yule wa rada tutaweza kumkamata? Tunawaambia nini Watanzania? Bunge hili kama kweli tutapitisha watanzania watashindwa kutuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mengi lakini kutokana na muda naomba nichangie hayo machache na nisisitize tu kwamba siungi mkono hoja hii kwa sababu watanzania bado wana matatizo mengi, hatuna shule, hospitali zetu hazina dawa, leo tuje tukae hapa kufuta madeni haya, kwa kweli nawaonea huruma Watanzania na nasikia aibu, siungi mkono!

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru kwa kurekebisha kauli yako katika matamshi ya kuelezea nini unachokiazimia. Naomba nimwite Mheshimiwa Msindai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi na mimi nichangie kwa hizo dakika chache ulizonipangia, Azimio hili. Kwa kweli nimesikitika sana kuona tunafuta madeni mpaka ya Juni, 2006, juzi. Hivi kweli

tumeshindwa kupata majibu zile fedha ziko wapi? Tumeshindwa kupata majibu vile vifaa viko wapi? (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana, Sheria ya Fedha na Sheria ya Manunuzi zizingatiwe sana. Sheria ya Fedha na Sheria ya Manunuzi zizingatiwe. Sheria hizi zilipokuja Bungeni, Serikali ilituambia kwamba sasa uzembe ule wa manunuzi na upotevu wa fedha usio na msingi utakwisha. Lakini leo bado unakuja. Na mwakani tutaletewa tena fedha zingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina wasiwasi na wasimamizi wa fedha hizi. Wengi sio waaminifu, wengi wanashirikiana na wale walio chini yao ili kucheza na fedha na vifaa vya Serikali. Na mimi ningeiomba serikali, kama alivyosema Mheshimiwa Kilasi, hebu wafanye sensa ya wahasibu wote. Sasa hivi tuna wahasibu wengi sana wenye sifa za kufanya hizi kazi lakini wapo wale ambao wako kwa miaka mingi walipanga vyeo kwa kukaa muda mrefu kazini na wale ndio wanawawekea *kauzibe* wahasibu wetu waliosoma. Mimi naomba tusioneane aibu tufanye sensa wale wakae pembeni tuwaweke wahasibu wenye sifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ofisi nyingi za Serikali bado haziwatumi *Internal Auditors*, *Internal Auditors* wamebanwa hawapewi nafasi kufanya kazi mapema, kwa sababu hawa wakipewa nafasi ndio watu wa kwanza kugundua na si ajabu *Internal Auditors* wengine hawafanyi kazi zao wamekuwa kama wahasibu wa kawaida. Mimi naomba Serikali ipitie na hawa *Internal Auditors* wavezeshwe kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningetofautiana kidogo na pendekezo la Kamati juu ya zimamoto, wamezungumzia magari ya zimamoto lakini sasa hivi uhakika ninao kuna magari ya zimamoto yananunuliwa kienyeji na mpaka sasa ukienda Idara ya Zimamoto yapo pale yameshindwa kusajiliwa. Kuna mifano ipo, injinia wa Halmashauri ya Wilaya, injinia mdogo kama yule wanakwenda na mhasibu nje kuangalia gari la zimamoto, hivi sheria za manunuzi ya Serikali zilishafutwa? Manunuzi ya Serikali yanasmamiwa na Idara ya Ujenzi sasa leo anatoka *engineer* mdogo kwenda Malyasia, kwenda Ulaya kwenda kuangalia gari la zimamoto. Tutaendelea kuteketeza mali zetu kwa moto kwa stahili hii, kwa hiyo, mimi ningeomba Serikali iangalie sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kesi zetu zinazopelekwa mahakamani. Afisa Mhasibu akishafungua kesi basi hafuatilii, inakwenda yenewe na inajizika yenewe na hawa wanaotuibia hela zetu wanacheza na fedha zilezile walizoiba pamoja na Mahakimu wachache ambao siyo waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakushukuru lakini naomba Serikali ijipange sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kunipa nafasi na mimi kujibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa katika hili Bunge lako Tukufu. Kwanza Mheshimiwa Grace Kiwelu, amesema kwamba kazi ya Bunge siyo sheria tu na bajeti. Kumbuka leo asubuhi katika Kamati zilizotajwa mojawapo ni *PAC* na Kamati nyingine ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ni moja katika wajibu wetu. Na sisi kama sheria inavyosema tunawajibika kwa Mkaguzi Mkuu (*CAG*) na *Accountant General*. Baada ya *CAG* kutoa ripoti yake tunawajibika kupeleka *PAC* na *PAC* kama Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa ameipitia taarifa yote hii ungekuwa umeona ndani yake kila kesi ya upotevu ulivyotokea katika Wizara mbalimbali. Utaona Sh.8,888,454,882.4/= ni maduhuli ambayo yalikuwa katika *estimates* ambayo hayakupatikana. Kwa hiyo, kiasi hasa ambacho hakikukusanywa ni shilingi bilioni moja na kitu hivi.

Waheshimiwa Wabunge kutokana na busara ya Bunge hili Tukufu hapo siku za nyuma mwaka 2002 kama ulivyosema Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Basil Mramba wakati aliposimama katika Bunge lako Tukufu hili, Bunge likaamua kuwa upotevu huu usiwe unafutwa tu lakini lazima upitiwe na *PAC* uletwe hapa na ukubaliwe na *PAC* na ule ambao bado uchukuliwe hatua. Utachukuliwa hatua kama tunavyokwenda na mwingine umebakizwa, hivyo *PAC* wamebakiza huu ambao hawakubali ili tuendelee nao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mgana Msindai unaposema unashangaa fungu hili la sita kwamba baadhi ya upotevu mwingine umefutwa ni kitu ambacho hakiwezi kupatikana kwa njia yoyote ile. Wizara ya Afya haiwezi na vitabu vyetu lazima viwekwe sawa.

Waheshimiwa Wabunge mwaka 2002 upotevu wetu ulikuwa zaidi ya shilingi bilioni 72. Nikawaomba mwongozo wenu na mwongozo wa Bunge lako Tukufu hili. Katika kurekebisha wahasibu na uhakikimali kwa sehemu mbalimbali za Serikali ndio maana hivi leo tumefikia hapo, upotevu wa shilingi bilioni 9 kutoka bilioni 72, 1/8 na siyo kwamba Waziri wa Fedha ndio anakuja kutaka kwamba zitue hapa ni kwa umahiri wa *PAC* iliyokaa na kuchambua kupitia moja moja ya haya yaliyokuwemo katika kitabu hiki.

Upotevu umetokea vipi na hakuna lililofichwa hapa na kutokana na hesabu ya *Controller and Auditor General* ya mwaka 2005/2006 ndio *PAC* ambayo sote Waheshimiwa Wabunge wote kwa kambi zote mbili, kwa vyama vyote wapo kule na wao kwa niaba yao tunasimama hapa kama Waziri wa Fedha mwenye jukumu la kuja kutaka kufutiwa upotevu ambao hawezi kurekebisha vitabu vyetu ndio maana tunaleta hapa. Kwa hiyo, kusema Sh.8,888,454,882.40/= kukubali zifutwe tutazipata wapi jamani? Huwezi kusema kwamba zile fedha lazima ziwepo, zitapatikana wapi na mashirika yale hayaku-perform vizuri kama ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sensa ya wahasibu na wahakikimali kama alivyoomba Mheshimiwa Mgana Msindai imefanywa na ndio maana kila mwaka tunaajiri wahasibu na wahakikimali kuhakikisha kwamba tunawapeleka hata huko kwenye Halmashauri ili na hesabu za *local government* ziweze kukaa sawa. Na ndio maana tumeweza kupata ufanisi huu wa kupunguza upotevu kutoka shilingi bilioni 72 mpaka tukapata 1/8 ya

biliontiisa tuzakwana ni kweli Mheshimiwa Mgana Msindai tunakubali kwamba kuna wahasibu au wahakikimali kwa mazoea tu na bado wanaachiwa katika Halmashauri na asubuhi si mmesema hapa, wakati tunajibu baadhi ya maswali tunesema hapa na nimwambie hata Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na huko kwako nako wapo muwasaidie hawa wapya waliokuja washirikiane na hawa wahasibu tunaowaleta ambao ni *trained* pamoja na wahakikimali ili haya yapungue na hayo ndiyo makusudi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Posta, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Miundombinu amesema kwamba Shirika la Posta sasa hivi kazi zimepungua. Kuna mambo hayawezi kufanywa tena na Shirika la Posta, lazima tuyatolee baadhi ya haya madeni ambayo hawayewezi tena wao kuyarejesha kama ni maduhuli ya Serikali. Jamani leo tunakuja hapa tena tuseme Mashirika ya Posta lazima yapate maduhuli yale ambayo hawayewezi kuyapata kwa njia ye yeyote ile? Tuna-*refute exercise* yenye.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Serikali inawasilizeni mnaposema hili lipunguzwe, ndio tunakokwenda huko na ndio maana tumefuzu tumefika hadi kwenye shilingi bilioni tisa kwa sababu tunawasilizeni. Mheshimiwa Estherina Kilasi ni bahati mbaya kwamba hatukushiriki mara hii na mimi, hali yangu ndiyo hiyo lakini siku zote huwa nashiriki katika mikutano yote ya *PAC* mnapojadili *Controller and Auditor General reports*, nakuhakikisha kwamba yale yote na tufanye nini, tunahakikisha kwamba *progress reports* tutatengeneza kwa mujibu wa matakwa yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache labda nimwombe mwenzangu aje kuendelea na mimi naunga hoja mkono hoja hii asilimia mia moja. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba wengi wamejitokeza kuchangia hoja hii. Ningependa kuwatambua wale waliochangia na wa kwanza ni mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, Mheshimiwa Felister Bura na upande wa Upinzani ni Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mgana Msindai na mwisho ni Mheshimiwa Abdisalaam I. Khatib. Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna waliochangia kwa maandishi, nao ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Madgalena Sakaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu amejaribu kujibu kwa ufasaha, mimi nitajaribu kueleza yale ambayo yanawafanya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na Mheshimiwa Chacha Wangwe wakatae kuunga mkono hoja hii. Kwanza, Mheshimiwa Abdisalaam Khatib ameelezea haya yote tunayoyapendekeza hapa, mengine yanaanzia mwaka 1981/1982 mpaka mwaka jana, sasa Serikali ilichofanya ni kweli huko nyuma tulikuwa na matatizo lakini tumeanza kuhakikisha kwamba haya hayatokei tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 Waheshimiwa wa *CHADEMA* watakumbuka kwamba aliye kuwa mgombea Urais mwenza, Mwenyezi Mungu alimchukua wakati tuko kwenye mchakato wa uchaguzi. Ikabidi uchaguzi uahirishwe

kwa miezi kadhaa kama isingekuwa hilo malipo yote ya Wabunge yalikuwa yamekwishalipwa mpaka mwisho wa mwezi wa Oktoba lakini kwa sababu ulikuwa haujakamilika Wabunge wale wakalamika kwamba wanastahili wapewe malipo mpaka mwisho wa Desemba.

Kwa utaratibu malipo yale hayakuwa kwenye utaratibu kwa sababu Bunge lilikuwa limekwishamaliza muda lakini kulikuwa na watu ambao walidai wapewe pesa, kilichofanyika hawakulipwa mishahara, wanglipwa mishahara kusingekuwa na matatizo kwa sababu ukilipwa mshahara kuna mfumo maalumu wa kukatwa kodi, unakatwa kabla ile *balance* yako hujalipwa, wakaona wawalipe *honorarium*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukitumia neno *honorarium* ni kama vile umekwenda kutoa mhadhara mahali. Arusha unakwenda kutoa semina wanakulipa *honorarium* kwa utaratibu wa kodi *honorarium* haikatwi kodi. Sasa baada ya kuwalipa Waheshimiwa Wabunge TRA wakachukua kwamba hawa ni Wabunge na kwa sababu ni Wabunge walitakiwa wakatwe kodi, kwa hiyo, waka-*rise demand* za kulipa kodi. Maelezo ya Mlipaji Mkuu wa Serikali ni kwamba kwa kweli huu haukuwa ni mshahara kwa maana ya mshahara, kilikuwa ni kitu kingine, nadhani hivyo ndivyo ilivyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nitamshangaa sana rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kama utaacha kuunga mkono mapendekezo haya kwa sababu hiyo. Mimi nakuomba kwa kweli kwa sababu Serikali imejitahidi kusawazisha mambo, kwa mfano, sasa hivi katika muda wa miaka miwili iliyopita tumeajiri wahasibu na wakaguzi 1,500 ambao tumewasambaza kwenye wizara, kwenye Halmashauri na kwenye MDAs. Ni mategemeo yetu kwamba kwa kweli jinsi tunavyoendelea uhasibu ndani ya Serikali utakuwa mzuri zaidi.

La pili ambalo pengine wenzetu ambao wamechangia sana kwa maandishi ni *effectiveness* ya *public procurement process*, tunakubali kwamba kuna *weaknesses*, tumepokea mapendekezo tutayafanya kazi. Ni matumaini ya Serikali kwamba kwa kweli tunaweza tuka-*improve* upande wa *procurement* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, mimi nilihudhuria kweli Kamati ile kwa niaba ya Waziri na Kamati ya PAC inalalamika kwamba Mawaziri wa Fedha na Manaibu wake hawahudhurii Kamati ile, nadhani niliyowaeleza yalikubalika. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba vikao vitavyofuata Waziri mwenyewe au mmoja wa Naibu Mawaziri wake watahudhuria vikao vile.

Lakini pia ningependa kusema kwamba si kweli kwamba yuko Waziri siyo tu Waziri wa Fedha Waziri ye yole yule nadhani bosí wangu Waziri Mkuu anasikiliza, hakuna Waziri ye yole kwa kweli ambaye anadharau Kamati ya Bunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu tu ni kwamba kinachotokea mara nydingi wanapewa taarifa maofisa, sasa ofisa akipewa taarifa anajua tu kwamba yeze anatakiwa kwenda kutoa maelezo kule haweziz kwenda kumwambia Waziri wake kwamba mimi nimeitwa.

Nafikiri kinachotakiwa ni kujulishwa tu rasmi kwamba kuna siku fulani kuna kitu fulani, Waziri fulani atatakiwa ahudhurie, kwa mfano, Waziri wa Fedha bosi wangu hajawahi kukosa kuhudhuria kikao cha Uchumi na Fedha. Kwa hiyo, hakuna sababu kwa nini asuhudhurie kikao cha *PAC*. Kwa kuwa niliomba nizungumze kwa uchache, natumaini yale mengine yamekwishajibiwa na mwenzangu, niliona nisisitize tu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge kuridhia kufuta na  
kusamehe madeni liliptishwa na Bunge)*

**Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya NEPAD kuhusu Mwongozo wa Sera ya Udhibiti na Ujenzi wa Mkongo wa TEKNOHAMA wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini.**

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Bunge lako Tukufu liniwie radhi kwa sababu ya sauti yangu, hali ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya NEPAD kuhusu Mwongozo wa Sera na Msimamizi wa Mkongo wa Teknolojia, Habari na Mawasiliano TEKNOHAMA wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (*The Protocol and NEPAD ICT Broadband Infrastructure Network for Eastern and Southern Africa*). Kabla ya kuwasilisha rasmi Azimio hilo la Bunge napenda kutoa maelezo mafupi kuhusu chimbuko la itifaki hii ya NEPAD.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2003 Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika AU waliidhinisha mpango wa NEPAD wa kujenga mikongo ya baharini (*sub marine fibre optic cable*) itakayolizunguka Bara la Afrika na pia mikongo ya nchi kavu (*terrestrial backbone network*) inayoziunganisha nchi zote za Afrika. Lengo la mpango huu ni kuziunganisha nchi zote za Afrika na pia kuliunganisha Bara la Afrika na nchi nyingine Duniani kwa mawasiliano ya uhakika yaliyo bora na yenye gharama nafuu.

Mpango huu utaruhusu mikongo mitatu ya mawasiliano kama ifuatavyo: wa kwanza mkongo wa mawasiliano unaziunganisha nchi za kanda ya Afrika Magharibi, Afrika ya Kati na Kaskazini, wa pili ni mkongo wa mawasiliano ya nchi kavu kwa nchi za Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika utakazozungisha nchi zote za ukanda huo na vituo vya mkongo wa baharini vitakavyojengwa katika Pwani ya Bahari ya Hindi na tatu ni mkongo wa mawasiliano wa baharini utakaopita katika ukanda wa Pwani wa nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (*the East African sub-marine fibre optic cable system*) maarufu kama *Easy Project*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa Mradi wa *Easy* ambao kuanzia tarehe 15 Oktoba, 2007 unafahamika kama uhuru *network* umeasisiwa na nchi 23 za Bara la Afrika ikiwemo Tanzania pamoja na makampuni 33 yanayotoa huduma za mawasiliano. Kwa upande wa Tanzania makampuni hayo ni ZANTEL, TTCL na SATCO ndiyo yaliyotia saini hati ya makubaliano *MOU* ya kutekeleza mradi huu. Nchi hizo 23 ni Uganda, Kenya, Tanzania, Rwanda, Burundi, Msumbiji, Lesotho, Botswana, Somalia, Malawi, Zambia, Zimbabwe, DRC, Ethiopia, Eritrea, Swaziland, Angola, Namibia, Sudan, Djibout, Madagascar, Mauritius na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki ya *NEPAD* iliyombele ya Bunge lako Tukufu ilisainiwa mjini Kigali nchini Rwanda, tarehe 28 Agosti, 2006. Nchi zilizosaini itifaki hiyo siku hiyo ni saba yaani Lesotho, Tanzania, Madagascar, Malawi, Rwanda, Afrika Kusini na Uganda kati ya nchi 23 zilizoidhinisha mradi wa mkongo wa mawasiliano wa Uhuru *Network*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, itifaki hiyo iliwekwa wazi kwa kusainiwa mpaka tarehe 30 Novemba, 2006. Hadi kufikia tarehe nchi tano zaidi zilikuwa zimekwishaweka saini itifaki hiyo. Nchi hizo ni Zimbabwe, DRC, Botswana, Mauritius na Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya muda maalumu uliowekwa wa kusaini itifaki hiyo kwisha nchi zilizosaini itifaki hiyo zinatakiwa kuiridhia itifaki hiyo na hatimaye itifaki hiyo kuwasilishwa kwenye Sekretarieti ya *NEPAD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali madhumuni ya hoja hii ni kuliomba Bunge lako likubali kuridhia itifaki ya *NEPAD* kuhusu mkongo wa mawasiliano wa kanda ya nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika. Itifaki hii inatoa mwongozo wa ushiriki wa kila nchi mwanachama na jinsi ya kuitekeleza kwa ufanisi mikongo ya msingi ya mawasiliano hususan ule wa bahari, Uhuru *Network* na ule wa nchi kavu ambao unajulikana sasa kama Umoja *Network*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki ya *NEPAD* imegawanyika katika sura 10 kama ifuatavyo: Sura ya kwanza inaorodhesha na kutoa tafsiri ya maneno iliyyotumika kwenye itifaki hii.

Sura ya pili, inaelezea madhumuni ya itifaki hiyo pamoja na maeneo yanayolengwa kutekelezwa chini ya mpango wa *NEPAD* na kujenga miundombinu ya huduma za mawasiliano Barani Afrika.

Sura ya tatu, inahusu masuala ya uanzishwaji, umiliki na uongozi wa chombo au vyombo vitakavyoshiriki katika ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa mradi wa mkongo huo wa *NEPAD*. Itifaki inapendekeza kuanzishwa kwa chombo maalumu (*special purpose vehicle*) kitakachokuwa na jukumu la kujenga, kumiliki na kuendesha mkongo huo wa kanda kwa kuzingatia masharti ya itifaki hii.

Sura ya nne, inaelezea haki, wajibu na majukumu ya chombo au kampuni itakayoanzishwa na nchi wanachama kusimamia ujenzi na uendeshaji wa mkongo huo wa kanda.

Sura ya tano, inahusu maelezo ya kisera, usimamizi pamoja na taratibu za utoaji leseni na mwongozo wa sera na usimamizi unaolenga kufanikisha ujenzi wa mkongo huo kwa ufanisi.

Sura ya Sita inafafanua miongozo ya mahitaji ya fedha za mtaji wa Mkongo huo na taratibu za kuweka viwango vya ada, malipo, au tozo kwa ajili ya huduma za mawasiliano.

Sura ya Saba, inaelezea taratibu na masharti yatakayozingatiwa katika kuunganishwa kwenye Mkongo wa Baharini na Mkongo wa Nchi Kavu ambayo hayatakuwa ya kibaguzi (*non-discriminatory*) na yatakayotoa fursa sawa kwa watumiaji wote wa Mkongo huo (*open acces principle*).

Sura ya Nane, inaweka utaratibu wa kutatua migogoro endapo itajitokeza.

Sura ya Tisa, inafafanua na kuweka utaratibu wa kuunda chombo cha juu cha kusimamia ujenzi na uendeshaji Mkongo wa *NEPAD*. Sura ya Kumi na ya mwisho inaelezea taratibu za kurekebisha itifaki hiyo na viambatisho vyake pamoja na masuala mengine ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Bunge lako Tukufu litakubaliana na mimi kwamba teknolojia ya Habari na Mawasiliano ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Itifaki hii itakaporidhiwa Tanzania itakuwa imejiunga kwenye ubia na Umoja wa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika zinazotekeliza mradi wa ujenzi wa Mikongo ya Mawasiliano ya Baharini (*Uhuru Network*) na ule wa nchi kavu (*Umoja Network*) chini ya Programu ya *NEPAD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu wa mawasiliano ni ukombozi kwa Bara la Afrika ambalo kwa muda mrefu maendeleo yake yameathiriwa kwa kiwango kikubwa kwa kutokuwepo na mfumo wa mawasiliano ulio wa uhakika na wa gharama nafuu.

Mradi huu wa *NEPAD* unakusudia kuweka mfumo mbadala wa mawasiliano badala ya kutegemea tu mfumo wa mawasiliano kwa njia ya *satellite* ambao huduma zake ni za gharama kubwa kwa watumiaji na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mkongo wa Nchi Kavu, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maandalizi ya kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mkongo huo yanaendelea vizuri. Serikali imedhamiria kwa dhati kupata mkopo wa masharti nafuu utakaowezesha ujenzi wa Mkongo wa Nchi kavu sambamba na ujenzi wa Mkongo wa Baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu ujenzi wa mikongo hii kusema kweli ni suala la kufa na kupona kwa sababu ujenzi wa jamii habari nchini unategemea sana kuwepo kwa mikongo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kwa Tanzania suala la kutokuwa na Mikongo hiyo ya mawasiliano siyo chaguo. Hivyo kuwasilishwa kwa Azimio la Bunge la kuridhia kwa itifaki ya mawasiliano ya *NEPAD* ni ushahidi tosha wa dhamira safi ya Serikali ya kujenga miundombinu ya huduma za mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza na kuishukuru kwa dhati Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Kusini kwa kazi nzuri iliyofanya ya kuchambua maudhui ya itifaki hii na hatimaye kuyaafiki. Aidha, naishukuru sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa Azimio la Bunge la kuridhia itifaki hiyo ya *NEPAD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya sasa naomba niwasilishe Azimio lenyewe kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya *NEPAD* kuhusu mwongozo wa Sera na Usimamizi wa Ujenzo wa mkongo wa teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

KWA KUWA mwezi Machi, 2003 Viongozi wakuu wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (*AU*) walipitisha mpango wa *The New Partnership for Africa Development* kwa kifupi *NEPAD*, kwa madhumuni ya kutekeleza programu ya kujenga miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA);

NA KWA KUWA TEKNOHAMA inalenga katika kukamilisha na kuendeleza miundombinu kwa kujenga mikongo ya baharini inayozunguka Bara la Afrika na mkongo wa nchi kavu na hivyo kuziunganisha nchi zote za Afrika na pia kuliunganisha Bara la Afrika na nchi nyingine duniani;

NA KWA KUWA juhudii hizi zinaendeleza shughuli za ujenzi wa jamii habari kwa kutandazwa mkongo wa mawasiliano wa baharini katika ukanda wa Pwani wa nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika utakaouniganisha nchi zote wanachama wa Umoja wa Afrika kupitia Mikongo ya ndani ya nchi zao na hivyo kuwezesha:-

- (1) Kuimarika kwa huduma za mawasiliano ya ndani na nje ya nchi.
- (2) Kupungua kwa gharama za huduma za mawasiliano kutokana na kuongezeka kwa mitandao ilio bora na yenyewe nguvu hivyo kuwawezesha wananchi wengi kumudu gharama za huduma za mawasiliano ikilinganishwa na hali ilivyo sasa.
- (3) Kufungua njia kuu ya mawasiliano kwa nchi za nje na hivyo kuwezesha Tanzania kupata mapato kwa kutoa huduma hiyo.
- (4) Kupanuka na kuongezeka kwa shughuli za kibiashara za kiuchumi na kijamii na hivyo kuchochea mapambano dhidi ya umaskini.

NA KWA KUWA Sura ya Kumi ya Itifaki hii inaeleza taratibu za kuridhia na kuidhinisha itifaki hiyo ya *NEPAD* hivyo basi kwa kuzingatia umuhimu wa itifaki ya *NEPAD* hususan manufaa ambayo wananchi wa Tanzania watapata endapo mpango wa *NEPAD* utaanza kutumika nchini na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya 2 ya Sheria za nchi;

KWA HIYO BASI Bunge hili katika Mkutano wa Tisa sasa linaazimia kuridhia itifaki ya *NEPAD* kuhusu Mwongozo wa Sera na Usimamizi wa ujenzi wa mkongo wa TEKNOHAMA wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika ya mwaka 2006 (*The Protocol on the Policy and Regulatory Framework for NEPAD ICT broadband infrastructure for Eastern and Southern Africa 2006*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na kuungwa mkono sasa naomba nimwite msemajii wa Kamati ya Miundombinu aweze kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya karibu.

**MHE. SULEIMAN OMAR KUMCHAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya kimataifa iliyowasilishwa na Wizara ya Miundombinu.

Lakini kabla sijaanza kutoa taarifa hiyo ningependa kuchukua nafasi hii kuwapa pole wale wote waliofiwa tukiwemo sisi Wabunge, kwa kuondokewa na mwenzetu Mheshimiwa Salome J. Mbatia. Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi, *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuwapa pole wote ambao wamepatwa na ajali wakiwemo Waziri wetu wa Ulinzi Mheshimiwa Juma A. Kapuya na Ndugu yetu Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ambaye amepoteza mkono wake.

Natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi.

Napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Makamu wetu wa Rais Dr. Ally Mohamed Shein, kwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu wa Chama cha Mapinduzi. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Vilevile nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ndugu yetu Mheshimiwa Edward N. Lowassa, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi. Pia nawapongeza Wajumbe wote waliochaguliwa pamoja na Wabunge wenzenetu ambao wamepata nafasi hii ya kuchaguliwa kuwa Wajumbe wa Halmashauri ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bunge litajadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano ambayo kwa masharti yake inapaswa kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyeiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 88 (9), Toleo la Mwaka 2004, Kamati ya Bunge ya Miundombinu ilipata fursa ya kupitia Itifaki iliyowasilishwa na Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mb., Waziri wa Miundombinu mbele ya Kamati ili kujadiliwa na kupata maoni na Ushauri wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kujadili na kuridhia Itifaki na makubaliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki iliyopitiwa na Kamati ni *New Economic Partnership for Africa's Development (NEPAD)* inayohusu mwongozo wa sera na usimamizi wa ujenzi wa Mkongo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika ambao unalenga kukamilisha na kuendeleza miundombinu kwa kujenga mikongo ya baharini inayolizunguka Bara la Afrika na hivyo kuliunganisha na nchi nyingine duniani (*The Protocol on Policy and Regulatory Framework for the NEPAD, ICT, Broadband, Infrastructure for Eastern and Southern Africa, 2006*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 88 (9), Toleo la 2004, sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la kuridhia Itifaki ya Kimataifa iliyowasilishwa na Serikali kama ilivyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi zake zilizoleta manufaa makubwa kwa Taifa letu. Aidha, Kamati pia inatambua kuwa haki ya kupata mawasiliano mionganini mwa wananchi ni wajibu wa msingi kwa Serikali yoyote na ni mahitaji ya kikatiba. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali ifanye kila linalowezekana ili Itifaki zenye manufaa ya Taifa letu kama hii ziwe zinaridhiwa na Bunge lako Tukufu mapema na kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha miaka mingi sasa wananchi wamekuwa wakilalamika kuhusu gharama kubwa wanazotozwa na wanaotoa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi. Matumizi ya kuanza kutumia mkongo wa aina hii badala ya *satellite* ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wetu na hasa wanaoishi katika maeneo ya vijiji na wale wanye kipato kidogo. Pamoja na kwamba Serikali imechelewa kuridhia Itifaki ya kimataifa ya mwaka 2006 inayohusu mwongozo wa Sera na Usimamizi wa ujenzi wa Mkongo wa TEKNOHAMA wa Kanda ya Afrika na Kusini mwa Afrika (*The Protocol on Policy and Regulatory Framework for NEPAD, ICT, Broadband, Infrastructure for Eastern and Southern Africa 2006*) bado umuhimu wake ni mkubwa kwa ajili ya kuboresha huduma za mawasiliano na kuongeza tija. Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu mzuri utakaowezesha utekelezaji wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inaishauri Serikali itenye bajeti ya kutosha itakayowezesha Itifaki inayoridhiwa kutekeleza kwa urahisi na hivyo kufungua wigo wa ushirikiano wa Kimataifa katika uchumi na uwekezaji. Vilevile Kamati inaishauri Serikali idumishe ushirikiano na nchi nyingine wanachama wa Umoja wa Afrika katika kutoa mafunzo ya kisayansi na kiteknolojia kwa wananchi wake juu ya umuhimu wa utekelezaji wa mpango huu wa *NEPAD* katika kuendeleza miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Kamati inayapongeza kwa dhati makampuni ya ZANTEL, TTCL na SATCOM kwa kuwa mstari wa mbele katika kusaini mkataba wa makubaliano (*Memorandum of Understanding*) na makampuni mengine ya ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika unaolezea jinsi watakavyoshiriki katika kutekeleza Itifaki hiyo. Kwa kuwa mafanikio ya Itifaki hii yatategemea sana jinsi miundombinu ya

mawasiliano itakavyokuwa imeandaliwa na kuleta unafuu kwa watumiaji wa huduma hii, Serikali itoe kipaumbele katika kueneza mtandao wa mkono (*optic fibre*) katika maeneo ya nchi pamoja na ile inayounganisha nchi za nje na hasa za majirani kwa minajili ya kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuridhia itifaki hii bado Kamati inaishauri Serikali isimamie vizuri utekelezaji wake ili wale wenye nia mbaya ya kuendelea kuwatoza wananchi gharama kubwa za mawasiliano wadhibitiwe. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuititia watalaaamu wake kuangalia itifaki zote za kimataifa ambazo Tanzania bado haijaridhia iwapo zina manufaa kwa maendeleo ya nchi na watu wake, itifaki hizo ziwasilishwe Bungeni ili Bunge lako Tukufu liweze kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, namshukuru Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mb., Waziri wa Miundombinu pamoja na Watendaji wote wa Wizara yake kwa kuwasilisha Azimio hili kwa ufasaha jambo ambalo limerahisisha kazi kwa Kamati yangu. Pia naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa ushirikiano wao pamoja na moyo wa kujitoa katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Napenda kuwatambua kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Joyce Massunga, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Ephrahim Madeje, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Masolwa Masolwa, Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Mwaka Ramadhani, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Hafidh A. Tahir na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Justina Shauri, Ndugu Zainab Issa na Ndugu Michael Chikokoto, kwa kuihudumia vema Kamati na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni na ushauri huo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ya Miundombinu imejadili Azimio hili na kwamba limezingatia mahitaji ya nchi. Kwa hiyo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu kujadili na kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Kumchaya kwa uwasilishaji wako wa maoni ya Kamati kuhusiana na Azimio hilo. Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Bakari Shamis Faki.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI – MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii kutoa Maoni ya Upinzani kuhusu Azimio lililo mbele yako kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 43(5)(c), Tolea la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inadhani kuwa mwonekano wa Azimio hili ni mzuri, hata hivyo, kuna maswali kadhaa ya kujiuliza kwa lengo la kulinda maslahi ya nchi yetu.

Mpango wowote ni lazima kwanza ulinde maslahi ya taifa letu. Uzoefu tuliuopata ni kuwa katika miradi mikubwa na hasa inayohusisha makampuni makubwa mara nydingi kuna ajenda zilizojificha zinazokwu na athari kwa taifa moja moja kama Taifa halitakuwa makini katika maandalizi. Mpango huu wa *ICT Broadband* unasimamiwa na *NEPAD* ambayo iko chini ya Umoja wa Afrika (*AU*). Lakini watekelezaji wake na watoa fedha ni vyombo vya kimataifa ambao nao wanalinda maslahi yao na nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkongo huu wa TEKNOHAMA, *ICT Broadband* katika utekelezaji unasimamiwa na Serikali ya Afrika Kusini kwa niaba ya Mamlaka ya *NEPAD*. Kambi ya Upinzani kimsingi haina tatizo kama mpango huu ungelikuwa unasimamiwa moja kwa moja na Serikali ya Afrika Kusini, mashaka yetu ni pale makampuni binafsi ya Afrika Kusini yanapokuwa ndiyo wasimamizi wakuu na bila udhibiti wowote wa mamlaka na watalamu wa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiumwa na nyoka hata jani ni lazima uliogope. Yaliyotupata Tanzania katika ushirikiano na makampuni ya Afrika Kusini mathalani ushirikiano kati ya *ATC* na *SA* au migogoro na migongano iliyokuwepo katika Shirika letu la *NDC* baada ya kuchukuliwa na *ABSA* na *AFGEM* au hata na *TLB* ambao kama tunavyofahamu kuna wakati ilifika hata chupa za kuweka bia zililetwa kutoka Afrika Kusini wakati Tanzania ina kwanda cha kutengeneza chupa. Matokeo ni viwanda vya kwetu kuuliwa mbali, ajira zetu kupotea na hata ujuzi wa Tanzania katika makampuni yaliyofungwa kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu huu unatutaka tuwe waangalifu sana katika kuingia mikataba ya aina hiyo ambayo hatuna Mamlaka na usimamizi wa moja kwa moja. Na kwa kuangalia Tume ya *NEPAD* inayoshughulikia suala hili makao yake makuu yako Afrika Kusini katika Mjini wa Pretoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake katika Kamati ya Miundombinu alieleza kuwa Afrika Kusini iko tayari hata kubeba gharama ya ziada ya mpango huu. Ni vema tusibweteke na hali hii kwani cha bure kinaweza kuwa na

gharama kubwa zaidi au kutokana na masharti yatakavyokuwa au kwa vyovoyote itakavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mawasiliano ndiyo sekta ambayo inatoa mchango mkubwa katika dhama nzima ya kupiga vita umaskini na ni dhahiri kuwa Afrika Kusini kwa kutambua umuhimu huo inakuwa tayari hata kubeba gharama za ziada. Wanafahamu fika manufaa yake kwao; je, ni kwa kiasi gani Tanzania tumefanya tathmini ya manufaa na athari ya mpango huu kwetu? Kambi ya Upinzani inaona ingelikuwa vema Serikali yetu kabla ya kuridhia jambo hili kwanza ifanye upembuzi yakinifu kwa kutumia watalaamu wake na kufanya mawasiliano ya karibu na wenzetu mathalani Wakenya kuangalia ni jinsi gani nchi hizi zitafanikisha na kunufaika na Azimio hili.

Aidha, jambo lingine la kuijuliza ni kwa nini wenzetu Wakenya siyo tu kwamba hawajaridhia Azimio hili bali hata kuweka saini bado hawajaweka hadi leo hii. Kambi ya Upinzani inapenda Waziri alieleze Bunge hili kwa urefu na upana majirani zetu hawa wameona nini kiasi cha kusita kuweka saini jambo hili ambalo kwa nje linaoneka lenye neema na heri na sasa wanajenga mkongo wao kutoka Mombasa kwenda Djibout.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa miundombinu itakayotumika katika zoezi zima la kutandaza mkongo huu itahusisha Serikali za nchi wanachama; je, uhushishwaji wa Sekta Binafsi uko wapi? Na kwa wale watakaohusishwa umiliki utakuwaje? Kampuni zote hata zile ambazo hazikushirikishwa katika zoezi zima la kutayarisha miundombinu hiyo zitakuwa na haki sawa katika matumizi ya mkongo huo? Jambo hili ni vema likapata maelezo ya kina hasa ikizingatiwa kuwa kwa sasa nchi yetu inatekeleza sera ya biashara huria na sekta ya mawasiliano nayo imeshaingia katika biashara huria (*liberalization*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na wasiwasi wa kupatikana kwa mazingira sawa ya utendaji katika biashara kutokana na hali inayoweza kujitokeza kwa wale watakaokuwa *special purpose vehicles* ambazo kwa maana nydingine ni makampuni ambayo yatapewa haki maalumu na Serikali husika ya kushughulikia suala hili au kwa maana nydingine zitapewa *golden share and vital power* katika biashara ya ushindani katika soko huria. Mkataba huu haukuweka wazi suala la makampuni yanayotoa huduma ya mashindano kwa nchi wanachama. Kuwepo na *open access* kwa wale wote wakaotumia mkongo huu. Hii kama haitawekwa wazi ushindani wa kibiashara utakuwa hatarini na dhana nzima ya ushindani sawa haitakuwepo katika tasnia hii ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania kuridhia mkataba huu maana yake itatubidi kama nchi kurekebisha Sheria zetu zinazohusiana na sekta nzima ya utoaji leseni na usimamizi mzima wa Sekta ya mawasiliano. Maana yake ni kurekebisha Sheria ya uuanzishwaji wa Tume ya Mawasiliano, vinginevyo Mheshimiwa Waziri atueleze hali halisi itakavyokuwa baada ya kuridhia mkataba huo. Kambi ya Upinzani inaona kwamba kama hali itakuwa kama ilivyo kwenye mkataba, nchi yetu inaweka rehani uhuru wake kwani inatakiwa Sheria kama hizo ziende sambamba na Sheria zetu tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema pia Mheshimiwa Waziri akalileleza Bunge lako ni kwa kiasi gani Serikali imefanya mashauriano ya kina na wadau mbalimbali wa sekta ya mawasiliano kupata maoni ya ushauri wao. Wadau ndiyo watu muhimu na hivyo Serikali haipaswi kusukumwa tu na mikataba na protokali za kikanda pale ambapo protokali hizo zinaweza kuwa na athari za kina kwa wadau wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye mtandao kuna hisia kuwa tukisharidhia mkataba huu kuna hatari makampuni yaliyokwishapewa leseni yatapaswa kuondolewa leseni zao na kuwekwa chini ya Mamlaka itakayokuwa inadhibitiwa kutoka nje ya nchi. Hii ina maana kuwa hata *TCRA* itakuwa inanyimwa mapato yake. Kambi ya Upinzani inapenda kupata maelezo ya kina kuhusu hali hii. Makao Makuu na leseni ya mkongo huu na udhibiti wake yatakuwa wapi? Na udhibiti wake utakuwa katika nchi ipi? Athari ya hali hiyo ni nini kwa Tanzania? Tanzania ilikwishafikia hatua nzuri katika kutengeneza mazingira ya kuwavutia wawekezaji. Je, athari ya hatua hiyo nini kwa wawekezaji wa Sekta ya Mawasiliano ambao wanavutiwa na mazingira ya Tanzania ambayo baada ya mkataba huu hayatakuwepo tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu moja inayotoka kwa wadau kama ilivyo kwenye mtandao ni kuwa kuridhiwa kwa mkataba huu kutafanya kitu kinachoitwa *State lead operating entities or specialized vehicles consisting of Government Representatives who command golden and vital power*. Je, hali hii imefanyiwa tathmini ya kina? Na je, kukubali kichwa kichwa katika mkataba huu siyo kwenda kinyume na sera ya Tanzania ya Biashara Huria kama ilivyo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapenda kufahamu tofauti kati ya *ICT Broadband* iliyozungumziwa na *Broadband* inayotumika hivi sasa Tanzania kama vile *Broadband* ya *TTCL* ambayo tayari imekwisharahisisha sana mawasiliano katika sehemu mbalimbli za nchi yetu. Je, Mkataba huu utakuwa na athari gani kwa mpango wetu unaotekelawa na *TTCL* ambao hivi sasa uko katika hatua ya kupanuka karibu nchi nzima? Kwenye mtandao wadau wengi inasemekana wameshauri kuwa Tanzania isiridhie mkataba huu katika umbo lake la sasa hadi madhara yake kwa Tanzania yamechambuliwa kwa kina. Je, Serikali inatoa tamko gani katika jambo hili linaloweza kuathiri maendeleo ya sekta ya mawasiliano katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuwa makini sana katika kuchunga maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Shamis Bakar Faki kwa kutuwasilishia maoni ya Kambi ya Upinzani. Waheshimiwa Wabunge Azimio hili halina mchangiaji hata mmoja. Kwa kuwa halina mchangiaji hata mmoja, sasa namwita mtoa hoja kama ana neno lolote la kuongeza ili ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Waziri tafadhali!

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii niweze kuhitimisha hoja yangu kwa kifupi sana. Niwashukuru sana Mheshimiwa Suleiman Kumchaya kwa kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu na Mheshimiwa Shamis Bakar Faki, Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Naishukuru sana Kamati ya Miundombinu, wameielewa hoja vizuri sana na wanawakilisha mawazo ya Watanzania walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumedhamiria kama nilivyosema, Serikali ya Tanzania na zile nchi ambazo ni waasisi wa mradi huu, lakini pia ambazo zimeshasaini Mkatuba huu zimedhamiria kabisa kujenga mkongo huu. Hisia za Kambi ya Upinzani tunazichukua ni hisia tu. Tunataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa nchi hizi si mbumbumbu, Tanzania tunaelewa tunachokifanya. Mimi siwezi kusemea maslahi ya Kenya, naweza kusemea maslahi ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri haya yanayosemwa tukayaelewa katika *proper perspective*. Itifaki hii hata kama unataka kuyafanya haya ambayo Kambi ya Upinzani inayasema, lazima kwanza ianze kutumika na ndiyo maana nchi hizi zinahangaika kupata akidi ili itifaki ianze kutumika. Sasa itakapoanza kutumika ndiyo mnajipanga, misingi ambayo imo katika *protocol* hii je, inatosheleza au ina vitu vingine ambavyo wengine haviwapatii usingizi? Sasa ukifikisha hapo kama wewe ni nchi huru, ukiona maslahi yako hayajazingatiwa kikamilifu utasema, *exit clause* ipo, utajiondoa. Tanzania na wenzetu ndio tumekuwa tunawaambia hoja hiyo kwamba haiwezekani, kwa sasa hivi hata ungekuwa na mawazo mazuri sana huwezi kuirekebisha protokoli hii kwa sababu haijaanza kutumika, ianze kutumika ndiyo utaanza kujenga hoja zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti na NEPAD pamoja na sisi nchi wanachama kwa Ukanda huu wa Afrika Mashariki tumekuwa tunapata ushauri mzuri sana *technical*. Kwanza tuna chombo kizuri sana TCRA, mimi napenda kuipongeza sana kwa kazi nzuri ambayo inafanya. Tuna wataalamu wazuri waliobobeaa sana kwenye masuala haya.

Tusiogope kama kwamba tunakwenda kichwa kichwa hapana! Sasa ni kweli nilielezea Serikali ya Afrika Kusini imesema mchango wake na yenyewe inaweza kufanya hiyo. Fursa ni fursa ikitolewa siyo lazima uitumie, utaangalia kama kweli mchango wao wanaotoa unawapelekeni katika kuimarisha chombo hiki au wanataka kujenga nafasi yao ya kipekee katika mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau katika sekta hii tumeongea nao sana na ndiyo maana makampuni haya matatu ya Tanzania, ZANTEL, TTCL yenyewe na SATCOM walisaini *memorandum of understanding*. Sasa huwezi kumlazimisha Vodacom kama hataki lakini mradi huu utakapokamilika, kwa sababu sasa hivi wao wanatumia *satellite*, ni gharama kubwa sana ukilinganisha na hii teknolojia inayokuja, tunajua na wao wanajua kupiga mahesabu, watachagua teknolojia ile ambayo inawaleta *bottom line* nzuri kwa faida sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria. Kwanza, katika mtazamo wa *East Africa* tuna *check list* ya masuala haya. Tumekwishafanya yote na Tanzania ndiyo inaongoza katika kuwa na Sheria ambazo zimekaa vizuri, ndiyo maana wanakuja kujifunza kwetu. Tusiwe na wasiwasi kwa suala hili, hawatubabaishi, ndiyo maana tunatembea kifua mbele, ukimwona Profesa Nkoma na timu yake tunakwenda kwenye vikao hivi wanaeleza mpaka watu wanasesma, hebu rudia tena. Sasa tumefikia hatua nzuri, unapokuwa *with a converged licensing system* kama ya Tanzania haya maswali yanayouлизwa yaliyomo kwenye *statement* hii, kusema kweli wala hayana nguvu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SPV* au *High breed SPV* hawa watakuwa na *veto*. Hili sijui linatoka wapi, utakuwaje na *veto* kwenye chombo ambacho siyo cha kwako, wewe umepewa kazi ya kujenga kukiendesha na kusimamia. Kuna kile chombo cha juu ya *inter-governmental*, uwakilishi wa wenyе sera maana mkongo huu sisi tunauona kama wa ukombozi na ndiyo maana wameuita uhuru, ulikuwa unaitwa *easy project*. Sasa wamesema tuuite uhuru kwa sababu mwaka huu ni mwaka wa 50 tangu Bara la Afrika lianze kujiondoa katika mnyororo wa ukoloni na wametumia Kiswahili kwa sababu wanasesma hii ndiyo lugha ambayo inatuunganisha sasa Afrika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkongo wa nchi kavu watauila umoja kwa sababu tunafanya kazi ya umoja na kampuni mama itakayoshikilia hii inaitwa *baharicom* kwa sababu mkongo huu utawekwa baharini. Kwa hiyo, Kiswahili ndiyo sasa kinaanza kuchemka kweli kweli. Lakini katika maelezo yangu nimesema kwamba kuna misingi ambayo ni ya wazi sana katika yule anayetaka kuunganishwa katika mfumo huu wa mkongo wa baharini kwenda kwenye mkongo wa nchi kavu au *vice-versa*, kwanza misingi imewekwa hakuna ubaguzi kabisa, yule anayetaka kutumia atatumia sawasawa na wengine, kwa hiyo, hata wale ambao hawamo katika *MOU*, wakitaka na wenyewe watapata fursa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tumelewsima ni *principle* ya *open access* na ndiyo ya msingi sana katika shughuli hizi. Kwa hiyo, mimi niwaondolee wasiwasi Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu kwa haya ambayo yamesemwa na porojo nyingi ambazo zinapita kwenye mtandao. Pengine ni kutaka kutishia tu kwamba mbaki nyuma kwa sababu wananaufaika sana na mfumo huu wa *satellite*, lakini hata kwa upande wa biashara tu kwa upande wa *private sector*, napenda kutoa taarifa rasmi kwamba Kampuni ya Kimarekani inafahamika kama *Seacom* ambayo imekwishafanya ukaguzi wa njia kuanzia *South Africa* mpaka *point* ya kuingia kwenye *Suez Canal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wamelewana na Serikali ya Afrika Kusini, mahali ambapo wataingiza *line* yao ile *landing station* yao na mchana huu Meneja wa mradi huo amenipigia simu akasema katika miezi miwili ijayo wataanza kutandaza au kulaza baharini ule waya na kwa upande wa Tanzania *landing station* ambayo Serikali ya Tanzania tumewapatia ni *White Sands* katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tuna sababu ya msingi kwa nini tumechagua *site* hiyo kwa sababu kwetu tunataka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinufaika sana na teknolojia hii. Lakini hiyo ndiyo *private sector* inafanya hivyo. Tunaousemea sisi ni huu ambao malengo yake ni ya maendeleo na kama nilivyosema nilieleza kwenye Bunge hili na walionitangulia wamekuwa wakilieleza

kwamba lengo letu katika kujenga huu mkongo wa nchi kavu, ni kwa sababu tunataka hii teknolojia ifike kwa kuanzia katika Wilaya zetu zote. Hatutaki eneo moja la Tanzania lijisikie kama kwamba limesahaulika na kwa bahati nzuri tunaanza vizuri kwa sababu tuna makampuni ya umma ambayo tayari yana *excess capacity* ya teknolojia ya *fibre optic*, tunayafahamu. Kwa hiyo, tunaanza vizuri, tunakuja kuongezea tu, tunajenga huu wa ndani utakuwa na urefu wa kilomita 6500 na njia tumekwishaikagua, tunajua na tutaunganisha mpaka Zanzibar na Pemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, nimewasumbua sana na sauti yangu mbaya kidogo, lakini nitatafuta dawa leo jioni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Azimio la Kuridhia Itifaki ya NEPAD kuhusu Mwongozo wa Sera na Udhibiti wa Ujenzi wa Mkongo wa Teknohama lilipitishwa na Bunge*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoweza kutoa ufanuzi wa kina kabisa ingawa hakukuwa na hoja yoyote kutoka kwa mchangaji yejote kutoka hapa ndani. Kwa kweli naomba nikupongeze sana. Sasa hoja imetolewa na imeungwa mkono, kwa hiyo, na mimi sasa nitawahoji kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhuria Itifaki ya NEPAD kuhusu Mwongozo wa Sera na Udhibiti wa Ujenzi wa Mkongo wa Teknohama wa Kanda ya Afrika ya Mashariki na Kusini.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, sasa naomba niseme kwamba shughuli zilizopangwa leo hapa mezani tumezimaliza zote na kwa kweli nawapongeza sana. Leo tumekuwa na kazi nzito, hatukujitambua lakini tumekuwa na kazi nyingi sana. Tumelazimika kuitisha Maazimio matatu, lakini tumekuwa na Muswada mmoja na tumekuwa na kipindi cha maswali na majibu. Hata nilikuwa nina hofu kweli kama tungeweza kumaliza shughuli hizi na kama tunavyojua kesho tutakuwa na hotuba ya Waziri Mkuu ya kuhitimisha shughuli zetu za Mkutano huu wa Bunge. Kwa hiyo, nawashukuruni, nawapongeza kwa ushirikiano na hasa kwa kuweza kufanikisha kumaliza shughuli zote za leo katika muda hasa amba tulikuwa tunahitaji kufikia.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo na kumaliza shughuli hizi, basi nitakuwa sina ajenda nyingine tena mezani wala sina tangazo lolote, naomba sasa nahirishe shughuli zote za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya Ukumbi wa Bunge.

(*Saa. 1.45 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 15 Novemba, 2007, Saa 3.00 Asubuhi*)

